**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MKUTANO WA NANE**

---

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 7 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. MOHAMED ALI SOUD (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 365

**Uhitaji wa Soko la Kimataifa Holili**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU (K.n.y. MHE. ALOYCE B. KIMARO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Vunjo wanafanya biashara ndogo ndogo na Kenya kupitia kwenye soko la Taveta:-

Je, Serikali itakubali sasa kuanzisha soko la kimataifa karibu na mpaka wa Holili ili wananchi wa Kenya waweze kuja kununua bidhaa zetu zikiwemo za kilimo badala ya Watanzania kwenda Kenya kupeleka bidhaa hasa zile za kilimo kwa magendo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Beti Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikubaliane na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kuhusu shughuli za biashara ndogo ndogo zinazofanywa kupitia soko la Taveta pamoja na ushauri wake wa kuanzisha soko la kimataifa karibu na eneo la mpakani la Holili lililoko katika Wilaya ya Rombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile jukumu la kuanzishwa na kuendeleza masoko ni la Mamlaka za Serkali za Mitaa katika eneo husika, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo inaweza kushirikishwa na wazo hili zuri la Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, kwa kuzingatia azma hiyo ya kuwa na soko la kimataifa huko Holili Halmashauri ya Wilaya ya Rombo inashauriwa iangalie uwezekano wa kuingiza mradi wa ujenzi wa soko hilo katika mipango yake ya Wilaya.

Kwa upande wake Serikali itakuwa tayari kushirikiana nao katika kutafuta uwezo wa utekelezaji wa mradi huo kwa kupitia fursa mbalimbali kama vile programu ya kuendeleza mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo nchini *(AMSDP)* inayotekelezwa katika Wilaya 37 hapa nchini zikiwemo Wilaya za Rombo na Moshi Vijijini ambazo zinaweza kuhudumiwa na soko hilo iwapo litaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kupitia programu hiyo ya kuendeleza masoko, hivi sasa tayari Wilaya ya Rombo imeanzisha ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la Tarakea litakalogharimu shilingi milioni 277.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Serikali kwamba soko hilo likianzishwa na kukamilika litawawezesha wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mikoa ya nchi jirani kufanya biashara zao kwa manufaa kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa nguvu ya wananchi wa Halmashauri ya Vunjo haijaweza kabisa kufikia uwezo wa wao kuwa na soko la kimataifa ambalo Mheshimiwa Mbunge analiulizia. Na kwa kuwa hili soko kimsingi litashindanisha nchi mbili kati ya Kenya na Tanzania na

kuwafaidisha wakulima wa Tanzania ambao kimsingi watauza mazao katika nchi jirani ya Kenya. Je, Serikali haioni umuhimu wa kulifanya hili soko liwe soko la kitaifa na kwa hiyo kuweka fedha ambazo itasaidia wananchi wa Vunjo kuwa na soko ambalo lina hadhi kubwa na linaweza likashindana kabisa na wenzetu wa Kenya?

Swali la pili. Kwa kuwa tatizo la soko ni tatizo la nchi nzima na kuna maeneo mengi muhimu sana kama eneo la Ilongero katika Jimbo la Singida Kaskazini. Eneo la Ilongero lina mazao ya asilimia ya gilagilani, alizeti na ufuta, mazao ya karanga na mazao muhimu ya wanyama na mifugo na wananchi hawa muda mrefu sana wameomba kupatiwa soko la kimataifa na hadi sasa hivi Ilongero wana soko dogo tu ambalo linaweza kukidhi mahitaji ya Kata ya Ilongero na kidogo Tarafa ya Ilongero.

Je, Serikali haiko tayari sasa kuungana na wananchi wa Tarafa ya Ilongero kuweza kujenga soko kubwa kabisa la kimataifa kwa ajili ya kukidhi mahitaji hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa masoko haya ambayo Mheshimiwa Mbunge muuliza swali la msingi ameongelea pamoja na haya ya nyongeza ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaulizia. Kutokana na umuhimu huo ndiyo maana Serikali mara zote inazidi kushauri kwamba mipango hii ianzishwe kule kwenye Halmashauri za Wilaya kwa sababu wao ndio watakuwa na jukumu la kuyaendeleza masoko hayo na kuyasimamia.

Endapo mipango hiyo itakuwa imeanzishiwa kutoka huko Serikali haitasita kuwatafutia wadau wa Maendeleo ambao wanaweza kushirikiana nao kama ambavyo nimetoa maelezo hapa kwamba lile soko ambalo limeanzishwa Tarakea hivi karibuni linachangiwa pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Kule Ilongero alikokusema Mheshimiwa Mbunge mimi mwenyewe nilishatembelea huko pamoja na Iguguno ambako kwa kweli nilitoa ushauri pale pale kwamba kun a haja ya masoko inajionyesha wazi wazi isipokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba pamoja na ya Singida kwa sasa hivi kwa Iguguno wakiyaibua hayo tunaweza tukashirikiana nao.

**NAIBU SPIKA** Kuhusu soko la kimataifa la ng'ombe Mheshimiwa Telele. *(Kicheko)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuniona na kunipa nafasi. Kwa kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Kimaro kuhusu biashara kule mpakani na nchi jirani ya Kenya. Yeye amezungumzia biashara inayotokana na mazao ya kilimo. Lakini kule Ngorongoro sehemu za Angaresero, kuna mifugo mingi sana kutoka Shinyanga, Mwanza, Ngorongoro kwenyewe, Mkoa wa Mara, inapita huko kwenda Kenya. Ni lini Serikali inaweza ikaanzisha mnada mkubwa kwa ajili ya mifugo ili kuzuia hii mifugo isiendelee kwenda Kenya na kunufaisha Wakenya kwa upande wa uchumi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika kujibu swali la msingi nilijikita zaidi katika masoko ya mazao ya kilimo ambayo kwa kweli ilikuwa ndiyo msingi wa swali lenyewe.

Lakini napenda nikubaliane naye pia kwamba iko haja kubwa kabisa ya kuanzisha minada mikubwa kwa maana ya kuhudumia mifugo ambayo mimi naamini kabisa kwamba wenzetu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo walipokuwa wanawasilisha hotuba ya Makadirio yao hapa ni moja ya mipango ambayo wameielezea. Naamini kwamba Serikali itashirikiana nao kuhakikisha kwamba masoko ya minada ya mifugo nayo yanatiliwa maanani.

**NAIBU SPIKA:** Kwa upendeleo maalum Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ambaye kwa muda mrefu alikuwa mgonjwa. Sasa amepona, na yeye alete soko, Profesa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naongeza majibu swali la Mheshimiwa Kaika Telele. Kuhusu uwepo wa mnada kwa ajili ya wafugaji na mifugo inayouzwa nchi jirani kwa eneo la mpakani Wilaya ya Ngorongoro. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tayari kuna mnada wa mpakani wa Wasso kule Ngorongoro ambao unatumika kwa ajili ya biashara ya mifugo kwa nchi yetu na nchi jirani.

Napenda kutoa wito kwa wananchi wa Ngorongoro na wafuji wote wanaotumia au wanaopaswa kutumia mnada huo kuutumia kikamilifu ili kuimarisha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na jirani ya Kenya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa nimeisha mwita Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na yeye soko la kimataifa la mahindi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya upendeleo na kwa Wabunge wenzangu kuweza kutambua kuwepo kwangu hapa baada ya kuugua kwa muda. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile swali la msingi linahusu masoko haya ya kimataifa. Napenda kushukuru Wizara kwa kujenga soko moja la kimataifa kwa mpango wa *ASDP* pale Mlangali katika Wilaya ya Ludewa ambalo kwa sasa limeshakamilika, limekwisha, limekamilika sasa swali. Ni kwamba kwa vile msimu wa kuuza mahindi hasa mahindi kule Ludewa ambayo ni wilaya inayolima sana mahindi ndio unakaribia.

Mheshimiwa Naibu Spika, isingekuwa vema utaratibu ukafanywa soko lile likazinduliwe upesi haraka iwezekanavyo kusudi wananchi waweze kuanza kulitumia kuuza mahindi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa pole kwa kuugua lakini vile vile nitoe faraja kubwa kwa kurudi kwake hapa yuko salama. Namwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuijalia afya yake. Baada ya hayo nataka tu nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza tunapokea shukrani zake alizozitoa kwa ajili ya soko la Mlangali ambalo tumeshirikiana naye kwa karibu sana mpaka hivi sasa limekamilika. Kwa hiyo, ombi lake la kulianzisha soko hilo haraka iwezekanavyo, nakubaliana naye kwamba tutaangalia uwezekano wa kuhakikisha kwamba soko hilo linafanya kazi mara moja.

Na. 366

**Chanzo cha Maji**

**MHE. SAID A. ARFI** alijibu:-

Je, ni nini maana ya chanzo cha maji, na watu wanatakiwa wakae umbali gani kutoka katika chanzo cha maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha maji ni eneo lote lenye kuhifadhi ama kutiririsha maji juu ama chini ya ardhi kwa kiwango kinachoweza kutumika kwa matumizi mbalimbali. Kuna aina ya vyanzo vya maji vingi kama vile chemchem, vijito, mito, malambo, mabwawa, maziwa, bahari na maji chini ya ardhi. Wingi na ubora wa maji katika vyanzo hivyo hutegemea sana hali ya mazingira yanayokizunguka chanzo husika kama vile misitu, miamba, udongo, uoto wa asili na viumbe hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Maji *Cap. 331* ya mwaka 2002 kifungu namba 8 hairuhusiwi kuwa na shughuli za kudumu umbali usiopungua mita 200 kutoka katika kingo za vijito, mito na mita 500 kutoka katika kingo za maziwa na bahari. Aidha, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kifungu cha 57 (1) imetamka wazi kwamba hakutakuwa na shughuli zozote za kudumu za binadamu katika umbali usiopungua mita 60 kutoka katika kingo za vijito, mito, malambo, mabwawa, maziwa na bahari. Hivyo,

Waziri mwenye dhamana ya Mazingira ana wajibu wa kuweka taratibu za matumizi ya maeneo yaliyokatazwa kufanyika shughuli za kudumu. Kwa kuwa, Sheria ya Mazingira inakinzana na Sheria ya Maji kuhusu umbali unaoruhusiwa, Kifungu Na. 232 cha Sheria ya Mazingira kinaipa uwezo sheria hiyo kuamua juu ya umbali unaoruhusiwa wa mita 60 sanjari na Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 54 (2) cha Sheria ya Mazingira kinatoa nafasi kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazinigira kuangalia hali ya kijiografia, ukubwa wa mto au upana wa mwambao wa ziwa au bahari na kusikiliza mapendekezo ya wananchi kabla ya kulitangaza eneo la kingo za mto au ziwa kuwa ni eneo lililozuiliwa kufanya shughuli za kudumu. Kifungu cha 55(1) na (2) kinaagiza Baraza la Mazingira na Serikali za Mitaa husika kutoa miongozo katika eneo hilo kuhusu taratibu zitakazochukuliwa ili kuhifadhi maeneo ya vyanzo vya maji.

**MHE. SAID A. ARFI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa nataka kufahamu kwamba Sheria hii inatumika vijijini tu peke yake na si mijini kwa sababu nimeona watu wakijenga pembezoni mwa mto Mirongo kule Mwanza na pembezoni mwa mto Msimbazi kule Dar es Salaam kule Dar es Salaam na watu wa vijijini wanakatazwa kujenga karibu na mito? *(Makofi)*

Swali la pili, je Serikali inasemaje katika suala la kilimo cha umwagiliaji, wakulima wetu ambao hawana fursa za kupata mikopo ya kununua pampu za kusukuma maji, wanaolima pembezoni mwa vijito hivyo, kwa nini wanazuiliwa kuendelea na kilimo cha umwagiliaji pembezoni mwa mito inayozunguka katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza napenda kusema kwamba Sheria haibagui. Aliyoko mjini aliyoko kijijini, aliyoko popote pale sheria hizi za kuhusu matumizi ya maji na umbali gani hifadhi ifanyike zinahusika na yoyote yule. Kwa mfano ametoa kuhusu Mirongo huko Mwanza na Msimbazi Dar es Salaam kwamba watu wanalima kwenye hizo kingo. Hiyo ni kwamba wanakiuka sheria hizo na naomba kwamba Halmashauri za Wilaya husika wafuate taratibu zinazohusika na wachukue sheria zinazohusika na pia wazidi kutoa elimu kwa wananchi wote wafahamau kuhusu jambo hilo.

Swali la pili ambalo linahusu kilimo cha umwagiliaji. Napenda kusema katika taratibu za utumiaji wa maji, kuna kibali ambacho kila mtu anayetaka kutumia maji ya ziada zaidi ya maji ya kawaida ya kutumia majumbani ambayo wanalipa kufuatana na bili lakini maji ya ziada kwa shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji, na mambo mengine yoyote ni kwamba lazima mtu apate kibali cha kutumia maji hayo na pia katika kibali hicho atapimiwa kiwango gani atumie na atalipia kiwango hicho na nasema kwamba naomba kutoa tahadhari kwamba siyo kwamba chanzo chochote cha maji watu wakitumie tu kwa kumwagilia. Kwa sababu wakifanya hivyo ina maana kwamba kwa kuwa kile chanzo hakitumiki na wamwagiliaji peke yao kinatumika na watu mbalimbali jinsi kinavyoshuka kwenda sehemu zingine.

Kwa hiyo, watu wengine watashindwa kupata huduma ya hayo maji. Nasisitiza wanaomwagilia wawaone wahusika wa maji kwenye Ofisi zetu za Mabonde waweze kupewa vibali maalum na kiasi gani cha maji anayoweza akatumia. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza. Kabla sijauliza swali la nyongeza

ningependa sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya maji hapa nchini na hasa Naibu Waziri kwa sababu kila mahali palipo na matatizo ya maji kwa kweli amejitahidi kufika ili aweze kuelezea hali ya pale. *(Makofi)*

Swali, je, haingekuwa vizuri Wizara kutokana na umuhimu wa maji nchini na kazi nzuri inayofanywa na Wizara, wakatoa orodha ya miradi yote ya maji kabla ya Bunge hili halijaisha, wakaiorodhesha ili wananchi wajue kiasi gani Serikali inawajali katika suala hili la maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru kwa jinsi alivyotupa hongera Wizara yetu tunavyofanya kazi. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo napenda kusema kwamba tumepokea ushauri wake na tutafanya hivyo na pia tutajitahidi kila wakati kutangaza na watu waweze kufahamu miradi ya maji iko wapi na mradi gani, kijiji gani kinapewa maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 367

**Maji ya Bomba Jiji la Dar es Salaam**

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ya bomba yanayotumika Dar es Salaam huwa yana tope kiasi kwamba hayafai kufulia nguo nyeupe kwani hufifia:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupata Maji yasiyo na tope, safi na salama?

(b) Je, maji hayo sio chanzo cha magonjwa ya kipindupindu katika Jiji la Dar es Salaam yasiyoisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yanayotumika Jiji la Dar es Salaam yanatoka kwenye vyanzo vya Mto Ruvu, Mtoni na Visima mbalimbali vilivyoko Dar es Salaam. Maji hayo kabla ya kusambazwa husafishwa kwenye mitambo ya kutibu maji kwa vigezo vya viwango vinavyokubalika kimataifa.

Aidha, maji yanayosambazwa jijini huwekewa dawa ya kuulia wadudu na vimelea na kuyafanya kuwa salama kwa matumizi ya binadamu *DAWASCO* pia huhimiza wananchi kuchemsha maji ya kunywa, ili kuondoa uwezekano wa maambukizi, yanayotokana na uchafuzi wa maji yanapokuwa majumbani kwa wateja. Hata hivyo, kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusambaza maji, uchafu au tope huingia kwenye mabomba ya wateja kupitia kwenye mipasuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati wa kuendelea kutoa maji safi yasiyo na tope na salama kupitia mradi wa ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na uondoaji wa majitaka Dar es Salaam *(DWSSP)* ulioanza kutekelezwa mwaka 2003.

Mradi huu unahusu ukarabati wa mitambo ya uzalishaji maji ya Ruvu Juu, Ruvu Chini na Mtoni. Kubadilisha na kuongeza mabomba ya usambazaji, kuunganisha wateja 17,400, kupunguza uvujaji na uchakavu wa mabomba ili kuboresha huduma kwa wateja ambapo kila mteja ataunganishwa kwenye mtandao umbali usiozidi mita 30. Hii itaondoa kabisa uchafuzi wa maji unaosababishwa na kupasuka kwa mabomba yaliyounganishwa umbali mrefu. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2008.

Aidha, maabara kuu ya maji pamoja na *DAWASCO* huratibu usafi na ubora wa maji Dar es Salaam kwa kuchukua sampuli za maji maeneo mbalimbali 35 katika mtandao wa maji kila wiki ili kuona uchafuzi na kutoa tahadhari kwa wahusika na hata kuyatibu maji pale inapobidi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha kipindupindu sio maji yanayozalishwa na *DAWASCO* kwa sababu ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na vijidudu vinavyopatikana kwenye kinyesi cha binadamu.

Hivyo, kama wananchi hawatazingatia elimu ya afya na usafi wa mazingira watapata ugonjwa wa kipindupindu kwa kunywa maji yatokanayo na vyanzo visivyo salama kama vile visima vilivyochimbwa kwenye msongamano mkubwa wa makazi ya watu bila kuzingatia utaalam au kula chakula kilichochafuliwa kwa vinyesi.

Napenda kusisitiza kwamba maji safi na salama ya kunywa ni lazima yachemshwe, yachujwe na kuhifadhiwa katika vyombo safi.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam sasa hivi kumekuwa na adha kubwa ya wafanya biashara ya maji ya matenki. Wafanya biashara hawa hukata mabomba ambayo yanaelekea kwa wananchi ili wapate adha, wakanunue maji katika sehemu zao. Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti hali hii ili kuwaondolea kero wananchi wa jiji la Dar es Salaam? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna watu ambao wanauza maji kwa kutumia matoroli au kwa kutumia mikokoteni lakini pia wenyewe kwa kukata mabomba ili wapate maji hayo ni kosa. Na ni kosa ambalo pia mtu akiweza kupatikana anahitaji kupewa adhabu na tuna adhabu mbalimbali ambazo katika sheria zetu za maji zinaelekezwa kwamba kwa mtu atakayekata mabomba makusudi au kwa nia ya kuleta athari mbalimbali kuna adhabu ambazo atapewa. Napenda kutoa wito kwamba kwa wale wote wenye tabia ya kukata mabomba waache kwani sasa hivi tutaweza kuanza kuchukua hatua za nidhamu kuhakikisha kwamba hakuna kitendo kama hicho kinaweza kikatokea.

Na. 368

**Malipo ya malimbikizo ya madai ya polisi**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi katika bajeti yake ya mwaka 2006/2007 kupitia Wizara ya Usalama wa Raia kwamba, italipa mapema malimbikizo ya madeni mbalimbali ya askari polisi:-

(a) Je, hadi kufikia mwisho wa mwezi Mei, 2007, ni kiasi gani cha fedha kimetumika kulipa madeni ya askari hao?

(b) Je, ni madeni ya askari wangapi waliofariki duni ambapo warithi wao wamelipwa kwa askari wa Tanzania Zanzibar?

(c) Je, ni askari wangapi (kwa majina) wa mkoa wa Kaskazini Pemba wamelipwa madai ya malimbikizo yao hadi kufikia mwezi Mei, 2007?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali iliahidi kulipa malimbikizo ya madai ya Askari polisi katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2006/2007. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Mei, 2007 jumla ya shilingi bilioni 5.4 zilikuwa zimetumika kulipa madeni ya askari polisi nchini, wakiwemo wa Zanzibar, ambapo wamelipwa jumla ya Shs. 595,497,064/=.

(b) Madeni ya askari watano waliofariki dunia warithi wao wamelipwa jumla ya shilingi 5,054,450/= kama ifuatavyo:-

*(i)Assistant Inspector* Salehe H. Mwariko Sh.2,150,000/=;

.*(ii)Assistant Inspector* Ahmed Burhani Sh. 780,000/=;

(iii) Askari Na. E.3500 PC Haider Sh. 1,155,000/=;

(iv)Askari Na. D. 9497 CPL Hamadi Abeid Sh. 889,450/=; na

(v) Askari Na. D. 5083 CPL Mohamed Khamis Sh. 80,000/=.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya askari polisi 447 wa mkoa wa Kaskazini Pemba wamelipwa madai ya malimbikizo yao hadi kufikia mwezi Mei, 2007. Kwa kuwa majina ni mengi naomba nimkabidhi Mheshimiwa Mbunge, orodha yao kwa maandishi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya askari hawa wengine wanaondoka duniani katika mazingira ya kutisha kwa sababu wengine wanauwawa wakiwa kazini. Na mafao yao yanapochelewa kutolewa wale warithi wao huwa wanapata adhabu mbili ya kukosa mtu wao na kukosa kile kidogo cha kuwasaidia kimaisha.

Je, Wizara inaonaje kuharakisha malipo haya kwa mfano askari D. 2339, Juma Fadhili, ambaye aliuwawa katika shughuli za kazi na wengine?

Ni muda gani hasa inachukua kwa mujibu wa mipango yao katika Wizara mtu anafariki mpaka anapopewa mafao yao. Inachukua muda gani hasa jambo hilo kutendeka?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni usumbufu mkubwa kwa wale ambao wanafariki dunia na baadaye warithi wao wanachelewa kupata malipo yao. Lakini si nia ya Serikali kufanya usumbufu huu lakini hutokea wa ufuatiliaji wa taarifa mbalimbali zinahitajika kwa nia ya kufanyiwa malipo. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya kila jitihada sasa kubadili tatizo hilo na tuweze kulipa kwa kutumia muda mfupi kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muda gani tungependa isichukue zaidi ya miezi mitatu lakini tutajitahidi ifike chini ya hapo.

Na. 369

**Ajira katika Jeshi la Polisi**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa wako Watanzania warefu na wengine wafupi na kwa kuwa sifa mojawapo ya kuwa askari ni kuwa mrefu:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa iko haja ya kubadilisha sheria zake ili iwatendee haki Watanzania wote katika kuajiri, hasa katika jeshi la Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za jeshi la Polisi yaani *Police General Orders,* kifungu Namba 54 kimeainisha utaratibu na sifa zinazotakiwa ili kijana aweze kujiunga na jeshi la polisi. Pamoja na sifa ya urefu, sifa nyingine ni kiwango cha uadifu, uaminifu, elimu, ujuzi na umri wa mwombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hakuna nia ya kubadili kanuni ya sifa ya urefu, kwani wakati wa zoezi la ajira Wilaya zote hapa nchini zimekuwa zikipata nafasi kwa uwiano na kulifanya jeshi la polisi kuwa na sura ya kitaifa.

Aidha, inapotokea vijana kukosa sifa ya urefu unaotakiwa katika Wilaya au Mkoa wowote, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya eneo husika inaweza kutuma maombi kwa inspekta jenerali wa polisi ili waweze kuchukua vijana wasiofikia urefu huo lakini wana sifa nyingine, na jambo hili limekuwa likifanyika mara nyingi bila matatizo.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu nzuri la Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nashangazwa kwa sababu ingekuwa tuko Phillipino, sheria kama hii ingewataka wangesema kwamba watu warefu wasipate kazi ya polisi Phillipino basi ingelikuwa ni sahihi kabisa, kwa sababu wote ni wafupi.

Lakini Tanzania kuna wafupi na warefu kwanini utaratibu wa kubadilisha sheria hii hauji mara ikabadilishwa ili watu wote wakapata haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Phillipino kwa sababu wote nao ni wafupi kwa hiyo kuna askari wafupi si tatizo, lakini hapa kwetu kuna watu wafupi na warefu na tunavyoamini watu warefu wanaweza kupambana zaidi na uharifu na ndiyo maana hasa tunatumia kigezo hicho lakini hata hivyo yako majukumu mengine ambayo yanafanywa na askari wafupi kwa hivyo huwaajiri mfano ni kamishina wetu wa polisi Mheshimiwa Mtweve ni mfupi lakini yupo katika jeshi la polisi.

**MHE. JOB YUSTINO NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri

wakati akijibu amesema kwamba kwa Wilaya ambazo wanavijana wafupi wapeleke maombi yao rasmi kwa mkuu wa polisi sasa swali.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali kuchukua ombi la wananchi wa Kongwa kupitia Mbunge wao ambaye anaonekana kwa urefu wake. Kwa hiyo, wananchi wangu wanafananaje, anaweza akachukua ombi la Kongwa kwamba Kongwa iwe *specially* ikubalike kwamba wawe inhold kwenye jeshi la polisi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze mfupi kama yeye mwenye nguvu, kwa kule Kongwa kwa sababu tunajua anauwezo mkubwa kwa hivyo kwao wao tutaweka kipaumbele kwa watu wa Kongwa tutakuwa tuweke *special priority* kwa sehemu hiyo. *(Makofi)*

Na. 370

**Gharama za Kusambaza Umeme Mbinga**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ipo kwenye mchakato wa kununua na kufunga Genereta zenye uwezo mkubwa wa *2 MVA* kwa ajili ya Mbinga:-

Je, Serikali, itatenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kusambaza mtandao wa umeme wilayani hapo ili umeme huo utumike vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 150,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa laini na shilingi 450,000,000/= kwa ujenzi wa njia mpya za umeme katika Mji wa Mbinga. Kazi ambazo zimeshafanyika ni pamoja na ukarabati wa njia ya *Kv33* na ya *Kv 0.4* yenye urefu wa kilometa 10, ukarabati wa transfoma 6 na ununuzi wa transfoma moja.

Kazi hizi zilifanyika ili kuuweka mtandao wa umeme kuwa tayari kupokea umeme unaozalishwa kwa kutumia jenereta ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga yenye uwezo wa *Kva320* wakati utaratibu wa kununuliwa jenereta mbili kubwa zenye uwezo wa *kVA1,250* kila moja ukifanyika. Jenereta hizo zinatarajiwa kuanza kazi katika robo ya nne ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa umeme uliokamilika katika mji wa Mbinga ni zaidi ya asilimia hamsini (50%), Serikali itaendelea kutenga fedha awanu kwa awamu katika Bajeti yake ili kuendelea kusambaza mtandao wa umeme katika mji huo.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo sana la nyongeza. Ni lini hasa umeme utawashwa Mbinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tulizokuwa nazo kutoka shirika letu la *TANESCO,* matarajio ya kuwasha umeme katika mji wa Mbinga ilikuwa yafanyike mwishoni mwa mwezi huu ama mwanzoni mwa mwezi ujao wa mwezi wa tisa.

Na. 371

**Hitaji la Umeme Kipumbwi – Pangani**

**MHE. RIZIKI O. JUM**A aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa umeme unawalenga Watanzania wote waishio Mijini na Vijijini, kwa nia ya kuwasaidia kimaendeleo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia huduma hiyo muhimu Watanzania wa kijiji cha Kipumbwi wilayani Pangani?

(b) Kwa kuwa, wananchi nao wamefanya juhudi kubwa ya kuwasiliana na *TANESCO* kupitia Serikali ya Kijiji, na kilichoshindikana hadi sasa ni *TRANSFORMA.* Je, Serikali itawasaidiaje Watanzania hao ili nao wafaidike na huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi, wa kupeleka na kusambaza umeme katika Kijiji cha Kipumbwi utajumuisha ujenzi wa *Sub Station* yenye uwezo wa *Kva 50, 33/0.4kV* pamoja na kujenga laini ndogo ya *volt* 400 yenye urefu wa kilometa 1.2.

Tathimini ya kusambaza uememe katika Kijiji cha Kipumbwi imeshafanyika na gharama zinakadiriwa kufikia shilingi 7,839,975/=. Kukamilika kwa mradi huu kutawapatia umeme wateja wapatao 32 katika awamu ya kwanza na baada ya miaka mitano ijayo wateja wataongezeka kufikia 50.

Mheshimwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali iliyopangwa kwa ajili ya umeme vijijini, mradi huu haujaweza kutekelezwa. Kwa mwaka 2007/2008, Serikali inaanzisha wakala wa Nishati Vijijini ambaye atatekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema ni kwamba kuhusu mradi huu *TANESCO* wametuthibitishia kwamba utekelezaji wa mradi huu utaanza wakati wo wote kuanzia sasa. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kipumbwi waendelee kuwa wavumilivu wakati Serikali tunaendelea kutekeleza mradi huu.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, Mheshimiwa Waziri naye nimshukuru kwa majibu yake mazuri ambayo yamenipa matumaini na mwanga kuelekea kule kijiji cha Kipumbwi.

Lakini suala hili lilikuwa ni la muda na kiwango hiki cha fedha kidogo sana kwa Serikali, shilingi milioni 7 kuwafikishia wananchi wa kijiji cha Kipumbwi umeme jambo ambalo ni maombi yao ya muda mrefu, lilikuwa ni suala la kuwanyima haki ya kimaendeleo na wao wananchi wake. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu mkubwa kulitilia maanani pamoja na taarifa aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwamba ahakikishe kwamba mwaka huu basi nao wanawekwa katika utaratibu huu wa kuwapatia umeme.

La pili wananchi hao wamehangaika muda mrefu sana, na pale kuna zahanati ambayo inawasaidia wananchi wa kijiji cha Kipumbwi. Je haoni Mheshimiwa Waziri kwamba muda wote huu ambao wameleta maombi yao ya muda mrefu ili kufikishiwa umeme kwamba kuna umuhimu wa kuwepo umeme kwa haraka pale ili kuwaondolea matatizo wakina mama wajawazito hasa pale wanapohitaji kujifungua na watoto wachanga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu letu la msingi ni kweli tunafahamu kwamba ni busara wananchi wa Kipumbwi wameweka maombi yao kwa muda na tunafahamu pia umuhimu wa kutoa huduma ya umeme kwa ajili ya kuwezesha kuboresha huduma za zahanati zilizopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tumedhamiria kikweli na naomba hili nisisitize kwamba na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ofisi yetu imekuwa ikiwasiliana na yeye tunamwarifu kwamba utekelezaji wa mradi huo utaanza hivi karibu na huenda ukaanza kabla ya mwisho wa mwezi huu. Kwa hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani na Serikali itaendelea kufanyia kazi jambo hili kwa dhati kabisa.

Na. 372

**Ujenzi wa Mitambo ya Mawasiliano ya Simu**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kujenga mtambo wa *Celtel* Nkungi na ikaahidi kukamilisha ujenzi wa mtambo wa *TTCL* kwenye eneo la Lambi kabla ya mwezi Oktoba, 2006 lakini mpaka sasa kampuni hizo hazikujenga mitambo hiyo na kusababisha

wananchi wengi wenye simu za mkononi kupanda kwenye mawe/miti ili kupata mawasiliano ya kibiashara na familia jambo ambalo ni hatari sana kwani mtu anaweza kuanguka na kuumia:-

Je, Serikali sasa inasema nini juu ya ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya simu Tanzania *TTCL* inatekeleza kwa awamu mradi wa kusambaza simu za mikononi kwa kutumia teknolojia ya *CDMA (Code Division Multiple Access)* katika maeneo mbalimbal kote nchini. Awamu ya kwanza ya mradi huu inaendelea kwa kasi. Maeneo ya Lambi na Nkungi ambayo yapo katika Jimbo la Iramba Mashariki, yako katika utekekelezaji wa awamu ya pili ambayo inategemewa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2008.

Hata hivyo, eneo la Lambi kwa sasa linapata huduma ya mawasiliano ya simu kutokea Ishuela. Eneo la Nkungi ambayo nalo utekelezaji wake uko katika awamu ya pili, tayari kwa sasa limeanza kupata mawasiliano ya huduma ya simu kutokea Dungunyi ambayo imo katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Celtel* katika kuhakikisha kwamba inadumisha shughuli zake katika maeneo mbalimbali nchini, ina mpango wa kupeleka huduma zake katika maeneo ya Nkungi ifikapo mwezi Septemba, 2008. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza napenda kukwanza naona pale kakosea kidogo hii ni tuna eneo la Iyami hiyo siyo Lambi. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kampuni hizi za simu za Mikononi zimeenea sana kwa Iramba hili tunasema kwa baadhi ya Kata ambazo zimefikiwa tunazifagilia sana kampuni hizi kampuni. Kwa kuwa kampuni hizi zinajiendesha kwa njia ya biashara zinapokuja kufunga minara tayari zinajiendesha kibiashara kwa sababu kila unaponunua ile kazi unanunua unalipia na ndipo upata huduma.

Lakini kwa kuwa wanapokuwepo pale wanafunga hiyo minara ni sehemu ambazo zina makazi ya watu. Serikali za Kijiji ambayo maeneo hayo yanamiliki na mikataba wamekubaliana kwamba wanapofunga pale huo mnara ili wanapofunga huo mnara wakati wanaendelea na miradi wailipe fedha kidogo kwa kijiji. Na kwa kuwa liko tatizo katika mnara wa Magira uliopo Ndago pale Kampuni ya *Vodacom* wamefunga mnara kwa kipindi kirefu na wakaahidiana kulipa 150,000 kila mwezi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swali bwana.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye swali.

(a) Naibu Waziri anasemaje kuhusiana na kampuni ya *Vodacom* kutokutimiza masharti ya kulipa kama walivyokubaliana na Serikali ya Kijiji cha Nguvumali makubaliano ya awali yalivyokuwa?

(b) Kwa kuwa sambamba na lile la msingi. Je, Wizara iko tayari kuhamasisha kupeleka minara katika Kata za Tulia ambazo lipo Ziwa Kitangiri kwa ajili ya wafanyabiashara huko waweze kufanya biashara ya samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa pongezi zake alizozitoa kwa kampuni hizi na mimi nitazifikisha lakini pili kuhusu Kijiji cha Ndago kutolipwa shilingi 150,000 kama ambavyo waliahidiana na *Vodacom* hilo alilete na sisi tutalifikisha kwa sababu kiutaratibu ni kwamba Makampuni haya yakikubaliana ama na mtu binafsi au na kijiji kutumia eneo lao kuweka mnara basi huwa kuna makubaliana ya kulipwa. Kama kuna tatizo lolote ambalo anadhani lipo basi tusaidiane naye tunaweza tukalitatua.

Suala la kupeleka mnara kwenye eneo hilo alilolitaja ni kwamba kampuni zetu kwa kweli linafanyakazi hizi zimedhamiria kwa kweli kuhakikisha kwamba zinasambaza hudumu ya simu nchini kote na ndiyo maana sasa hivi utakuta kila eneo la nchi kampuni hizi zinafika. Lakini hufanya hivyo mara baada ya kufanya tathimini ya kibiashara na nina hakika kwamba baada ya kufanya tathimini hiyo na vile vile kuangalia hali halisi basi maeneo hayo ya Sekenke yataweza kufikiwa. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo haya yaliyosemwa na Mheshimiwa Msindai yanafanana sana na baadhi ya maeneo katika Jimbo lako Mheshimiwa Naibu Spika, la Njombe, ambalo linapakana na Jimbo langu katika maeneo yangu ya mpakani mwa Tanzania na Msumbiji Kijiji cha Mhukulu halafu kijiji cha Kilagano na Kata ya Ifinga.

Tayari maombi yetu yalishapelekwa rasmi kwenye Wizara ya Miundombinu kupitia Mbunge, mimi na Naibu Spika na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu anayehusika na masuala hayo Mheshimiwa Dr. Maua Daftari alishayapokea. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atatuhakikishia lini maeneo hayo niliyoyataja yatapatiwa mawasiliano hayo ya simu kama ilivyoanza kupelekewa maeneo mengine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, usibadilishe ahadi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwa kweli kampuni hizi zina nia ya kupeleka mawasiliano katika nchi nzima. Maombi hayo ambayo Mheshimiwa

aliyoleta yalishapelekwa kwenye kampuni husika na tutafuatilia kuona kwamba sasa wameweka mikakati gani ya kufika maeneo yote katika Jimbo la Peramiho, Jimbo la Njombe na maeneo yote ya Nchi nzima. Lakini kuhusu suala hilo tutalifuatilia na tuweze kuona lini ahadi hiyo itatimizwa. *(Makofi)*

Na. 373

**Ujenzi wa Barabara toka Mtwara – *Mbamba Bay***

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali ya Japan imekubali kufadhili sehemu kubwa ya ujenzi wa brabara toka Mtwara – *Mbamba Bay* ya eneo la Ukanda wa Maendeleo ya Kusini *Mtwara Development Corridor*, hivyo kuibua na kutumia raslimali zilizopo kwa Maendeleo ya Mikoa husika na nchi kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali imefanya maandalizi gani ili kuhakikisha kwamba ujenzi wa Barabara hiyo hautagubikwa na matatizo kama yaliyojitokeza katika ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Lindi?

(b) Kwa kuwa, lami kati ya Mtwara na Masasi imechakaa kabisa. Je, kuna mpango wowote wa kuiondoa na kuweka nyingine mpya badala ya kuweka viraka viraka?

(c) Je, yale madaraja yaliyong'olewa na mafuriko makubwa ya mwaka 1990 kama vile Chipite, Nangao,Chikukwe, Namakongwa na kadhalika Sasa yatajengwa upya ili kufanya ufumbuzi wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kwamba miradi yote ya ujenzi wa Barabara inatekelezwa vizuri na kwa ubora unaotakiwa. Serikali itahakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa kwa umakini wa hali ya juu ili uweze kukamilika kama ilivyopangwa. Aidha, tutatumia uzoefu wa matatizo yaliyojionyesha kwenye ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Lindi kuhakikisha kwamba matatizo hayo hayajirudii katika miradi inayofuata ikiwemo hii ya Masasi – Tunduru – Songea – *Mbamba Bay*.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Mtwara – Mongoyo – Masasi yenye urefu wa kilomita 205 iliyojengwa miaka ya 1970 uhai wake (*design life*) umeisha na inahitaji ukarabati kwa kuwekewa tabaka jingine la lami au baadhi ya maeneo kujengwa upya.

Kwa sasa, Serikali inaendelea kuitengea fedha za matengenezo ili iendelee kupitika wakati inatafutiwa fedha za kuikarabati kwa kiwango kinachotakiwa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Barabara hii ilitengewa shilingi 422.638 milioni kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*). Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, Barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 2,570.66 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya kawaida na matengenezo ya sehemu korofi.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu madaraja yaliyozolewa na mvua za mwaka 1990 katika Barabara ya Mingoyo – Masasi Serikali inaendelea na mikakati ya kutafuta fedha za ndani na kutoka kwa wafadhili mbalimbali ili kuyajenga upya na kupata ufumbuzi wa kudumu.

Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali ilitenga fedha za ndani shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Chikukwe. Katika mwaka huu wa fedha, jumla ya shilingi milioni 760.45 zimetengwa kwa ajili ya madaraja ya Namakongwa, Loloya na Mandiwa.

**MHE. RAYNALD ALFONS MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri yanayoridhisha na kuishukuru pia Wizara yake kwa juhudi inazozifanya katika kujenga barabara kati ya Dar es Salaam na Lindi. Baada ya kusema hayo naomba kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika eneo la Chipite ni eneo gumu sana Kijiolojia. Je, Serikali ina mpango gani wa kulidhibiti eneo hili hasa kwa kuinua tuta au kujenga bwawa juu yake ili kwamba maji yasije yakawa na nguvu na kuharibu hiyo barabara?

(b) Kwa kuwa madaraja mawili ya Nanganga na Daraja la Nangoo hivi sasa yamezidi kudidimia na yanagusa maji. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha madaraja haya mawili hayawezi kuchukuliwa wakati wa mvua za masika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la Chipite ni korofi na lina hali mbaya ya Kijiolojia. Lakini kama ambavyo nimeshamweleza tumeamua kutumia kidogo utalaam wa hali ya juu tuweze kuona ni namna gani tukaweza tukarekesha eneo lile. Watalaam tayari wamefanyakazi hiyo, ripoti imefika Wizarani na tutajaribu kuangalia najua itakuwa ni gharama kidogo kulingana na hali halisi ya eneo lile. Lakini Serikali itahakikisha kwamba inapaboresha eneo hilo ili pasiendelee kuwa ni kero ya kila wakati.

Kuhusu swali la pili, la Daraja la Nangoo pamoja na lile la Nanganga niseme tu kwamba kwa upande wa daraja la Nanganga kwa mwaka huu wa fedha tumetenga milioni 400 kwa ajili ya kurekebisha daraja lile. Lakini kwa bahati mbaya kwa mwaka huu Daraja la Nangoo halikuweza kupata fedha yoyote. Kama nilivyosema madaraja ni mengi na yale ambayo nimeyataja pamoja na hili la Nanganga tutayashughulikia mwaka

huu. Isipokuwa hili la Nangoo tutajaribu kuangalia kuweka fedha kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Na. 374

**Vyuo vya Walimu wa Shule za Awali Vilivyoko Mitaani**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y.MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa kuna vyuo vya kufundisha walimu wa shule za awali mitaani; na kwa kuwa sifa za walimu wa shule hizo zinahusisha mambo mengi kuliko yale ya walimu wa shule za msingi au sekondari:-

Je, Serikali inavijua vyuo hivyo na inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba vinafanya kazi kulingana na matakwa ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, naomba kutoa maelezo ya utangulizi. Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Elimu ya Awali ni kwa ajili ya watoto wa miaka 5 na 6 ambayo hupaswa kuwa sehemu ya shule za msingi. Madarasa ya shule za awali hufundishwa na walimu waliopita Vyuo vya Ualimu vya Daraja A ambavyo ufundishaji wa Elimu ya Awali ni sehemu ya mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Vipo vyuo 41 vya Ualimu vya daraja A vinavyojulikana na Serikali. Kati ya hivyo 18 ni vya Serikali 23, si vya Serikali ila ni vya watu binafsi. Ili kuhakikisha kuwa vyuo vinafanya kazi kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Serikali, Wizara hufanya ukaguzi wa Miundombinu, Vifaa vya Kufundisha na Kujifunzia na kuhakikisha kuwa Chuo kina wakufunzi wenye sifa. Aidha vyuo vinatakiwa kufundisha kwa kutumia mitaala iliyoidhinishwa na Wizara. Kuanzisha na kuendesha Chuo cha Ualimu wa Shule za Awali mitaani bila usajili ni kinyume cha utaratibu. Mtazamo wa Wizara, ni kuona namna ya kushirikiana na Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto katika kuangalia suala la utoaji wa elimu ya watoto ambao hawajafikia umri wa kuanza daraja la kwanza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize kama ifuatavyo. Kwa kuwa baadhi ya vyuo sasa ambavyo amevitaja vya watu binafsi 23 wamekuwa na tabia ya kuweka mabango ya kusema kwamba wanafundisha watoto wa shule za awali pamoja na walimu je, Serikali inalitambua hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, na kama inaitambua ni hatua gani Serikali itachukua ili kuhakikisha kwamba elimu izingatiwe kwa kadri ya uwezo wake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nyawazwa kama ifuatavyo. Kama anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna udanganyifu unaofanyika katika ufundishaji wa walimu wa shule za awali, hili suala tulitambua na ndio maana tunasisitiza kwamba ni lazima yeyote anayeanzisha chuo kinachofundisha walimu wa elimu ya awali au anayeanzisha kituo cha kufundisha watoto wa elimu ya awali, vyote ni lazima viandikishwe na Wizara ya Elimu. Hapa tunayo idadi ya vyuo 23 ambavyo shule au vyuo hivi ndio vilivyoandikishwa kama kuna mtu ambaye anaendesha nje ya utaratibu huu, basi huyo anavunja sheria na tunaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, wale ambao wanaendesha shule hizi za awali wanaendesha vyuo kwa ajili ya walimu wa shule za awali bila vibari maalum tupewe taarifa ili tuweze kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Kuhusu swali la pili la kuhakikisha elimu inayotolewa ibaki kuwa bora Wizara yangu inapeleka ukaguzi wa mara kwa mara katika vyuo hivi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi waliopo ni wale wenye sifa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vipo vya kutosha ili elimu inayotolewa pale iwe ni elimu bora na inayokubalika na Wizara yetu ya elimu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umeisha, sasa nina matangazo. Kwanza nina matangazo ya wageni nianze na wageni wa Waziri anayesoma hotuba yake leo, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu, Waziri wa Michezo anao wageni wake wafuatao katika *Speaker's Gallery* yupo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bibi Kijazi Mtengwa, huyu ni mama, ninataja hivyo kwa sababu wako wachache na ndio maana ninamtaja kama ni mama, tunaye Mkurugenzi wa Michezo Bwana Henry Ramadhani, tunaye Mkurugenzi wa Utamaduni Prof. Mwasoka, tunaye Bibi Rose Shellukindo, tunaye *DPP* Bwana Makundi, tunaye Mkurugenzi wa *TUT* Tido Mhando wanakufahamu toka *BBC* ndio maana unapigiwa makofi, tunaye Naibu Mhariri wa Habari Bwana Nyundo, hawa ni wageni mahususi wa Waziri. Mheshimiwa unaulizwa mke wako hawajamwona pamoja na familia yako. (*Makofi*)

Pia tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana wapo katika makundi matatu, wapo wageni wanaotoka *High Law* kuna Ndugu Ansiga Mushi, kuna George Langisi, kuna Louis Flota, kuna Steven Shekiondo, Bwana Langisi anatoka Canada na Bwana Louis Flota anatoka Geneva na wale wengine wanatoka Dar es Salaam. (*Makofi*)

Pia tuna Wakuu wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wengine tuliwataja juzi lakini si vibaya kuwarudia kuna Doker Ramadhani Dau *NSSF* tunashukuru naona siku hizi umeamua kujenga majumba yetu yote mpaka ya Ubalozi, tunashukuru sana, kuna Ndugu Willium Erio *PPF,* tuna Emanuel Pumba wa *NHIF*, kuna bwana Kida wa *LAPF* yeye hayupo, kuna Bi. Hawa Manga wa *PSPF*, kuna bwana Msangi wa *GEPF*, ahsanteni sana.

Ilani ya Uchaguzi imetambua sana mifuko ya hifadhi ya jamii na tunakumbuka wakati tunatengeneza Ilani hii mlikuwa mmesema kwamba tunaweza pia tukatafuta hifadhi ya jamii hata wakulima mmoja mmoja na mlikuwa tayari kufanya hiyo kazi nadhani mnaendelea kufanya brain storming, mimi nilikuwa mmojawapo nilishiriki kuandaa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa hiyo ninajua jua. (*Makofi*)

Wageni wengine ni Bwana John Mchenya Mwakilishi wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi *TUCTA*, tunaye Bwana James Mashinga Mwakilishi wa Chama cha Waajiri *ATE* karibu sana, tunaye Bwana Alhaj Elsi mweka hazina wa CCM, tunaye Prof. Joseph Kanywani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Felisiani Tungaraza Chuo Kikuu cha Mkwawa nadhani mna mkutano. Pia tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe wananchi nane kutoka Kyera wakiongozwa na Ndugu Lameck Mbembera wa Kyera naomba msimame mliko, karibuni.

Pia tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka ni msaidizi wake Bwana Mahiku Malagande na wengine waliofuatana nao Bwana Mengi Jafam na Bwana Katambo hawa ni wajumbe wawili wa Majimaji *Salaam Club* ya Morogoro Mjini, karibuni sana. Pia tuna wataalam wa Benki ya Dunia tunaye Pamenda Blaa, tuna Bwana Messy Sabai na tuna bwana Hurbert Mengi hawa wanakuja kuonana na Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC* ili kuweza kuona jinsi wanavyoweza kushirikiana na kulifanya Bunge liweze kufanya kazi yake *effectively* ile kazi ya *oversight* ya Bunge, kwa hiyo watakuwa na mkutano nao baadaye.

Halafu kumtangaza bwana Ludovick Utto Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kwa taarifa yake mimi na yeye tumesoma pamoja mambo haya ya hesabu ni *class mate* wangu, wageni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya Bwana Kasma Haruna Mwenyekiti wa Chama cha Wilaya ya Urambo, Bwana Soud Nassor Mkurugenzi wa Haki za Binadamu Wilayani Urambo Chama cha *CHADEMA* siyo Chama cha CCM, tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi Bwana Deo Mloli kutoka Rukwa Manispaa Sumbawanga ni Mwenyekiti wa *PROTESO NGO* wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, yuko wapi karibu sana, tunao wageni wengine kuna Ndugu Matilda Switi kutoka Manispaa ya Mbeya nadhani ni Ndugu yake na Switi mwenyewe, halafu kuna Grace Charles Mwamlima kutoka Dodoma mjasiriamaali, halafu tuna wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma wako 40 simameni na walimu wenu, karibuni sana. Pia tunao wanafunzi 24 kutoka Shule ya Sekondari Dodoma nadhani wamekosa nafasi, pia tunao wanafunzi 23 kutoka Shule ya Msingi Msalato Dodoma, tuna wageni wa Mheshimiwa Sevelina Mwijage kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri ndiyo hao hao na wageni wengine wote mnakaribishwa na ninaomba niendelee na shughuli za kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa anaomba kuwatangazia Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwamba kutakuwa na kikao leo saa saba mchana mara baada ya kuahirisha Bunge katika ukumbi wa Kasusura Namba 219. Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Bwana Cheyo na Mwenyekiti wa Kamati ya Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mgana Msindai anaomba wajumbe wote wa Kamati hizi mbili leo saa saba

wakutane katika ukumbi namba 428 jengo la utawala saa tano, nadhani wakutane na wale wageni niliowatangaza wale wa Benki ya Dunia kutakuwa na kikao, wajumbe wa Kamati hiyo msikose kwa sababu ni vizuri mkawasiliana wageni. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawatangazia wajumbe wake kwamba saa saba mchana katika ukumbi 219 mtakuwa na mkutano wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anawatangazia wajumbe wake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika chumba 231 ghorofa ya pili, Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anapenda kuwatangazia wajumbe wake kuwa saa saba leo mchana katika ukumbi wa *Dodoma Hotel* kutakuwa na kikao, kwa hiyo wajumbe wote mkumbuke *Dodoma Hotel*, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa Shellukindo anawatangazia wajumbe wake kuwa leo tarehe saba saa tano asubuhi kutakuwa na mkutano chumba namba 133.

Tangazo lingine ni kwamba Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo ambaye pia ni Meneja wetu wa Michezo Mheshimiwa John Bendera anawatangazia Wabunge wote kwamba ziko zile fulana za *Taifa Star* wote mnakaribishwa ziko pale kwenye *lob* inafaa mkazichukue ili tarehe 8 Septemba, 2007 wakati timu yetu inapambana na timu ya Taifa ya Msumbiji basi na nyie huko mtakapokuwa mvae maana wananchi watakuwa wamevaa na nyie mvae.

Tangazo lingine ni kwamba jana wakati tulipokuwa tunaahirisha kikao nilieleza kwamba Mheshimiwa Spika hamtamwona leo na kesho kwa sababu amefiwa na mjomba wake Chief Abdallah Fundikira, ni mjomba wake kwa maana ya kwamba mama yake na Spika ni dada yake na marehemu Chief Abdallah Fundikira, wanaondoka leo mchana kwenda kuzika Tabora na bahati nzuri Mheshimiwa Rais naye ataenda leo atashiriki katika mazishi hayo na kuna Wabunge watakaoenda lakini Wabunge tuliowachagua rasmi kwenda *officially* atakuwa Mheshimiwa kiongozi wa Upinzani Mheshimiwa Rashid Mohamed Rashid ndiye atakayeongoza ujumbe huo.

Aidha ataenda na Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw' kwa niaba ya *Steering Committee*, ataenda na Estherina Kilasi kwa niaba ya Tume na Mheshimiwa Mohamed Rashid ataenda kwa niaba ya Wapinzania pia kwa niaba Zanzibar na Wabunge wengine wataenda. Kuna Waziri wa zamani pia ambaye alifanya kazi na Marehemu Abdallah Fundikira, Mzee George Kahama, pia atashiriki katika mazishi hayo na Mheshimiwa John Malecela pia ataenda na wengine.

Pia Mheshimiwa Shoka ataenda, Mheshimiwa Shoka ataenda kwa sababu Marehemu yeye alikuwa Mbunge kati ya 2000 na 2005 kwa kuteuliwa na Rais, Ukumbi ule wa Msekwa upande wa kushoto wa Spika wanakaa wapinzani na upande wa kulia wanakaa Chama Tawala sasa mzee kwa sababu alikuwa hawezi kupanda ngazi alikuwa anakaa upande wa Upinzani ingawa alikuwa wa CCM.

Sasa huyu Bwana Shoka yeye ndiye alikuwa anabeba vifurushi vya mzee akitaka posho ataenda, waswahili wanaita swahiba wake. Kwa hiyo, kwa heshima hiyo na

kwamba walikuwa karibu sana na Marehemu wakati akiwa Mbunge pia ataenda. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Spika, hamtamwona ataenda leo mchana, ujumbe mwingine unatoka Dar es Salaam wataungana na wengine hapa ili waende kumzika. Mzee yule. Ni mzee mashuhuri kama nilivyosema alikuwa *Chief* lakini ndio Waziri wa kwanza kabisa wa Sheria katika nchi na tunataka azikwe kwa enzi ya Chama chetu cha Mapinduzi (CCM), ahsanteni sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008
### Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na asasi zake kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii, kwa niaba yangu na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kuwapongeza wenzetu waliojiunga nasi hapa Bungeni, Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalumu. Vile vile ningependa kuwapongeza waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba, Mheshimiwa Septuu Nasoro, Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janet Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Lwanyatika Masha. Tunawatakia mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa akinamama Watanzania waliopewa nyadhifa kubwa katika asasi za Kimataifa, kama vile Mhe. Dr. Asha Rose Migiro, ambaye hivi sasa ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Getrude Mongela, Mbunge wa Ukerewe, ambaye hivi sasa ni Rais wa Bunge la Muungano wa Afrika, Mheshimiwa Amina Salum Ali, ambaye hivi sasa ni Balozi wa Umoja wa Afrika nchini Marekani na Mheshimiwa Balozi Liberatta Mulamula, ambaye sasa ni Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Ukanda wa Maziwa Makuu. Ninawatakia mafanikio katika kutekeleza majukumu yao mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilifikwa na msiba mkubwa kwa kumpoteza aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, aliyefariki kutokana na ajali ya ndege iliyotokea huko Mbeya. Ajali hiyo pia ilisababisha vifo vya wafanyakazi wa Serikali marehemu John Bendera, Nathanieli Katinila na Theresia Nyantori.

Napenda pia kutumia fursa hii kuelezea huzuni na masikitiko makubwa yaliyotufika kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu wa Viti Maalumu kupitia

Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Marehemu alikuwa kijana shupavu na jasiri aliyeipenda nchi yake na watu wake hususani vijana ambao alikuwa mtetezi wao mkubwa. Mungu azilaze pema peponi roho za marehemu hao, Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, inayoongozwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, iliyojadili na kutoa ushauri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 07 Juni, 2007 na tarehe 19 Julai, 2007. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hii tumeyaingiza kadri ilivyowezekana katika bajeti hii na tutaendelea kuyafanyia kazi maelekezo ya Kamati yaliyobakia na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu leo wakati wa kujadili bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia inapenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Dkt. Emannuel Nchimbi, kwa ushirikiano na ushauri mzuri aliotoa wakati akiwa Naibu Waziri katika Wizara yangu. Nafasi yake, kama tunavyofahamu, ilichukuliwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, aliyekuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majukumu ya Wizara, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ina majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa Sera za Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera za Habari, Utamaduni na Michezo.
- Kuandaa Mipango ya ukuzaji wa sekta ya habari, utamaduni na michezo.
- Kuhamasisha uanzishaji wa vyombo vya habari katika maeneo ambayo hayavutii sekta binafsi.
- Kukuza na kuimarisha fani mbalimbali za sanaa nchini hususan sanaa za maonesho, ufundi na muziki kama kielelezo cha utaifa na chanzo cha ajira.
- Kuimarisha na kukuza Kiswahili ambacho ni lugha ya Taifa letu.

  Aidha, kuhimiza lugha za kiasili ambazo ni vijenzi vya lugha ya Taifa na kuhimiza mafunzo ya lugha za kigeni kwa ajili ya mawasiliano ya kimataifa.
- Kuimarisha utawala bora katika michezo nchini.
- Kuimarisha mafunzo yanayohusu fani za Wizara kwa watumishi wa Wizara.

- Kuongeza na kuimarisha miundombinu inayotakiwa kwa Wizara.
- Kuratibu shughuli za asasi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

- Kuandaa na kusimamia Viwango vya Ubora wa kazi za Habari, Utamaduni na Michezo.

- Kukuza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika fani za habari, utamaduni na michezo.

- Kusimamia Maendeleo ya Watumishi katika sekta za Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2006/2007, mwaka wa 2006/2007 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Tsh.98,403,000/= kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi 2007, jumla ya Tsh.147,661,418 zilikuwa zimekusanywa ambazo ni asilimia 150. Mchanganuo wa Makusanyo hayo upo kwenye Kiambatisho Na.I.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa kwanza wa uhai wa Wizara yangu, tumeshuhudia maendeleo ya kuridhisha katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025, ambayo ni kuwa na Taifa lenye raia wenye ufahamu, linalothamini utamaduni wake na lenye wananchi mahiri na hodari katika michezo.

Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na Tanzania kuanza tena kusikika katika michezo ya kimataifa, hususani mpira wa miguu; Watanzania kuwa na utaratibu wa kufikisha maoni, maswali na kero zao moja kwa moja Serikalini kwa kupitia mtandao wa tovuti badala ya kutegemea vikao vya Bunge na mikutano ya hadhara pekee. Mafanikio mengine ni kuwa na uwanja wa michezo wenye hadhi ya viwango vya kimataifa; lugha ya Kiswahili kuendelea kushamiri duniani na Tanzania kuendelea kuwa na vyombo vingi na anuai vya habari katika sehemu nyingi za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2006/07 Wizara yangu ilitekeleza mikakati mbalimbali iliyowekwa kisekta ili kufanikisha ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005, na maelekezo yaliyo kwenye Sera za Habari na Utangazaji, Maendeleo ya Utamaduni na Maendeleo ya Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Habari, Sekta ya Habari imeendelea kuongozwa na Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003 na maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipotembelea Wizara, mwezi Machi, 2006. Sera inakusudia kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha kukua na kushamiri kwa vyombo vya habari vyenye kuzingatia maadili ya taaluma na wakati huo huo vikilinda na kudumisha maadili ya jamii. Aidha, tunakusudia kuondoa malalamiko mengi ya wananchi kuhusu uduni wa huduma zitolewazo na vyombo vya habari na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki yao ya kikatiba ya kupata na kutoa habari wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kutayarisha mswada wa sheria wenye malengo yafuatayo:

Kuwa na sheria mwafaka itakayosimamia na kuongoza Sekta ya Habari.

Kurekebisha au kufuta kabisa sheria za vyombo vya habari zilizopitwa na wakati zinazolalamikiwa na wadau, kwa mfano Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, Sheria ya Utangazaji ya mwaka 1993 na Sheria ya Filamu na Maigizo ya Jukwaani ya mwaka 1976.

Kuvipa vyombo vya habari uhuru mkubwa zaidi katika kutafuta na kutangaza habari kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 116 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, 2005.

- Kuweka utaratibu wa kuwezesha kila raia kuwa na haki ya kudai na kupata taarifa kutoka kwenye asasi za umma na za binafsi kwa mujibu wa Kifungu cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Kuweka utaratibu wa usajili na umilikaji wa vyombo vya habari.
- Kulinda vyanzo vya habari vya waandishi wa habari.

- Kuwalinda watoto dhidi ya taarifa au picha zisizofaa kwa malezi yao.

- Kuweka bodi huru ya kusimamia taaluma ya habari.

Masuala hayo yaliwasilishwa kwa wadau ili kupata mchango wao, na mashauriano bado yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tovuti ya wananchi, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ilikamilisha utekelezaji wa Agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alilotoa katika Semina Elekezi ya Viongozi Wakuu wa Serikali huko Hoteli ya Ngurdoto, Arusha, Machi 2006, la kuanzisha Tovuti ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitambo yote ya Tovuti, ambayo ni pamoja na kompyuta, mawasiliano ya satelaiti na redio, imefungwa katika makao makuu ya Tovuti yaliyoko Idara ya Habari (MAELEZO). Idara hii itafanya kazi kwa ushirikiano na Wizara zote pamoja na mikoa kujibu hoja mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mawasiliano yao na Serikali, wananchi watakuwa huru kuwasilisha maoni, mapendekezo, maswali na kero kupitia ujumbe wa simu zao za mkononi, barua pepe au barua za kawaida kupitia posta.

Kila mwananchi anayewasilisha maswali au kero Serikalini atapatiwa majibu kutoka Wizara inayohusika katika kipindi kifupi iwezekanavyo. Kama ilivyo, kwa njia

nyingine zote za mawasiliano, hasa vyombo vya habari, Tovuti ya Wananchi inakusudia kufanikisha utekelezaji wa Aya ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo, pamoja na mambo mengine, inampa kila raia haki na uhuru wa kutoa na kupata taarifa zenye manufaa katika maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tovuti hii itaimarisha dhana ya uwazi na uwajibikaji Serikalini, dhana ambayo ni nguzo muhimu ya Utawala Bora. Mfumo huu mpya wa mawasiliano utaiwezesha Serikali kupata maoni ya wananchi kuhusu huduma wanazopatiwa na watumishi wa umma na binafsi kwa lengo la kuziboresha huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, Tovuti hii inampa mwananchi uhuru wa kuchagua moja ya njia tatu zifuatazo katika kuwasiliana na Serikali:

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya kwanza ni kutuma taarifa kwa njia ya tovuti yenyewe kwa kujaza fomu inayohusika na kuituma. Tovuti inampa mhusika namba ambayo ataitumia kufuatilia jibu lake kutoka Serikalini kuhusiana na taarifa aliyoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tovuti ya Wananchi inaziwasilisha taarifa za wananchi kwa maofisa husika wa Serikali katika Wizara zinazohusika na suala lililoletwa na mwananchi. Mara baada ya kupatikana kwa jibu la Serikali, jibu hupelekwa moja kwa moja katika tovuti ambapo mwananchi aliyetoa taarifa anaweza kupata jibu kwa kutumia namba yake ya kumbukumbu aliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya pili ni kutuma taarifa kwa simu ya mkononi. Mwananchi anatakiwa kuandika ujumbe anaoutaka na kisha kuutuma katika namba maalum iliyopangwa, ambayo ni 15715. Huduma hii inapatikana kupitia makampuni manne makubwa ya simu nchini Tanzania ambayo ni *Celtel*, Tigo, Vodacom na Zantel. Baada ya kutuma ujumbe huo mwananchi anapata namba ya kufuatilia majibu ya Serikali kuhusu ujumbe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwananchi ambaye anatoa taarifa yake kupitia ujumbe wa simu, jibu litatumwa kupitia tovuti na simu yake. Jibu la ujumbe wa simu linaweza kuwa muhtasari wa jibu lote ambalo limetumwa kwenye tovuti au linaweza kuwa kidokezo cha kuwaarifu wahusika kwenda kupata jibu lao mahali ambapo wanaweza kupata huduma za intaneti.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya tatu ni kutuma barua kwa njia ya posta. Wananchi watatuma barua kupitia Sanduku la Posta 9142, Dar es Salaam, ambako, baada ya barua hizo kuingizwa katika Tovuti wanaarifiwa kwa njia ya posta namba ya kufuatilia majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi ambao wanatoa taarifa kwa barua kupitia posta, mbali na kupata jibu katika tovuti, wahusika watapata jibu kwa njia ya barua ambayo itatumwa kwao kwa posta. Aidha, wananchi wanaweza kusoma kwenye Tovuti

maelezo mbalimbali yaliyotolewa na Serikali katika kujibu maswali ya wananchi, kama suala linalohusika ni la jumla na lina manufaa kwa jamii yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtandao wa habari za Serikali, uanzishwaji wa Tovuti ya Wananchi utafanikisha mpango wa Wizara yangu wa kuanzisha mtandao wa mawasiliano imara kati ya Idara ya Habari (MAELEZO) na Vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano ambavyo vimeanzishwa na Wizara zote ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji Serikalini. Katika utekelezaji wa mpango huo, mkutano wa kwanza baina ya Maofisa habari na Maafisa wa Vitengo hivyo ulifanyika jijini Dar es Salaam Agosti 25, 2006, na kubainisha vipaumbele katika kuimarisha mawasiliano kati ya wananchi na Serikali. Mkutano wa pili ulifanyika Mbeya, Oktoba 30 hadi Novemba 2, 2006, na kuhusisha maofisa 70. Katika mkutano huo mkakati wa pamoja wa mawasiliano ya Serikali na wananchi uliandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ofisi za Habari Mikoani, kama sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Habari kwa Umma wa 2006/2007, Wizara yangu iliahidi kufungua ofisi tano za Idara ya Habari katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma, Mbeya, Rukwa na Mtwara. Sehemu hii ya Mradi sasa itatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Wizara yangu na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo yanafuatia uamuzi wa Serikali wa kuzifanya ofisi za habari mikoani kuwa sehemu za Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maktaba ya picha, Maktaba ya Picha iliyoko Idara ya Habari ni hazina kubwa ya Taifa, kwani ina picha za kumbukumbu muhimu za matukio ya taifa na Serikali tangu mwaka 1948. Kutokana na mabadiliko ya teknolojia na matumizi katika vyombo mbalimbali imebidi mfumo wa uhifadhi wake ubadilike na uwe wa kielektroniki. Ndiyo sababu Wizara yangu ilianzisha Mradi huo ambao utakapokamilika utakuwa umeweka picha zaidi ya milioni mbili katika mfumo wa elektroniki na hivyo kurahisisha matumizi yake. Utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka 2006/2007 na unaendelea mwaka huu wa fedha kutokana na ukubwa wa kazi yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi ya Utangazaji Tanzania, Taasisi ya Utangazaji Tanzania (*TUT*) ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 239 la tarehe 14 Juni, 2000 chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 2 ya mwaka 1992. Majukumu makuu ya *TUT* ni kutoa huduma za utangazaji wa redio na televisheni, kueneza upatikanaji wa redio na televisheni nchini na kumiliki na kuendeleza rasilimali za redio na televisheni ya Taifa. Taasisi ya Utangazaji Tanzania inamiliki Radio Tanzania Dar es Salaam (*RTD*) na Televisheni ya Taifa (*TVT*). Aidha, *TUT* inamiliki vituo vya redio za kanda Dodoma, Kigoma, Nachingwea na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, *TUT* ilitekeleza ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, 2005 Ibara ya 116 (b), inayosema, na ninanukuu: "Kueneza Redio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa (*TVT*) nchi nzima na kuwa hewani kwa saa 24 kila siku" kwa upande wa televisheni na pia kwa upande wa redio kwa kutumia masafa ya *FM* ya Idhaa ya *PRT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendelea kutangaza kwa kiasi kikubwa vipindi vingi vya elimu ya umma, *TUT* imeanza kwa ari mpya kutangaza vipindi vinavyopendwa na wengi, hususan matangazo ya moja kwa moja ya mpira wa miguu. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka jinsi Televisheni ya Taifa na Radio Tanzania zilivyomudu kutangaza hivi karibuni mechi za mpira kati ya Timu ya Taifa na timu za Senegal na Burkina Fasso ambapo *Taifa Stars* ilipata ushindi wa kusisimua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ndani ya mfumo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, *TCRA*, kuna kipengele ambacho kinahusu Wizara yangu, nacho ni masuala ya maudhui katika utangazaji. Kamati ya Maudhui iliyotajwa katika Sehemu ya *IV* ya Sheria ya *TCRA* Na. 12 ya mwaka 2003 inateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya utangazaji baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Mamlaka. Kamati hiyo, kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya sheria hiyo, inahusika na:-

(a) Kumshauri Waziri kuhusu Sera ya Utangazaji.

(b) Kufuatilia na kudhibiti maudhui potofu ya utangazaji.

(c) Kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya utangazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 Sekta ya Utangazaji imeendelea kukua kwa kasi na watu wengi wanazidi kuomba leseni za kuanzisha vituo vya utangazaji. Mpaka sasa kuna vituo 40 vya redio nchini, vituo 22 vya televisheni na vingine 18 vinavyounganisha na kurusha matangazo ya vituo vingine (*relay*). Baadhi ya vituo hivyo vinamilikiwa na Halmashauri za Miji na za Wilaya. Aidha, vipo vituo 42 vinavyoendesha shughuli za '*cable' TV*. Kiambatisho Na.V kinaonyesha mtawanyo wa huduma za redio na televisheni kimkoa. Idadi ya magazeti iliyoandikishwa mwaka huu ya kila siku ni matano na mengine 40 ya kila wiki na hivyo kufanya jumla ya magazeti kila siku yanayoandikishwa nchini kuwa 33 na 187 ya kila wiki. Kadhalika katika mwaka huu fedha gazeti la Kiswahili la Serikali Habari Leo lilianzishwa na alihudhuria Rais Jakaya Kikwete tarehe 21 Desemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sheria ya *TCRA* ambayo inaruhusu wawekezaji kutoka nje ya nchi kumiliki asilimia 40 ya hisa katika kituo cha utangazaji, wawekezaji na wadau walio wengi katika sekta hii ni wazalendo ambao, pamoja na kutaka faida katika biashara zao, pia wanajali maslahi ya nchi yetu. Kwa ajili hiyo, kumekuweko na vipindi vingi vinavyotangazwa vya elimu kwa jamii na vinavyohamasisha wananchi katika kujiletea maendeleo. Katika mwaka 2006/2007, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

Kufanya mikutano na wadau katika mchakato wa kuhama kutoka teknolojia ya '*analogue'* kwenda '*digital'*. Uhamaji kutoka teknolojia ya '*analogue'* kwenda '*digital'* unatakiwa uwe umekamilika ifikapo mwaka 2015, kwa mujibu wa Shirika la Mawasiliano Duniani (*ITU*).

Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa vituo vya utangazaji nchini vinazingatia sheria na kanuni za utangazaji na kwamba hakuna mwingiliano katika matumizi ya masafa. Vituo vilivyokaguliwa ni vya Halmashauri za Songea, Njombe, Mbeya, Mbozi, Kyela, Rungwe na Iringa. Vingine ni vya Halmashauri za Mtwara, Tandahimba, Newala, Masasi na Tunduru. Kamati ya Maudhui pia ilikagua *ITV*, *Radio One*, *TVT*, *Radio* Tanzania Dar es Salaam, *Praise Power FM*, *Mlimani FM* na *Agape TV*, zote za Dar es Salaam.

Kufanya ziara za mafunzo katika nchi za Mauritius na Singapore, ambako kuna vyombo vya udhibiti wa utangazaji vinavyofanana na hiki cha kwetu, kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyoko katika sekta ya utangazaji ni kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa sasa ambao ni wa '*analogue'* kwenda '*digital'*. Kama nilivyosema, ifikapo mwaka 2015 redio na televisheni tulizo nazo sasa zitakuwa hazifai kutumiwa kwani hazitafanya kazi kutokana na mfumo mpya utakaotumika wa '*digital'* vinginevyo itabidi ziwekewe ving'amuzi ili ziweze kuendelea kutumika katika mfumo huo wa '*digital'*. Kuna umuhimu mkubwa sasa hivi wa kuwa na mikutano mingi na wadau ili kuwaelewesha juu ya ulazima wa kubadilisha teknolojia na pia kuwashauri wajiandae kwa gharama zinazohusu uhamaji huo. Hali kadhalika wananchi inabidi wahamasishwe na waelimishwe juu ya umuhimu wa kuzingatia teknolojia hii mpya ya '*digital'* katika utangazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*), ilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni (*CAP* 212) ya Mwaka 1961. Wamiliki wa Kampuni hii ni Serikali ya Tanzania, asilimia 99% na Mhariri Mtendaji, asilimia 1%.Madhumuni ya kuwa na Kampuni hii ni kutoa fursa kwa Watanzania kupata habari sahihi zilizotafitiwa bila upotoshaji. Kampuni inatakiwa kujiendesha kwa faida kama yalivyo makampuni mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha wa Kampuni ni kutoka Januari hadi Desemba, na hivyo malengo yake yanapangwa kwa mwaka unaoanzia Januari mpaka Desemba.

Kwa mwaka ulioishia Desemba 2006, Kampuni ilikuwa na malengo yafuatayo:-

Kupata faida ya Tsh. 450 milioni.

Kununua mtambo wa kuchapia magazeti.

Kuanzisha gazeti la Kiswahili.

Kuanzisha maktaba ya elektroniki ya magazeti, picha na machapisho mbalimbali ya Kampuni tangu ilipoanzishwa mwaka 1961.

Kubadilisha sura ya magazeti ya Kiingereza ( *Daily News* na *Sunday News*) ili kuongeza mvuto kwa wasomaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikia malengo hayo Kampuni imefanya yafuatayo:-

Kampuni imepata faida ya Tsh. 699 milioni kabla ya makato ya kodi kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2006.

Mtambo wa kuchapa magazeti umefungwa ikiwa ni pamoja na mitambo tegemezi kwa jumla ya Tsh. 2.2 bilioni; kati ya hizo Serikali ilitoa Tsh. 580 milioni.

Gazeti la Kiswahili liitwalo HabariLeo lilianzishwa na kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 21 Desemba 2006, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, 2005 Ibara ya 116(c) inayosema, na ninanukuu: "Kuanzisha gazeti la Kiswahili la Serikali".

Maktaba ya magazeti, machapisho na picha kwa njia ya elektroniki imeanzishwa kwa kunakili magazeti, machapisho na picha zote tangu mwaka 1961, gazeti la kwanza la "Tanganyika *Standard*" lilipoanzishwa.

Kusanifu upya magazeti ya Kiingereza kuyafanya yavutie zaidi wasomaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya utamaduni, katika mwaka wa 2006/2007 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ilitekeleza malengo yafuatayo:-

Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa Nne wa mwaka wa Sekta ya Utamaduni tarehe 27/11–1/12/2006 hapa Dodoma ambapo ulihudhuriwa na wadau 300.

Kuadhimishwa kwa Siku ya Utamaduni Ulimwenguni yenye ujumbe: "Utamaduni ni Uhai", tarehe 21 Mei 2007 ambapo jumla ya vikundi 18 vya utamaduni vilishiriki.

Tathmini ya Mradi wa TUSEME ilifanyika mwezi Februari, 2007 katika shule za sekondari 8 zifuatazo: Arusha, Machame, Lindi, Msalato, Kilakala, Korogwe, Bagamoyo na Mwenge. Tathmini inaonyesha kwamba mradi huo umewasaidia wanafunzi, hasa watoto wa kike, kueleza waziwazi matatizo yanayowasibu katika shule hizo na kuyatafutia ufumbuzi wao wenyewe.

Mradi wa ujenzi wa Jumba la Utamaduni umeanza mchakato wake baada ya kupatikana kwa eneo la ekari 100 katika kijiji cha Kiromo Wilaya ya Bagamoyo Mkoani Pwani. Tayari mkutano wa wadau kuhusiana na dhana nzima ya Jumba la

Utamaduni katika muktadha wa Tanzania umefanyika. Aidha, mchakato wa kupata michoro ya jengo unaendelea.

Kufanya utafiti katika Mikoa ya Kigoma, Tabora na Singida ili kupata dhamira ya busara inayohitajika katika utungaji wa sheria zinazotumika katika mwenendo wa maisha ya kila siku. Aidha, utafiti ulifanyika katika Mikoa ya Mtwara, Rukwa na Ruvuma ili kubaini mila na desturi zinazochochea na kusaidia kudhibiti maambukizo ya Virusi vya UKIMWI.

Kuendesha warsha ya vyombo vya habari yenye lengo la kuelimisha waandishi, wahariri, na watangazaji kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu, mwezi Septemba, 2006, Mjini Morogoro. Warsha hii ilijumuisha washiriki 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashindano ya *Miss World Africa* yamemshirikisha mrembo Nancy Sumari kutoka *Miss* Tanzania ambaye alishinda na kuifanya Tanzania iwe nchi ya kwanza kuchukua taji hilo Tanzania, alifanya vizuri katika mashindao ya Afrika Mashariki na Kati tangu alipoingia katika mashindano haya ya 1994.

Aidha Tanzania ni nchi mojawapo katika Afrika kufanikiwa kuingia fainali za Dunia ikiwa pamoja na Afrika Kusini, Nigeria na Zimbabwe na Liberia wakati huo Tanzania imefanikiwa kuingia katika sita bora baada ya kushiriki kwa miaka 10 tu, tofauti na India ambao wamewahi kutoa taji la *Miss World* kwa mara ya kwanza waliochukua miaka 15 kupita. *Miss University* imefanyika kwa mara ya kwanza Tanzania tarehe 14 mwezi Aprili mwaka huu ambapo *Miss* Flavian Mataka mwenye umri wa miaka 20 alipeperusha Bendera ya Taifa huko Mexico na kufanya vizuri kwa kuwa 10 ambao walichukua nafasi ya sita akiwa amepitwa kwa pointi 0.03 na mrembo wa Marekani. Hii mara ya kwanza kwa mshindi wa Afrika kufika hatua hiyo, Afrika ilitoa washindi wawili tu katika 10 ambao ndio Tanzania na Angola, hiyo inamaanisha kwamba Tanzania mama zetu wanazaa wanawake wazuri hapa Duniani. Mungu awabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tunzo ya zeze ya mwaka 2006 iliyoandaliwa na mfuko wa utamaduni wa Tanzania wasanii wanne wa asasi mbalimbali walitunikiwa wasanii hao ni bibi Loyce Joyce Henry kutoka Ngara, Dr. Martin Muhando kutoka Tanga, Sharrif kutoka Zanzibar na bwana Anania Ngorika kutoka Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Baraza la Kiswahili la Taifa lilitekeleza kazi zifuatazo:

Kuandaa warsha ya lugha kwa Wataalamu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) kwa lengo la kuwianisha matumizi ya maneno ya Kiswahili. Jumla ya maneno 80 yalijadiliwa na kufikiwa mwafaka.

Kuendesha warsha iliyowajumuisha walimu wa Kiswahili kwa wageni ambayo ilifanyika kwa lengo la kufanya maandalizi ya msingi ya kuandika kitabu cha

kufundishia Wageni Kiswahili Hatua ya I. Kazi iliyofanyika ni kuainisha mada za kitabu na uteuzi wa wataalamu wa kuandaa muswada wa kitabu hicho.

Kuendesha semina ya mafunzo kwa wafasiri na wakalimani kumi na tano (15). Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuwapatia wataalamu hao mbinu zaidi za kufanya kazi ya ukalimani na tafsiri kwa umahiri na ufanisi.

Kufanya Maadhimisho ya Tisa (9) ya Siku ya Kiswahili yenye kaulimbiu ya "Kiswahili ni Silaha ya Afrika". Maadhimisho hayo yalitambua mchango wa wataalamu hao wa Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), wa kukuza Kiswahili katika maendeleo ya Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano.

Kutayarisha na kurusha vipindi 52 vya "Lugha ya Taifa", vipindi 52 vya "Kumepambazuka" katika redio na vipindi 52 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" katika televisheni ambavyo vilielimisha na kuhamasisha matumizi fasaha ya Kiswahili.

Kufanya utafiti na kukusanya istilahi 1,800 katika uwanja wa diplomasia na uhusiano wa Kimataifa kwa lengo la kuzisanifu na kuandaa kamusi kwa ajili ya mikutano ya Umoja wa Afrika na kwingineko.

BAKITA, kwa mara ya kwanza ilifasiri Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2006. Kazi hii ilifanywa kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa miezi ya Februari/Machi 2007. Aidha, Baraza lilitoa huduma ya tafsiri za nyaraka mbalimbali kama vile vyeti vya shule na kuzaliwa, hati za ndoa na talaka na kadi za magari kwa asasi mbalimbali zikiwemo za Serikali, mashirika na watu binafsi. Jumla ya hati 500 na nyaraka 50 zilitafsiriwa.

Kutoa na kuratibu huduma za ukalimani na tafsiri katika mikutano ya Umoja wa Afrika pamoja na Bunge la umoja huo lenye makao yake nchini Afrika Kusini.

Ukarabati wa Banda la Maonyesho katika viwanja vya Sabasaba.

Kwa mara ya kwanza, BAKITA ilipeleka mtaalamu wake Makao Makuu ya Umoja wa Afrika kufanya kazi ya uelekezi. Kazi hiyo ilihusu kuisaidia Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuingiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli zake, hivyo kuipa fursa BAKITA kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika Bara la Afrika.

Kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine, kazi iliyofanywa kwa kukusanya makosa katika magazeti ya Uhuru, Mzalendo, Majira, Mwananchi, Rai, Nipashe, Mtanzania, Al Nuur na Kiongozi na pia idhaa za redio za ndani na nje ya nchi. Jumla ya makosa 180 yalibainishwa na kuorodheshwa pamoja na masahihisho yake katika toleo la makala Zingatia Matumizi Sahihi ya Kiswahili.

Kusoma miswada 107 ya vitabu vya Kiswahili vya masomo ya shule za msingi na vyuo na kuvipa ithibati.

Kukamilisha Mpango Mkakati wa Baraza wa miaka Mitano 2007/8 – 2011/12 kwa kukusanya maoni na mapendekezo ya wadau ili kuuboresha.

Kukamilisha rasimu ya pili ya marekebisho ya Sheria Na. 27 ya Kuundwa kwa BAKITA. Rasimu hiyo imejadiliwa katika warsha ya wadau kwa madhumuni ya kuiboresha.

Kukamilisha uandaaji wa itifaki ya kuanzishwa kwa "Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki", kazi iliyofanywa kwa kushirikiana na wajumbe kutoka Kenya na Uganda. Baraza la Mawaziri la Sekta husika la Jumuiya ya Afrika Mashariki lilipitisha itifaki hiyo mwezi Aprili 2007, na Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wameiridhia itifaki hiyo mwezi Juni, 2007 katika mkutano wao wa kilele uliofanyika Kampala, Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Sanaa la Taifa liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984 likiwa ni chombo cha kusimamia na kuhimiza maendeleo ya sanaa nchini. Katika mwaka 2006/2007 Baraza la Sanaa la Taifa lilitekeleza malengo yafuatayo:

Kutoa mafunzo ya uboreshaji sanaa ya muziki, ufundi wa mikono, ngoma, sarakasi na tamthiliya kwa wasanii binafsi. Aidha, mafunzo ya uongozi bora kwa vikundi na vyama vya Sanaa yalitolewa.

Kuhamasisha na kuhimiza uundwaji, usajili, ufufuaji vyama vya wasanii, mapromota, makampuni na wasanii binafsi 2,840 nchini.

Kufanya utafiti katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara na Ruvuma kuelewa maeneo yenye malighafi kwa ajili ya ufinyanzi, ususi na kazi nyingine za sanaa.

Kutoa elimu kwa kutumia sanaa na vipeperushi katika sehemu mbalimbali za burudani nchini kuhusu namna ya kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI.

Kuendelea na kazi ya ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa, Ilala Dar es Salaam.

Kuendelea kutoa elimu ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii mbalimbali. Kwa mwaka 2006/2007 wasanii 330 walipatiwa elimu hiyo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Manyara, Mbeya, Mwanza, Tabora, Pwani, na Tanga.

Kuanza mchakato wa kuhuisha Sheria Na.23 ya mwaka 1984 iliyoanzisha BASATA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Ukaguzi wa Filamu, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza iliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 4 ya mwaka 1976. Katika mwaka 2006/2007 Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuingiza ilitekeleza malengo yafuatayo:

Kuimarisha uongozi na utawala kwa njia ya mafunzo ambapo watumishi wa Bodi walihudhuria matamasha ya filamu na sanaa.

Kulinda maadili ya Utamaduni wa Taifa ambapo takwimu/data/torwi muhimu za fani ya filamu zilikusanywa katika Jiji la Dar es Salaam.

Filamu 17 zilikaguliwa, kanda za video 59 zilipangwa katika madaraja husika, wasanii na wadau 218 walipewa ushauri wa kitaalamu kuhusu fani ya filamu; maonyesho 76 yalipewa vibali halali, miswada (*synopsis*) 6 na tamthilia (*scripts*) 8 zilisomwa; Bodi ilichapisha vipeperushi 2,000 vya "Ijue Bodi ya Filamu" na kuvisambaza mikoani na wilayani.

Kutoa elimu ya jamii kwa wadau wa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ambao ni pamoja na watengenezaji wa filamu, wasambazaji wa filamu na video, wamiliki wa kumbi na majumba ya sinema na vituo vya televisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Sanaa Bagamoyo, kwa mwaka 2006/07 Chuo cha Sanaa Bagamoyo kilitekeleza majukumu yafuatayo:-

Kiliendesha mafunzo ya stashahada kw a wanafunzi 93 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 120 walio kazini katika sehemu mbalimbali nchini.

Kiliendesha Tamasha la 25 la Kimataif a la Sanaa Bagamoyo lililofanyika mwezi Septemba 2006. Tamasha hilo lilifunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Chuo cha Sanaa kimeanza kufanya ukarabati wa majengo ya ukumbi wa maonyesho yaliyoungua baada ya kumpata mkandarasi wa majengo.

Aidha, Chuo cha Sanaa kiko katika hatua ya mwisho ya kugeuzwa kuwa Wakala wa Serikali wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Utamaduni, Mfuko wa Utamaduni Tanzania ulianzishwa mwaka 1998 na Serikali kwa lengo la kuhamasisha na kuchochea kukua kwa fani za utamaduni. Katika kipindi cha 2006/2007 Mfuko wa Utamaduni ulitekeleza malengo yafuatayo:

Bodi ya Wadhamini ya Mfuko iliidhinisha ufadhili wa miradi 61 iliyotengewa Shilingi 394,446,500. Kwa kuwa fedha hutolewa kwa awamu miradi 33 ilipewa jumla ya shilingi 169,831,407/=. Baadhi ya miradi iliyofadhiliwa na Mfuko

imeweza kuendesha mafunzo kuhusu hakimiliki, ujuzi wa kutengeneza bidhaa bora, umuhimu wa urithi wa asili na jinsi ya kufufua na kuhifadhi urithi huo.

Miradi mingine imechapisha vitabu vya hadithi, kamusi, mapishi ya kiasili, kumbukumbu na historia ya ngoma za asili Zanzibar na uandishi wa vitabu kwa ajili ya wasioona. Orodha ya vikundi na fani zilizoidhinishiwa misaada Kimkoa zimeonyeshwa katika Kiambatisho Na. *VI*.

Kutambua, kuenzi na kutunukia Tuzo ya Zeze. Watu watano na asasi mbili zilizojitokeza katika kufanya kazi zilizo bora na zinazostahili kutunukiwa. Watunikiwa hao ni:

- Bibi Loyce Joel Henry kutoka Ngara.
- Dkt. Martin Muhando kutoka Tanga.
- Prof. Abdul Sheriff kutoka Zanzibar.
- Bw. Anania Ngoliga kutoka Mpwapwa.

Aidha, asasi zilizotunukiwa ni pamoja na:-

- Kiroyera *Culture Tourism* kutoka Bukoba.

- Mradi wa Vitabu vya Watoto kutoka Dar-es Salaam.

· Kuendesha mafunzo na semina kwa wadau mbalimbali kwa nia ya kuongeza ujuzi na kusimamia na kutekeleza miradi midogo midogo, pamoja na kuongeza ufahamu na maana, umuhimu na nafasi ya utamaduni katika mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kituo cha utafiti cha simulizi asilia na lugha za Taifa cha Mashariki ya Afrika (*EACROTANAL*), baada ya takribani miaka sita ya maandalizi, makubaliano ya kukianzisha Kituo cha Utafiti wa Simulizi Asili na Lugha za Kitaifa cha Mashariki ya Afrika yalitiwa saini mwezi Septemba, 1977.

Kituo kilianzishwa ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka Kumi (1972 – 1982) wa *UNESCO* kuhusu simulizi asilia na ukuzaji wa lugha za Kiafrika. Kwa kutambua umuhimu wa Mpango huo baadhi ya nchi za ukanda wa Mashariki mwa Afrika, zikiungwa mkono na *UNESCO* na Umoja wa Afrika, zilisaini mkataba wa kuanzishwa kituo hicho. Nchi wanachama anzilishi zilikuwa tisa: nazo ni Burudi, Comoro, Ethiopia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Somalia, Sudani na Tanzania. Lengo kuu la Kituo ilikuwa ni kuwa na chombo cha kupashana habari, kuhifadhi kumbukumbu na chanzo cha utafiti katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuelekea katikati ya miaka ya 1990, shughuli za Kituo zilianza kufifia kutokana na sababu nyingi, lakini kubwa ni kupungua kwa michango ya nchi wanachama. Katika jitihada za kukifufua, nchi wanachama zilikutana mwaka 2004 mjini Zanzibar na kuomba Tanzania ikilee Kituo kwa muda wa

miaka miwili yaani 2005-2006 na kukiweka katika hali itakayowezesha nchi wanachama kufufua uanachama wao.

Aidha, iliundwa Kamati ya Muda ya kusimamia shughuli za kufufua Kituo katika kipindi hicho. Kazi ya kwanza ya Kamati imekuwa ni kusimamia na kuratibu ajira ya watendaji wakuu. Katika mwaka 2007/2008 Serikali itaendelea na mchakato wa kufufua kituo hicho kwa kuitisha mkutano wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya michezo, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilikuwa na jukumu la kuendeleza Michezo kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995, ambapo yafuatayo yalitekelezwa:-

Kuendelea kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Eneo Changamani la michezo ambalo ni ujenzi wa uwanja wa kisasa wenye viwango vya kimataifa kwa ajili ya mpira wa miguu na riadha. Uwanja huo wenye uwezo wa kuchukua jumla ya watu 60,000 wakiwa wamekaa, utakabidhiwa kwa Serikali mwaka huu. Uwanja umekaguliwa na ujumbe wa Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Duniani (*FIFA*) ambao uliridhika kuwa ni moja kati ya viwanja bora duniani. Pia, ujumbe toka nchi za Zambia na Msumbiji uliutembelea uwanja wetu na kufurahishwa sana. Katika hali hiyo, uwanja wetu upo katika nafasi nzuri ya kupata michezo ya kirafiki kutoka nchi mbalimbali na ya kujipima nguvu baina ya timu zitakazoshiriki Kombe la Dunia huko Afrika ya Kusini mwaka 2010.Aidha, Wizara imesimamia ukarabati wa Uwanja wa Taifa ambapo eneo la kuchezea mpira linawekwa majani bandia (*artificial turf*) ili kuuwezesha uwanja huo kutumika kwa wakati wote na kwa muda mrefu zaidi. Ukarabati huu unafanyika kwa msaada wa *FIFA*.

Kuandaa maadhimisho ya Siku ya Michezo Tanzania iliyofanyika tarehe 21 Septemba, 2006 katika Uwanja wa Karume ulioko Ilala, jijini Dar es Salaam. Yalikuwepo maonyesho ya shughuli za michezo, maandamano ya wanamichezo na hotuba za viongozi.

Kuiandaa Timu ya Taifa iliyoshiriki michezo ya 9 ya Mataifa ya Afrika iliyofanyika huko Algeria mwezi Julai 2007. Timu ya watu 30 wakiwemo wachezaji na viongozi imeshiriki. Michezo tuliyoshiriki ni Ngumi, Michezo kwa Watu wenye Ulemavu (Paralimpiki), Riadha, Mpira wa meza na Judo. Tanzania imefanikiwa kutwaa medali moja ya fedha katika mbio za nusu marathoni (kilomita 21) na kuiweka Tanzania nafasi ya 31 kati ya nchi 52 zilizoshiriki.

Kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo (ualimu, uamuzi, uongozi bora na huduma ya kinga na tiba kwa wanamichezo). Jumla ya vyama 20 vya ngazi ya taifa vilipatiwa mafunzo hayo. Pia, semina elekezi kwa ajili ya uongozi na utawala bora zilitolewa kwa maofisa michezo, walimu wa michezo wa shule za msingi na za sekondari na kwa viongozi wa michezo kutoka taasisi mbalimbali za mikoa yote Tanzania Bara na wawili kutoka Tanzania Visiwani. Jumla ya watu 230 walifaidika na semina hizo.

Kusajili vyama na vilabu vya michezo kulingana na Sheria na Kanuni za michezo. Kiambatisho Na.VII ni orodha ya vyama na vilabu vya michezo vilivyosajiliwa kimkoa kuanzia mwaka 2000 – 2006.

Kuendelea kudurusu katiba za vyama na vilabu vya michezo ambapo jumla ya katiba 158 zilipokelewa, kutolewa ushauri kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na kisha kusajiliwa baada ya kukidhi matakwa ya katiba zitakazosaidia kupunguza migogoro katika vyama na vilabu hivyo.

Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo – Malya. Hivi sasa mafunzo ya Stashahada ya michezo sita inaendelea kwa wanafunzi 36. Michezo hiyo ni Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono, Mpira wa Wavu, Mpira wa Kikapu, Netiboli na Riadha.

Kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kushiriki mashindano ya Kitaifa na Kimataifa kwa kuiandaa timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu wa Akili *(Special Olympics*), yenye jumla ya watu 30 (wachezaji 24 na viongozi 6) itakayoshiriki katika mashindano ya Dunia yatakayofanyika huko Shanghai, China kuanzia tarehe 27 Septemba hadi 13 Oktoba 2007. Wachezaji hao ni wa Riadha na Mpira wa Miguu.

Kuwapima wanamichezo afya zao na kuwapa ushauri, ambapo jumla ya wanamichezo 3,500 wamepimwa kufikia Mei, 2007.

(i) Kufufua na kuimarisha michezo ya jadi ambapo kitabu cha mchezo wa Bao kimechapishwa. Aidha, utafiti kuhusu mchezo wa mieleka umeanza katika mkoa wa Kagera na rasimu ya kwanza ya sheria na kanuni za mchezo huo imepatikana.

(ii) Kusimamia maandalizi ya Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ambapo kocha wa timu hiyo na msaidizi wake wameajiriwa. Aidha, kocha wa timu ya Vijana naye ameajiriwa. Makocha wote hawa watatu ni kutoka nchini Brazili. Kutokana na kuwepo makocha hawa, kiwango cha mpira wa miguu cha Tanzania kimataifa kimepanda kutoka nafasi ya 165 mwanzoni mwa mwaka 2006 hadi ya 105 hivi sasa. Katika Afrika Tanzania inashika nafasi ya 28 na katika Afrika Mashariki inashika nafasi ya tatu ikitanguliwa na Uganda na Ethiopia.

Ili kuimarisha uwezo wa timu ya taifa kufanya vizuri katika mchezo wake na Msumbiji Serikali kwa kushirikiana na Serengeti inapeleka timu yetu *Denmark* na *Uswis* kwa ajili ya mazoezi. Hivi leo kocha wetu anatangaza majina ya kikosi hicho kabambe cha kwenda kujinoa huko *Denmark* na Uswisi.

Timu ya Taifa ya Ngumi ilishiriki katika mashindano ya Jumuiya ya Madola huko Uingereza ambayo ilipata medali nne na kushika nafasi ya tano kati ya nchi 20 zilizoshiriki na ya kwanza katika Afrika. wachezaji waliopata medani hizo ni: Amos Godwin Mwakapata – medali ya fedha, hamshangilii jamani? Mpaka niombe?Petro

Mtagwa – medali ya shaba, Ally Kimwaga – medali ya shaba na Hassan Fikiri – medali ya shaba. (*Makofi*)

Katika jitihada za kuinua viwango vya michezo yote nchini, Serikali itajitahidi kuajiri makocha wa michezo mbalimbali kwa awamu kutegemeana na uwezo wa fedha. Napenda kuwahakikishia Watanzania kuwa lengo la Serikali ya Awamu ya Nne ni kuhakikisha kuwa michezo yote inapata msukumo mpya.

Mchezo wa Gofu wamepata kocha, Bwana Charles Farah kutoka Ujerumani anayetoka na Klabu ya Jimkana kwa mkataba wa miaka miwili. Chama cha *Tennis* kimepata kocha bwana Pins Madema kutoka Zimbabwe, yeye ana mkataba wa miaka 8 analipwa na shirikisho la *Tennis* duniani. Serikali kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani imepata mtaalamu bwana Hans Peter ambaye anafanya kazi ya kuibua vipaji katika michezo ya riadha na mpira wa mikono kwa mkataba wa miaka miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maneno kwamba Serikali inashabikia tu mpira wa miguu lakini ushahidi ni kwamba sasa hivi tumejaribu kutoa machoka katika michezo mbalimbali ikiwemo *tennis, criket* na kadhalika.

(iii) Kushirikiana na wadau kuibua na kukuza vipaji ambapo katika mpira wa miguu tumeanzisha mashindano ya *Copa Coca Cola* kwa vijana wenye umri wa chini ya miaka 17. Jumla ya timu 776 katika nchi nzima zilishirikishwa katika mashindano ya ngazi ya Wilaya. Katika ngazi ya Taifa, timu 28 za Mikoa zikiwa na jumla ya wachezaji 560 zilishiriki. Mkataba huu wa *Copa Coca Cola* ni wa miaka mitano kuanzia Januari, 2007 na mashindano haya yanatumika kuteua wachezaji wa Taifa kwa timu za umri mbalimbali ambao baadaye wataingia kwenye timu ya Taifa (Taifa *Stars*). Mashindano ya mwaka huu (2007) yametoa wachezaji watatu bora ambao wamekwenda Brazil kwa mafunzo zaidi. Wachezaji hao naomba muwashangilie pia: Richard Machumu kutoka Mara – Golikipa bora; Abdallah Bunu kutoka Ilala – Mfungaji bora; Nasoro Mhagama kutoka Ruvuma – Mchezaji bora. Sijui kama ana uhusiano na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, sijui. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mtoto wa dada yake.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Hongera Mwenyekiti wetu.

(iv) Wizara inajitahidi kutafuta wadhamini kwa michezo mingine ili kuinua viwango vya michezo hiyo kwa kuwekeza kwa vijana na watoto.

(v) Kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika mafunzo na mikutano muhimu nje ya nchi ambapo Chama cha Mpira wa wavu walikwenda China, mpira wa meza walikwenda Ujerumani, *Paralimpiki* walikwenda Misri na '*Special Olympics'* walikwenda Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika*,* Baraza la Michezo la Taifa liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na Marekebisho yake katika Sheria Na. 6 ya mwaka 1971. Katika mwaka 2006/2007 Baraza la Michezo la Taifa lilitekeleza yafuatayo:

(i) Kufanya utafiti katika wilaya za Kilindi, Hai, Simanjiro, Kondoa, Singida, Mpwapwa, Morogoro na Iringa ili kubaini vipaji vilivyopo na changamoto zinazokwamisha maendeleo ya michezo. Utaratibu huu utaendelea katika mikoa na wilaya nyingine hatua kwa hatua.

(ii) Kuendesha mafunzo kwa viongozi wa vyama 20 vya michezo vya Taifa kuhusu uandaaji wa mpango wa kazi, uanzishwaji wa timu za vijana, utawala bora katika Michezo na Elimu dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

(iii) Kuendesha na kuratibu mjadala kuhusu Mustakabali wa Michezo katika ngazi za wilaya na mikoa yote ya Tanzania Bara ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mjadala wa Taifa uliopangwa kufanyika mwezi Oktoba, 2007.

(iv) Kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi wake na wafanyakazi wenye ajira za kudumu au mikataba maalumu na Vyama vya Michezo ngazi ya Taifa. Mafunzo hayo yalihusu sheria na taratibu za kazi pamoja na elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI sehemu za kazi.

(v) Kuendeleza mazungumzo na viongozi wa "*UK Sports"* na Shirikisho la Vyama vya Michezo la *Norway (NIF)* kuhusu ushirikiano kwa lengo la kuanzisha miradi endelevu ya michezo. Aidha, *NIF, UK Sport* na *BMT* walifanya ziara ya pamoja katika Mkoa wa Iringa na kushiriki katika Tamasha la Michezo la Watu wenye Ulemavu.

(vi) Kusimamia na kufanikisha kufanyika kwa chaguzi za Vyama vya Michezo ya Riadha (*RT),* Kriketi (*TCA),* Kamati ya Olimpiki (*TOC*), Mashirika ya Umma (SHIMMUTA), Ngumi *(BFT*), Baiskeli (CHABATA) na Wizara (SHIMIWI).

(vii) Kushirikiana na Kamati ya *Paralimpiki* ya Tanzania *(TPC)* kuendesha mafunzo kwa Walimu wa Michezo kwa watu wenye Ulemavu Jijini Dar es Salaam na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara imeendelea kukamilisha upatikanaji wa wafanyakazi wenye sifa, kwa kuajiri watumishi wapya kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa Ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nafasi wazi zilizokuwepo ni 41, kati ya hizo nafasi 19 zimejazwa. Nafasi 22 hazikupata waombaji wenye sifa na mchakato wa kuzijaza unaendelea. Aidha, watumishi kumi walipandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** ili kuwajengea uwezo watumishi, Wizara iliwagharamia watumishi 14 mafunzo ya muda mfupi na mrefu, mafunzo ya Shahada ya kwanza watumishi wawili, Shahada ya Uzamili watumishi tisa, Shahada ya Uzamifu mtumishi mmoja, Stashahada ya kawaida mtumishi mmoja, na Cheti mtumishi mmoja. Vilevile Wizara imepeleka jumla ya watumishi ishirini na nne kwenye mafunzo

mbalimbali ya muda mfupi. Aidha, watumishi watatu wamelipiwa gharama za kujiendeleza wenyewe kwa lengo la kupata elimu ya sekondari ambayo ndiyo kiwango cha chini kilichowekwa na Serikali kwa ajira ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika jitihada za Wizara kuhamasisha na kuwaelimisha watumishi juu ya ugonjwa wa UKIMWI na namna ya kupambana nao, Wizara iliunda Kamati ya UKIMWI na kuzinduliwa rasmi tarehe 10 Novemba, 2006. Vilevile, kwa kushirikiana na *TACAIDS*, Wizara iliendesha semina sita za UKIMWI kwa watumishi wa ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imewezesha uundwaji wa tawi la *TUGHE* na kuingia mkataba wa kuunda Baraza la Wafanyakazi, lengo likiwa ni kuwawezesha watumishi kushauri uongozi wa Wizara juu ya mambo mbalimbali yanayoihusu Wizara na maslahi yao. Baraza la Wafanyakazi lilizinduliwa rasmi tarehe 1 Machi, 2007. Wajumbe hao walipatiwa mafunzo juu ya Utawala Bora na Kanuni na Taratibu za utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, watumishi wote wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma.

Wizara imeendelea kupunguza mianya ya rushwa na kuhakikisha inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma. Vilevile, Wizara imekamilisha kuunda Kamati za Uadilifu za Wizara na Taasisi zake. Katika kuwawezesha watumishi kiuchumi, Wizara imeanzisha mchakato wa kuunda Ushirika wa Kuweka na Kukopa - *SACCOS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Habari kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara yangu, inatarajia kuimarisha utendaji wa kazi ya Tovuti ya Wananchi kwa kuongeza vitendea kazi na kuwapa mafunzo watendaji wake ili wawe na ujuzi mkubwa zaidi wa kuwatumikia wananchi. Wizara pia inatarajia kukamilisha mradi wa kukarabati Maktaba ya Picha na kuanza kuhifadhi picha katika mfumo wa elektroniki. Mfumo huu unawezesha mtu yeyote kupelekewa picha za matukio ya kitaifa na Serikali mahali popote duniani ikiwa ataomba.

Kwa upande wa mitambo, TVT itaongeza usikivu wa redio katika masafa ya *FM* kwenye mikoa ya Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Mara, Mbeya, Tabora, Tanga na Mwanza. Imebidi kufunga mitambo ya *FM* katika Mikoa hiyo kwa vile tayari kuna minara ya kurushia matangazo ya televisheni na hivyo kuokoa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendeleza juhudi hizo, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Taasisi ya Utangazaji itafanya mabadiliko makubwa katika matangazo ya taarifa za habari pamoja na habari za matukio. Kila mkoa utapewa mwandishi wa habari maalumu atakayekuwa na vifaa bora vya kisasa vya kunasia sauti na kupeleka habari motomoto zikiwemo nyingi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Radio Tanzania itatangaza moja kwa moja hotuba za viongozi wakuu wa Serikali kutoka popote pale walipo nchini wakati wowote. Juhudi pia zitafanywa kuvutia vijana wengi kuangalia na kusikiliza matangazo ya Radio Tanzania na Televisheni ya Taifa kwa kuimarisha matangazo ya michezo, hasa mpira wa

miguu, kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Mipira, *TFF*. Sambamba na hayo, TVT itatangaza moja kwa moja, kwa mara ya kwanza mechi za kandanda za ligi ya Uingereza ambayo hupendwa na wengi, si tu hapa nchini, bali duniani kote.

Hali kadhalika itaanzishwa idhaa maalumu na bora ya matangazo kwa lugha ya Kiingereza itakayosikika katika miji michache yenye kuishi wageni ambao hupendelea zaidi kutumia lugha ya kiingereza kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma, Kilimanjaro, Tanga na Mbeya. Baadaye wigo wa utangazaji utapanuliwa kwa miji mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/08, Taasisi ya Utangazaji Tanzania itafanya mipango ya kukarabati ofisi zake kadhaa ambazo zimechakaa ikiwa ni pamoja na kukamilisha majengo ya ofisi ya Taasisi ya jijini Dar es Salaam yaliyoko Mikocheni yaliyosimama kwa miaka kadhaa sasa. Mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kuwa makao makuu ya Taasisi. Kwa jumla huu utakuwa mwaka muhimu wa kufanya mabadiliko makubwa katika utangazaji wa Radio Tanzania na TVT, hasa kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08 Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN*) itafanya yafuatayo:-

(i) Kununua jengo la uchapaji kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF).*

(ii) Kumalizia kazi ya kuorodhesha machapisho ya TSN yaliyonakiliwa kielektroniki.

(iii) Kuongeza kasi ya ukusanyaji madeni ambayo mengi yanadaiwa toka Serikali na Taasisi zake.

(iv) Kuzindua upya magazeti ya Kiingereza kwa kuyapa sura mpya.

(v) Kuanzisha uchapaji wa kibiashara wa magazeti ya wamiliki wengine.

(vi)Kusadia Halmashauri za Wilaya kuanzisha magazeti na machapisho ya Wilaya/Kanda/Mkoa. Halmashauri kadhaa zimeonyesha nia ya kushirikiana na Kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni itaendelea kukuza, kuendeleza na kueneza utamaduni kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa Tano wa Sekta ya Utamaduni utakaofanyika mwezi Novemba, 2007.

(ii) Kuratibu na kusimamia maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Ulimwenguni ambayo huadhimishwa tarehe 21 Mei kila mwaka.

(iii) Kuratibu na kusimamia matamasha madogo madogo katika shule za sekondari 12, shule za msingi 6 na chekechea 4 kwa lengo la kuibua vipaji katika sanaa za ufundi, sanaa za maonyesho na muziki.

(iii) Kufanya utafiti wa lugha za asili katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Tanga ili kubaini maneno yatakayoweza kutumika katika Kiswahili badala ya maneno yanayotatanisha kama vile simu ya kiganjani na simu ya mkononi na yale ya kigeni.

(iv) Kuendeleza utafiti wa kubaini hekima za asili zinazoweza kuboresha uandaaji wa sheria mbalimbali katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Mbeya.

(v) Kufanya utafiti wa kutambua urithi wa utamaduni usioshikika na kuandaa orodha ya maeneo husika. Utamaduni usioshikika ni pamoja na mila na desturi, hadithi, lugha, mashairi na matambiko. Utafiti huo utafanyika katika wilaya za mikoa ya Arusha na Manyara.

(vi) Kuendesha warsha za mafunzo kwa maofisa utamaduni wa wilaya 19 katika mikoa minne, ambayo ni Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma, juu ya uhifadhi na utunzaji wa kumbukumbu za utafiti wa mila na desturi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/08 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kufanya semina ya matumizi ya Kiswahili Sanifu katika Biashara.

(ii) Kusanifu istilahi mchanganyiko zenye utata.

(iii) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya ‘Lugha ya Taifa’, vipindi 52 vya ‘Kumepambazuka’ katika redio na vipindi 52 vya ‘Ulimwengu wa Kiswahili’ katika televisheni.

(iv) Kuandaa na kufanya semina ya mafunzo kwa wakalimani na wafasiri 20.

(v) Kuandaa na kufanya warsha ya wahariri wa vitabu vya kiada vya kufundishia shuleni.

(vi) Kuchapisha kitabu cha Mwongozo wa Waandishi uliokusudiwa kuwaelimisha waandishi mbalimbali, walimu na wanafunzi kuhusu mbinu za uandishi sahihi, matumizi ya vituo na istilahi.

(vii) Kusanifu istilahi katika uwanja wa diplomasia na uhusiano wa kimataifa na kuchapisha Kamusi ya Diplomasia.

(viii) Kuhariri muswada wa Kitabu cha Kiswahili kwa Wageni Hatua ya I na kukichapisha.

(ix) Kusoma miswada ya vitabu vya taaluma na kuipa ithibati.

(x) Kuratibu na kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mikutano ya Kimataifa na katika shughuli za mashirika, kampuni na watu binafsi.

(xi) Kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine.

(xii) Kuandaa mkutano wa kimataifa wa Idhaa za Kiswahili Duniani ambao utafanyika, kwa mara ya kwanza**,** nchini mwezi Novemba, 2007. Tunakusudia kufanya mkutano wa kimataifa wa idhaa zote za Kiswahili duniani hapa Tanzania ili kuwa pamoja na kushirikiana na kusaidia kutumia Kiswahili fasaha na kubadilishana uzoefu. Ni jambo kubwa sana hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika*,* Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Katika mwaka 2007/2008 Baraza la Sanaa la Taifa litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti na uhifadhi wa makala ya nyaraka za Sanaa.

(ii) Kuendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya 1984.

(iii) Kuhuisha Muundo wa Utumishi wa Uendeshaji wa Baraza.

(iv) Kuraghibisha wasanii na watumishi wa BASATA kuhusu kujikinga na maambuziki ya virusi vya UKIMWI.

(v) Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa za Maonyesho, Ilala Dar es Salaam.

(vi) Kukuza stadi za usanii, uongozi na utawala wa shughuli za sanaa kwa wasanii 200 wa muziki, maonyesho na ufundi.

(vii) Kuendeleza mafunzo ya utekelezaji wa shughuli za Sanaa kwa Maofisa Utamaduni 60 kutoka Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa na Kigoma.

(viii) Kuendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wasanii utakaofanyika mwezi Mei, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu. Katika mwaka 2007/2008 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza itatekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kukagua filamu na kanda za video 5,000, vikundi vya sanaa za maonyesho 1,000, majumba ya sinema 21 na kutoa ushauri wa kuzingatia maadili kwa waandaaji 300 wa vipindi vya maigizo na programu mbalimbali za Televisheni.

(ii) Kuendelea na mchakato wa marekebisho ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza.

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya maadili ya filamu na utamaduni kwa wadau wa filamu na sanaa za maonyesho kupitia mpango shirikishi wa mikutano, semina, warsha na vipeperushi, kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa.

(iv) Kuendelea na zoezi la kukusanya takwimu za fani ya filamu na sanaa za maonyesho, hususan vikundi vya wasanii wa filamu, wamiliki wa majengo ya sinema, wamiliki wa vituo vya televisheni na wasambazaji wa filamu katika ya mikoa ya Morogoro na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Katika mwaka 2007/2008 Chuo cha Sanaa Bagamoyo kitatekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 100 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 150 walio kazini.

(ii) Kuwa mwenyeji wa Tamasha la Bagamoyo la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania litakalofanyika Oktoba, 2007.

(iii) Kuendelea kukamilisha ukarabati wa Jengo la Maonyesho ya Sanaa lililoungua.

(iv) Kujenga mabweni matatu ya wanafunzi na nyumba moja ya Mkuu wa Chuo.

(v) Kuanza rasmi kuwa Wakala wa Serikali wa Sanaa na Utamaduni Bagamoyo kwa kifupi TASUBA.

(vi) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa maonyesho wenye uwezo wa kuchukua watu 1500 kule Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kufuatia matukio ya baadhi ya wapiga muziki kupiga kelele na kuzidisha muda ulioruhusiwa na Sheria katika mji wa Dar es Salaam, uongozi wa Jiji la Dar es Salaam ulichukua hatua kadhaa za kuwaita na kuwaonya wamiliki wa kumbi za burudani. Kutokana na hatua hizo zilizochukuliwa kelele za muziki zimepungua kwa kiwango kikubwa sana, tunawapongeza sana wapiga muziki Dar es Salaam.

Hata hivyo, wapo wafanyabiashara wachache ambao wanapotosha kwa makusudi maagizo ya Serikali ya kupunguza kelele za muziki kwa kudai kuwa eti Serikali imepiga marufuku upigaji wa muziki. Serikali haikupiga marufuku upigaji wa muziki Dar es Salaam bali imesema ifuate taratibu na sheria kwa heshima na taadhima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusudia kuunda tume ya wataalamu kuainisha sheria mbalimbali zinazohusu uendeshaji wa biashara za vileo na burudani na kupendekeza marekebisho yatakayozingatia mahitaji halisi ya sasa.

Wakati zoezi hili linafanyika Serikali inaagiza Sheria zilizoko zizingatiwe na kuheshimiwa. Agizo hili halilengi tu wamiliki wa kumbi za burudani Dar es Salaam bali pia wafanyabiashara wa sekta ya burudani nchi nzima na mikoani pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Mfuko wa Utamaduni Tanzania utatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kufadhili miradi na shughuli za Utamaduni.

(ii) Kutambua, kuenzi na kutunuku watu na asasi zinazojitokeza kwa kufanya kazi za kitamaduni zilizo bora na za kutukuka.

(iii) Kujenga mtandao na ushirikiano wa watu wanaothamini utamaduni wetu ili kushawishi jamii kuchangia kwa hali na mali shughuli za utamaduni.

(iv) Kuendesha semina za wadau ili kuimarisha mfumo na huduma za Mfuko kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Michezo kwa mwaka 2007/2008, Wizara yangu imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia awamu ya pili ya ujenzi wa eneo Changamani la Michezo linalotarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha na litakalojumuisha:-

(ii) Uwanja wa kisasa wa maandalizi *(warm–up ground).*

(iii)Uwanja wa ndani wa kisasa kwa ajili ya michezo ya mpira wa kikapu, mpira wa wavu, ngumi, mpira wa meza, mpira wa vinyoya, netiboli, mpira wa mikono na mazoezi ya viungo vya mwili.

(iv) Mabwawa mawili ya kuogelea yenye viwango vya Olimpiki.

(v) Viwanja vya mazoezi ya mpira wa miguu: Viwanja vya mpira wa magongo; uwanja wa kriketi; hoteli na Kumbi za mikutano; Chuo cha Michezo na hosteli yenye vyumba 750 na Vyumba vya biashara.

(vi) Kuendelea na ukarabati wa Uwanja wa Taifa wa zamani ili uwe katika viwango vya kimataifa.

(vii) Kuandaa na kusimamia shughuli za Siku ya Michezo Tanzania, ambayo ni tarehe 21 Septemba, 2007.

(viii) Kushiriki kwa Timu ya Taifa katika michezo ya Dunia ya "*Special Olympics"* itakayofanyika huko Shanghai, China mwezi Septemba – Oktoba 2007.

(ix) Kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa fani mbalimbali za michezo zikiwemo ukocha, uamuzi, uongozi na menejimenti, kinga na tiba na miundombinu kwa lengo la kuinua viwango vya taaluma hizo katika vyama, vilabu, wilaya na mikoa yote nchini.

(x) Kuendelea kukarabati miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya.

(xi) Kupima afya za wanamichezo na kutoa ushauri wa kinga na tiba ya majeraha na magonjwa yatokanayo na ushiriki wa michezo. Aidha, kutoa ushauri wa namna ya kuitumia michezo kuwa tiba ya magonjwa.

(xii) Kuendelea kufanya utafiti na kuimarisha michezo ya jadi ya mieleka na kulenga shabaha katika mkoa wa Kagera.

(xiii) Kusimamia maandalizi na ushiriki wa timu ya taifa ya mpira wa miguu inayojiandaa kwa michezo ya kufuzu kwenye fainali za mataifa ya Afrika zitakazofanyika huko Ghana mwaka 2008.

(xiv) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutumia michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Michezo. Katika mwaka 2007/2008 Baraza la Michezo la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa mpango wa muda mfupi, kati na mrefu wa kuendeleza michezo nchini.

(ii) Kuendelea na maandalizi na kuendesha Mjadala wa Taifa kuhusu Mstakabali wa Michezo nchini.

(iii) Kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika michezo na kuchangia kwa hali na mali uendeshaji wa michezo katika maeneo yao.

(iv) Kuhamasisha vikundi mbalimbali vya michezo katika Wilaya zote kwa lengo la kuanzisha miradi endelevu.

(v) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kununua vitendea kazi kwa lengo la kuboresha utendaji wa Baraza la Michezo la Taifa katika kutoa huduma bora kwa wateja wake.

(vi) Kuhamasisha jamii kwa lengo la kustawisha usawa na uwiano wa kupata fursa zilizo sawa katika michezo.

(vii) Kusambaza kwenye Wilaya zote Sheria Na. 12 ya BMT na rasimu ya marekebisho ya Sheria hiyo ili kupata maoni na mapendekezo ya kuboresha.

(viii) Kutoa ushawishi wa uanzishwaji wa vituo vya michezo (*Sports Academies*) kwa lengo la kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana mijini na vijijini na hatimaye kukuza ajira kwa wanamichezo kitaifa na kimataifa.

(ix) Kuendelea kutafuta wabia wa kuchangia miradi ya maendeleo ya michezo na ile ya kutumia michezo kwa maendeleo ya jamii.

(x) Kutafuta wabia na kuchangia katika utekelezaji wa mipango ya Baraza kuanzisha miradi endelevu.

(xi) Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa vikundi mbalimbali vya michezo, kwa kutumia mikutano, semina na matamasha ya michezo kwa kushirikiana na asasi zinazojihusisha na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Michezo ya mwaka 1995 inatambua uendelezaji wa michezo katika ngazi ya kijiji hadi mkoa. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara yangu inashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa vyama vya michezo mbalimbali vinakuwepo, vinaendesha shughuli zao kwa mujibu wa katiba zao na mashindano ya michezo hiyo inafanyika kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa.

(ii) Kuhakikisha maeneo ya viwanja yanatengwa kuanzia ngazi za vijiji, yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na viwanja vilivyopo vinakarabatiwa ili vitumike vizuri kwa kuinua viwango vya michezo. Aidha, viwanja vya michezo vilivyovamiwa vinarejeshwa.

(iii) Kuwa na vituo vya kuibua vipaji vya watoto, kuvikuza na kuwa na mashindano ya watoto na vijana wa umri wa miaka 14, 16, 18, 20 na 23.

(iv) Kuhakikisha kuwa mafunzo ya wataalamu wa michezo yaani walimu, makocha na madaktari yanaendeshwa.

(v) Kuwa na timu za kombaini za vijiji, kata, tarafa, wilaya na mkoa zilizoandaliwa vizuri. Aidha, shule zote za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu viwe na timu na zishiriki mashindano kuanzia ngazi ya shule hadi mkoa na hivyo kuimarisha mashindano ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA), Sekondari (UMISETA) na vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA).

(vi) Kila Halmashauri iwe na bajeti ya kuendeleza michezo na iajiri Ofisa Michezo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za michezo hapa nchini, naomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie katika suala hili.

(v) Kushiriki kikamilifu katika mjadala wa Mustakabali wa Michezo Nchini ambapo wenyeviti wa kamati za michezo za mikoa na wilaya, yaani Makatibu Tawala wa mikoa na wilaya, watakuwa wenyeviti wa mijadala hiyo.

(vi) Kusimamia usajili wa vyama na vilabu vya michezo ambapo Msajili Msaidizi, ambaye ni Ofisa Michezo wa Wilaya, atatoa ushauri wa kitaalamu katika kuandaa katiba na hatimaye kuzipeleka kwa Msajili Mkuu kwa usajili kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa kina na mpango wa wizara yangu kwa mwaka 2007/2008 upo kwenye ukurasa wa 44 hadi 93 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maendeleo ya Watumishi katika mwaka 2007/2008, Wizara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya ugojwa wa UKIMWI na kuwahamasisha namna ya kupambana nao na kutoa huduma ya msaada kwa watumishi waathirika;

(ii) Kuendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi watakaostahili kulingana na Miundo ya Utumishi ya kada zao na kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

(iii) Kukamilisha upatikanaji wa watumishi wenye sifa kujaza nafasi wazi kwa mujibu wa ikama iliyoidhinishwa na kwa kuzingatia mwongozo wa masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma.

(iv) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kugharimia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

(v) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi kwa uwazi na kwa matokeo (*Open Performance Review Apprasal System - OPRAS*).

(vi) Kuendesha mafunzo kuhusu Utawala Bora na kusimamia utendaji kazi wa watumishi hao kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa.

(vii) Kuendesha mikutano ya wafanyakazi wote na ile ya Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, sasa naomba kutoa shukrani. Huduma zinazotolewa na Wizara yangu zinawagusa Watanzania wote kwa namna mbalimbali. Aidha, zinazigusa Wizara nyingine zote kwani shughuli za Wizara yangu ni za mtambuka. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ya mawazo na ushauri walionipa ndani na nje ya Bunge kwa nia ya kuendeleza huduma tunazotoa. Wizara itaendelea kuyapokea na kuyafanyia kazi mapendekezo, ushauri na maoni yatakayoendelea kutolewa na Waheshimiwa Wabunge ili tuendelee kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kupongeza mashirikiano mazuri yaliyopo kati ya Wizara yangu na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Serikali na Mapinduzi Zanzibar. Mtakumbuka kwamba safari hii katika mashindan yaliyofanyika Burkina Faso, Naibu Waziri wa Michezo wa Zanzibar alikuwa ndiye kiongozi wa timu yetu hii, huu ni ushahidi kwamba sisi tunaimarisha Muungano kwa vitendo. Mashirikiano hayo yamehusisha mikutano ya sekta ya utamaduni, matamasha ya sanaa na utamaduni, kubadilishana vipindi vya redio na TV na pia watangazaji. Aidha, kwa upande wa michezo, tumekuwa na mabadilishano ya timu mbalimbali na uzoefu. Ni azma ya Wizara yangu kuimarisha na kuendeleza mashirikiano hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu umewezekana kwa ushirikiano kuwa mzuri miongoni mwa viongozi na Wafanyakazi wa Wizara. Kwa hiyo, ninapenda kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Mabaraza, Mashirika na Taasisi zote kwa jitihada zao za kutekeleza majukumu waliyopewa na Taifa letu. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mjini, ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa msaada na ushauri wao wa karibu kwangu. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bibi Kijakazi Rajabu Mtengwa, Wakuu wa Idara, Watendaji Wakuu wa Mabaraza, Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara, na Bodi zao ambazo zimeshirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao wametuunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wahisani wote ambao walitusaidia na nina imani wataendelea kutusaidia. Siyo rahisi kuwataja wote lakini angalau niwataje wachache ambao ni Serikali za China, *Sweden, Norway, Denmark* na *Finland*; mashirika ya kimataifa ya *UNICEF, UNESCO* na '*Right to Play'*. Pia nayashukuru mashirika na makampuni ya hapa nchini ambayo ni kampuni za simu za *Vodacom* na *TTCL*, kampuni za bia za Serengeti na *TBL* na kampuni ya vinywaji baridi za *Coca Cola* Afrika, Kanda ya Tanzania, Kampuni ya Mbunge mwenzetu Mohamed *Enterprises* na *NMB*. (*Makofi*)

Mwisho, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Vyombo vyote vya Habari nchini kwa kufanya kazi nzuri. Vyombo hivyo vya habari vimekuwa vikifanya vizuri kuitangaza nchi yetu hususan sekta za Habari, Utamaduni na Michezo. Vyombo hivi, pamoja na kufanya kazi katika mazingira magumu, vimekuwa mstari wa mbele kuitangaza nchi yetu vizuri na kwa uadilifu wa hali ya juu. Hongereni sana wanahabari wetu**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 229,311,000/= kutokana na vyanzo vyake mbalimbali. Idara zinazokusanya mapato ni Idara ya Maendeleo ya Utamaduni, Idara ya Maendeleo ya Michezo na Idara ya Habari.

Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa 2007/08 ni kama inavyoonyeshwa katika Kiambatisho I.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu imetengewa jumla ya shilingi 11,030,476,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha: Mishahara ya Wizara Shilingi 1,196,109,000/=; Mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara Shilingi 2,352,976,000/=; Matumizi Mengineyo kwa Wizara Shilingi 2,896,355,300/=; na Matumizi Mengineyo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara Shilingi 4,585,035,700/=. Muhtasari wa Makisio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa 2007/08 kwa Idara na Taasisi umeonyeshwa katika Kiambatisho II na III.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 4,991,000,000/= kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 4,821,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 170,000,000/= ni fedha za nje. Muhtasari wa Bajeti ya Maendeleo umeonyeshwa katika Kiambatisho IV.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa 2007/08, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 16,021,476,000/= ambapo kati ya hizo, shilingi 11,030,476,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 4,991,000,000/= ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii au Mwakilishi wake, Mheshimiwa Capt. John D. Komba na wakati huo huo Mwenyekiti Mheshimiwa Job Y. Ndugai atanipokea.

*(Hapa (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Fungu 96 kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia ambaye alikuwa mjumbe wa Kamati hii. Marehemu Mheshimiwa Amina alikuwa hodari wa kujenga hoja na kutetea maslahi ya jamii na taifa kwa ujumla. Katika muda wake wote marehemu alikuwa akifanya kazi zenye kutanguliza zaidi maslahi ya umma. Kifo cha Marehemu ni pigo kwa Kamati aliyokuwa akiitumikia, Bunge na taifa kwa ujumla. Tumempoteza mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa katika Kamati, ndani ya Bunge na jamii. Mungu ailaze Mahali pema roho yake, Amini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Kapt. John Komba, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu,Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan na Mheshimiwa Haroon Ali Suleiman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Juni, 2007, Kamati ilifanya kikao na Wizara jinini Dar es Salaam na kupata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, akisaidiwa na Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Mheshimiwa Waziri na Timu hii yate walitoa maelezo ya kina kuhusu: Dira na Muundo wa Wizara; Mapato na Matumizi katika kipindi cha Fedha 2006/2007; Mafanikio na changamoto katika utekelezaji. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya Maombi ya Fedha za Matumizi kwa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Wizara ilitengewa shilingi 12.9 bilioni kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 40.0 bilioni kutekeleza Miradi ya Maendeleo na hasa ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Taifa, Dar- es Salaam. Katika kuelezea utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007, Waziri alielezea kwa kina utekelezaji wa bajeti hiyo katika taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:-

Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT) ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 239 la mwaka 2002. Madhumuni ya TUT ni kutoa huduma kama chombo cha umma katika kutoa habari, kuelimisha na kujenga vituo zaidi vya kurushia matangazo kwa redio na televisheni. Kueneza usikivu, kuimarisha mitambo na kuongeza uwezo wa taasisi kufanya biashara na kujiongezea mapato. Katika mwaka 2006/2007, TUT haikutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo hivyo kushindwa kuendeleza miradi yake.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Malengo ya mwaka 2007/2008, TUT ilijipangia kumalizia ujenzi wa majengo ya Taasisi, TVT Mikocheni, kufanya ukarabati wa Ofisi za RTD, Nyerere *Road* na kujenga vituo vya Televisheni na Radio katika miji ya mikoa minane iliyobaki ya Iringa, Morogoro, Rukwa, Ruvuma, Manyara, Kilimanjaro, Singida na Shinyanga. Aidha, Taasisi ilipanga kuanzisha mkondo wa pili *(2nd Channel*) wa televisheni kwa ajili ya kitengo cha biashara na mkondo wa tatu (*3rd Channel*) wa *FM* kwa ajili ya lugha ya Kiingereza. Lakini kutokana na Serikali kutotenga fedha za maendeleo sijui TUT kama itatekeleza malengo hayo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) ilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni (*CAP* 212) ya mwaka 1961. Wamiliki wa Kampuni hii ni Serikali yenye 99% na Mhariri Mtendaji 1%. Madhumuni ya kuwa na Kampuni hii ni kutoa fursa kwa watanzania kupata habari sahihi zilizotafitiwa bila upotoshaji. Kampuni inatakiwa kujiendesha kibiashara kama yalivyo makampuni binafsi.

Katika mwaka 2006 kampuni imepata faida ya shilingi 699 milioni. Kampuni imenunua mtambo wa kuchapa magazeti wenye thamani ya shilingi bilioni 2.2 na tayari umekwishafungwa. Maktaba ya magazeti, machapisho na picha kwa njia ya elektroniki yamefanywa kwa kunakili magazeti, machapisho na picha zote tangu mwaka 1931.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya *TSN* kwa mwaka 2007/2008, ni pamoja na kupata faida ya shilingi 702 milioni, kununua jengo la uchapishaji kutoka *NSSF*, kuzindua upya magazeti ya kiingereza kwa kuyapa sura mpya, kuanzisha uchapishaji wa kibiashara wa magazeti ya wamiliki wengine na kusaidia Halmashauri za Wilaya kuanzisha magazeti na machapisho.

Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo kilianzishwa mwaka 1981 kwa madhumuni ya kutoa wakuzaji wa sanaa, wabunifu, watafiti wa sanaa, kuinua viwango vya sanaa kwa jamii na kukuza mwamko. Katika mwaka 2006/07 chuo kiliendesha mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 100, kufanya ukarabati wa majengo ya ukumbi. Aidha, chuo kipo katika mchakato wa kuwa wakala wa Serikali na kuwa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Hata hivyo, kiwango kidogo cha fedha kinachotengwa kwenye bajeti ya chuo cha Sanaa Bagamoyo hakikidhi mahitaji ya Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa Sheria Na. 27 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1983. Madhumuni yake ni kuendeleza, kustawisha na kuimarisha lugha ya Kiswahili. Kushirikiana na wachapishaji kusaidia waandishi waandike kiswahili sanifu. Kutoa huduma za tafsiri kwa mashirika, Idara, wizara, balozi na watu binafsi, kutoa huduma ya ukalimani na kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, atika mwaka 2006/2007, Baraza la Kiswahili lilipata shilingi milioni 130 kwa madhumuni ya utafutaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za BAKITA. Lakini hadi Juni, 2007 kiwanja bado kilikuwa hakijapatikana, sehemu ya fedha zimetumika kutangaza tenda za kutafuta kiwanja. Aidha, ruzuku inayotolewa kwa

Baraza bado haitoshi na Baraza linakabiliwa na upungufu mkubwa wa wanataaluma na ofisi za Baraza ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Mwaka 2007/2008 ya Baraza ni pamoja na kuandaa semina ya matumizi ya Kiswahili sanifu, kuandaa vipindi mbalimbali, semina ya mafunzo kwa wakalimani na wafasiri. Kuchapisha kitabu cha mwongozo kwa waandishi. Aidha, kusanifu istilahi katika uwanja wa diplomasia na uhusiano wa kimataifa na kuchunguza makosa yanayofanywa na vyombo vya habari na kuendelea kutafuta kiwanja na kutayarisha michoro kutegemea na upatikanaji wa kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania imeundwa kwa Sheria Na. 4 ya mwaka 1976. Madhumuni makuu ya Bodi ni kulinda utamaduni kwa kuhakikisha kuwa sanaa ya filamu na michezo ya kuigiza inazingatia maadili ya taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya utekelezaji yaliyofanyika kwa mwaka 2006/2007 ni pamoja na kukagua na kupanga madaraja ya filamu na kanda za video, kukusanya takwimu muhimu zinazohusu majumba ya filamu, maduka ya kanda za filamu, watengenezaji wa filamu, mapromota, wasambazaji na watunzi. Kuanza mchakato wa marekebisho ya Sheria na.4 ya mwaka 1976 kwa lengo la kuifanya iendane na wakati.

Aidha, Matatizo ya Bodi ni kwamba haina wajumbe wa bodi tangu mwaka 1988 na haina Katibu Mtendaji na watumishi wengine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa limeundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984 kwa lengo la kuhimiza maendeleo ya sanaa za muziki, maonyesho na sanaa za ufundi wa mikono. Kufanya utafiti wa maendeleo na uzalishaji wa kazi za sanaa, utafutaji wa masoko, kutoa huduma ya ushauri na kuunda sheria ndogo ndogo zitakazochapishwa katika jarida na kudhibiti mfumo wa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2006/2007, mambo muhimu yaliyotekelezwa ni pamoja na kuhimiza na kuhamasisha kusajiliwa kwa wasanii, ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho, kufanya utafiti wa sanaa ya sarakasi ya asili na muziki wa asili ya ngoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuandaa mpango wa utafiti na uhifadhi wa makala ya nyaraka za sanaa, kuendelea na kuhuisha sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya mwaka 1984, kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa maonyesho na kukuza stadi za usanii, uongozi na utawala wa shughuli za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Utamaduni ni asasi ya kiutamaduni inayoendesha shughuli zinazohusu utamaduni hapa nchini Tanzania. Mfuko huu ulianzishwa na Serikali mwaka 1998 kuiwezesha na kuimarisha sekta ya utamaduni kuchangia kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya uchumi wa taifa kwa kufadhili miradi na shughuli za utamaduni na kutoa tuzo kwa kazi bora. Mfuko unaongozwa na

Bodi ya Wadhamini yenye wajumbe 10. Bodi ya Wadhamini huchagua wafanyakazi wa sekretariati ya Mfuko miongoni mwa watanzania wenye sifa na uwezo. Katika mwaka 2006/2007 Mfuko wa Utamaduni Tanzania uliwezesha jumla ya vikundi 11 vya sanaa na vyama vya sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba wananchi wengi bado hawelewi maana na nafasi ya utamaduni katika maendeleo. Utamaduni ni mchanganyiko wa mambo mengi yakiwemo ya kiroho, kimwili, kifikra na kihisia ambapo huitambulisha jamii. Hii ni pamoja na mifumo ya maisha, haki za msingi za binadamu, mifumo ya maadili na imani. Kwa kutambua hili tangu mwaka 1962, Baba wa Taifa Marehemu Julius Nyerere aliunda Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana. Baada ya hapo sekta ya utamaduni iliathiriwa kwa kupigwa danadana ya kuhamishwa mara kwa mara kutoka wizara moja kwenda nyingine. Utafiti uliofanywa umeonyesha kwamba toka Wizara hiyo ilipoundwa sekta ya Utamaduni imehamishwa mara kumi na moja

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kwamba kila sekta ina uhusiano mkubwa na utamaduni, na ni vigumu kwa sekta hizo kutimiza malengo yao bila kutilia maanani suala la utamaduni. Kwa mfano sheria zinazotungwa na Bunge hazina budi kuzingatia mila na desturi za watanzania, elimu inayotolewa ni lazima izingatie mila na desturi nzuri za watanzania, hivyo hivyo kwa sekta zote. Kwa maneno mengine utamaduni ni nyenzo ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 1960 nchi ya Korea ya Kusini kimaendeleo ilikuwa karibu sawa kabisa na nchi ya Tanzania, kimapato, viwanda, kilimo, biashara, miundombinu na kadhalika. Lakini kwa kutumia utamaduni kama vile utamaduni wao wa kupenda kufanya kazi kwa bidii, kuheshimu muda, kupenda michezo, kupenda kusoma na kadhalika ndio ulioifikisha nchi ya Korea ya Kusini mahali ilipo sasa, utamaduni wao umesaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hivi sasa katika nchi yetu umezuka utamaduni wa vijana wetu kutopenda kufanya kazi hasa mashambani na vijijini, utamaduni wa kupenda utajiri wa harakaharaka, utamaduni wa kuiga mambo ya nchi zilizoendelea na kadhalika. Hili suala la utamaduni lisipotiliwa maanani nchi yetu itaendelea kubaki nyuma, Serikali lazima iliwekee mikakati katika bajeti yake suala hili. Katika suala la utamaduni, ngoma, michezo, nyimbo lazima zikemee tabia ya vijana kutopenda kufanya kazi, kuchukia rushwa, uasherati, na hii itasaidia sana kuliko hata kutunga sheria kalikali kupambana na masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Michezo la Taifa liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake katika Sheria Na 6 ya mwaka 1971. Kwa mujibu wa sheria hiyo Majukumu ya Baraza ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa, kuidhinisha mashindano ya kitaifa na kimataifa, kuamsha ari ya kupenda aina zote za michezo kwa ngazi zote. Katika utekelezaji wa shughuli za Baraza kuna changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa vitendea kazi na upungufu wa miundombinu ya michezo katika maeneo mengi, kutokuwepo kwa mkakati wa maendeleo ya michezo, ufahamu na uelewa duni wa watendaji, na ufinyu wa bajeti ya kutekeleza mipango iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Baraza, Mikakati iliyowekwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ili kupata sheria inayokidhi mahitaji, kuandaa mkakati wa maendeleo ya michezo kwa ujumla, kuendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali wa michezo, kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika michezo. Kusambaza kwenye Wilaya zote Sheria Na. 12 ya BMT na rasimu ya marekebisho hayo ili kupata maoni na kutafuta wabia wa kuchangia katika utekelezaji wa mipango ya Baraza na kutoa elimu ya kujikinga na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara imepangiwa jumla ya shilingi 11,030,476,000 kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 4,991,000,000 kwa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Kamati ilijadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2007/2008. Baada ya kujadili kwa kina utekeleza wa bajeti ya mwaka 2006/2007 na Malengo na Mipango ya mwaka 2007/2008, Kamati imetoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:

Kwa kuwa katika mwaka 2006/2007, Baraza lilipata shilingi milioni 130 kwa madhumuni ya utafutaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za BAKITA, lakini hadi Juni, 2007 bado kiwanja kilikuwa hakijapatikana, sehemu ya fedha zimetumika kutangaza tenda za kutafuta kiwanja, hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali kukamilisha haraka iwezekanavyo utafutaji wa kiwanja ili fedha zinazotolewa zitumike kwa lengo liliokusudiwa.

(b) Kamati inaweza kusaidia utafutaji wa kiwanja hicho kama ikiombwa na Wizara hiyo kufanya hivyo.

Kwa kuwa katika mwaka 2006/2007, TUT haikutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo hivyo kushindwa kuendeleza miradi yake, katika malengo yake ya mwaka 2007/2008 TUT imepanga kumalizia ujenzi wa majengo yake, TVT Mikocheni, kukarabati *Radio Tanzania Dar- es Salaam, Nyerere Road* na kujenga vituo vya Televisheni na Radio katika miji ya mikoa minane iliyobaki ya Iringa, Morogoro, Rukwa, Ruvuma, Manyara, Kilimanjaro, Singida na Shinyanga. Aidha, Taasisi pia imepanga kuanzisha mkondo wa pili (*2nd Channel*) wa televisheni kwa ajili ya kitengo cha biashara na mkondo wa tatu (*3rd Channel)* wa *FM* kwa ajili ya lugha ya Kiingereza. Hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa TUT katika mwaka wa fedha 2008/2009 kwani taasisi za TUT ni muhimu sana kwa Taifa hili.

(b) Kamati inaiomba Serikali kutafuta wabia (ambapo *NSSF* imeonyesha nia hiyo) ili kumalizia ujenzi wa jengo la TVT Mikocheni na kufanya ukarabati mkubwa wa majengo ya *RTD, Nyerere Road*, Dar- es Salaam

Kwa kuwa jumba la utamaduni ni muhimu sana katika kuendeleza utamaduni hapa nchini na kwa kuwa kiwanja sasa tayari kimepatikana, Kamati inaishauri Wizara

kuendelea na mikakati ya kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa jumba la utamaduni hapa nchini.

Kwa kuwa mchakato wa kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa tovuti ya wananchi umemalizika na mkandarasi *Infocom Technologies Ltd* ameanza kazi baada ya mkataba kuidhinishiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na kwa kuwa kuwepo kwa tovuti ya wananchi itakuwa ni hatua moja muhimu hapa nchini, Kamati inaishauri Wizara kukamilisha mkakati huo mapema ili tovuti ya wananchi iweze kufanya kazi yake na wananchi waweze kutumia tovuti hiyo kuuliza maswali mbalimbali kuhusu utendaji kazi wa Serikali yao.

Kwa kuwa Wizara hii inayo Mashirika na Taasisi mbalimbali; na kwa kuwa mashirika hayo ni muhimu sana katika kuongeza mapato na hata kutoa gawiwo Serikalini, Kamati inaishauri Wizara kuweka mikakati katika kuimarisha Mashirika na taasisi zilizoko chini ya Wizara.

Kwa kuwa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania haina Wajumbe wa Bodi toka mwaka 1988 na haina Katibu Mtendaji na watumishi wengine muhimu, Kamati inaishauri Wizara kukamilisha utaratibu ili Wajumbe wa Bodi na watumishi wengine muhimu waweze kuteuliwa mapema iwezekanavyo.

Kwa kuwa ujenzi wa Uwanja wa Taifa awamu ya kwanza umekamilika; na kwa kuwa ujenzi wa Uwanja wa Taifa awamu ya pili utakuwa na manufaa makubwa sana kwa taifa letu, ujenzi ambao unahusu uwanja wa ndani wa kisasa wenye michezo ya mpira wa kikapu, wavu, netiboli, vyumba vya mazoezi ya viungo, kumbi na hosteli ya wanamichezo wapatao 750, na kadhalika, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati ya kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ili uwanja uweze kuleta manufaa makubwa zaidi.

Kwa kuwa suala la utamaduni na michezo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi kwa maana kwamba Sekta hizi mbili zinaweza kuleta maendeleo makubwa sana kama suala la utamaduni litaeleweka kwa wananchi wengi na suala la michezo kupewa uzito wa pekee, hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali kuliwekea suala la utamaduni mikakati ya pekee ili liweze kueleweka kwa wananchi na hasa kwa kupitia sera ya utamaduni kujadiliwa kwa kina na namna ya kuitekeleza.

(b) Serikali ione umuhimu wa pekee katika kutoa fedha za kutosha katika Wizara hii hasa katika sekta ya utamaduni.

(c) Serikali ipitie upya utaratibu uliotumika kuanzisha mfuko wa Utamaduni na kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuboresha ili uweze kupata fedha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na

Michezo, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Utamaduni, Mama Sayore na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN),* Ndugu Mruma kwa kazi nzuri wanazozifanya katika maeneo yao ya kazi, tunawaomba waongeze juhudi zaidi kwa lengo la kufanikisha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizowezesha kuiongoza Kamati hii. Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Lawrence Robert Makigi, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshukuru mke wangu Mama Salome Komba, na watoto wangu kwa kunipa muda wa kutosha kushughulikia masuala ya Taifa na hasa jimbo la Mbinga Magharibi. Napenda pia nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kuniruhusu kusoma taarifa hii. Naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kapteni John Komba. Kabla sijamwita Msemaji wa Maoni ya Kambi ya Upinzani, niwaandae tu wachangiaji watakaofuatia baada ya maoni hayo ambapo mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimwa Kapteni George Mkuchika na atafuatiwa na Mheshimiwa Nyaulawa na Mheshimiwa Vulu ajiandae.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, **a**wali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa leo na kusimama mbele yenu kuchangia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 43 (5),(b),(c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Amina Chifupa. Marehemu alikuwa mstari wa mbele

katika kutetea maslahi ya vijana wa Kitanzania na Watanzania kwa ujumla. Pia alikuwa mwanamichezo na mdau mkubwa katika shughuli mbalimbali zinazohusu michezo, utamaduni na pia alikuwa mwanahabari mahiri sana, namwomba Mwenyezi Mungu ampe makazi mema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapa pole Watanzania wote waliofikwa na majanga mbalimbali kwa muda wote tuliokuwa Bungeni. Mwenyezi Mungu atawaafu. Ni jambo la busara na muhimu kwa Watanzania wote kwa ujumla kuongeza maombi katika ibada zetu ili kumwomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aweze kutuepusha na majanga mbalimbali. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti**, n**itakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakishukuru chama changu, chama cha wananchi *CUF,* na mume wangu Bwana Selemani Saidi Ally Bungara, kwa ushirikiano ninaoupata kutoka kwake katika utendaji kazi wangu. Vilevile nawashukuru viongozi wote wa *CUF* wa Wilaya ya Kilwa kwa pamoja na wanachama wote kwa ushirikiano wao mkubwa, kwani kidole kimoja hakivunji chawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, kwa kufanya kazi kwa umakini mkubwa. Naishukuru kwa kuwa imeniamini na kunipa nafasi hii, pia nawashukuru kwa ushirikiano walionipa mpaka kukamilisha hotuba hii, bila kumsahau msaidizi wangu katika Wizara hii Mheshimiwa Mohamed Ally Saidi, kwa ushirikiano wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee naomba kutoa shukrani na pongezi kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Slaa kwa imani yao kwangu kuniteua kuwa Msemaji Mkuu katika Wizara hii, pia kwa ushirikiano wao katika kutimiza wajibu wangu kama Msemaji Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, napenda nichukue fursa hii pia kuwapongeza vijana wetu wa Timu ya Taifa (*Taifa Stars*) kwa juhudi na ushindi walioupata dhidi ya timu ya Taifa ya *Burkinafaso*. Hili ni jambo la kujipongeza na kujivunia kama Watanzania, kwani nchi yetu imekuwa katika nafasi nzuri ya kuwania nafasi ya kucheza katika mashindano ya kombe la Afrika yatakayofanyika Ghana mwaka 2008. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kuchukua nafasi hii kuiombea timu yetu kila la kheri iweze kufanya vizuri katika mashindano dhidi ya Msumbiji. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatujalia tutafanikiwa. Baada ya kutoa utangulizi huo mfupi naomba sasa nianze moja kwa moja kutoa hoja ya Kambi ya Upinzani katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuangalia masuala nyeti katika wizara hii naomba kwanza kutoa kilio chetu kuwa Wizara hii pamoja na umuhimu wake katika jamii lakini haina makazi ya kueleweka. Kwa maana kwamba kila Kurugenzi/Idara zimepanga katika majengo ambayo hayaendani na hadhi husika. Mfano Idara ya

michezo, ofisi zake zinatia aibu, Baraza la Kiswahili, Idara ya Utamaduni na kadhalika zote hizo ofisi zake zipo katika majengo yaliyochakaa. Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutafuta jengo moja litakalokuwa na idara zote zilizo chini ya Wizara hii pamoja na ofisi ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ni sekta muhimu katika kujenga makuzi na maisha ya vijana, kupunguza tatizo la ajira nchini, kulitangaza Taifa letu katika sayari ya michezo kimataifa, kukuza uzalendo, kuhamasisha maendeleo na mshikamano miongoni mwa wananchi.

Tanzania ni moja ya nchi ambazo zina wanamichezo wengi na wenye vipaji mbalimbali katika nyanja tofauti za michezo, hili linaweza kuthibitika katika miaka ya sabini na themanini. Tanzania ilikuwa ni moja ya nchi ambazo zilikuwa zikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali yakiwemo mashindano ya Olimpiki na michezo ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya hivi karibuni dira ya michezo nchini kwetu imekatisha tamaa kabisa kiasi kwamba tunaonekana kana kwamba ushiriki wa Tanzania katika michezo ni kupoteza fedha za walipa kodi, na hii imetokana na kutokuwa na dira/sera nzuri ya michezo. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama sera ni nzuri basi lazima iendane na mpango mkakati mzuri wa kuitekeleza sera hiyo. Kinyume na hapo sera inabakia kuwa ni ya kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya michezo ni moja ya hamasa katika kukuza michezo katika nchi yoyote. Kambi ya Upinzani inatambua jitihada za Serikali ya Awamu ya Tatu kwa juhudi zake za kuanzisha mpango wa ujenzi wa uwanja wa michezo wenye ubora wa kisasa katika jiji la Dar es salaam. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kuwa uwanja huu utakuza hamasa kwa Watanzania kurudisha ari ya kupenda michezo na hatimae wanamichezo wetu kuona wana dhamana kwa Watanzania pindi wawapo mashindanoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huo wa kisasa umegharimu takriban fedha za kitanzania shilingi bilioni 56 mpaka kukamilika kwake. Hii inadhihirisha kwamba kama nia ingekuwapo ya miaka mingi Serikali ingefanikisha ujenzi wa kiwanja kimoja walau kila mkoa, hii inawezekana kutokana na hali hiyo. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa mapendekezo muhimu kama ifuatavyo: Kwanza, Serikali ianze kuweka utaratibu wa kujenga kiwanja kila kanda. Pili, Serikali inatakiwa kupanga fedha ya bajeti ya Wizara ya michezo, ya mwaka 2007/2008 itakayowezesha huo ujenzi wa kiwanja kimoja kila kanda. Lengo hapa liwe ni angalau tuwe na kiwanja kimoja chenye hadhi ya kimataifa kila kanda. Hii itatuwezesha kuwa na dira yenye lengo la kuandaa matamasha ya michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa Watanzania kwa uwingi wetu hatushindwi kuchangia kujenga viwanja vyetu, suala ni kuwa usimamizi na matunda ya michango inaonekana na michezo katika mikoa nchini inapewa kipaumbele kinachotakiwa na jinsi wananchi wanavyoshirikishwa katika michezo kuanzia ngazi za

chini. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama hoja hizo zitapatiwa majibu basi ujenzi wa viwanja kwa michango ya wananchi tunaamini kuwa itafanikiwa na viwanja vya kisasa vitajengwa nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungeweza kufanikisha ujenzi wa kiwanja kila kanda tungeweza kupata faida kwa kuweka kambi za kufanyia mazoezi kwa timu mbalimbali kutoka kwa jirani zetu. Ni muhimu vituo vya michezo viboreshwe na *OC* zao ziwafikie wakati unaostahili. Wizara ya fedha ipeleke fedha kwa wakati katika Wizara husika ili wizara hizo ziweze kupeleka katika idara zao zilizopo Mikoani, Wilayani, na katika Halmashauri za Wilaya, hususan vituo vya michezo, Chuo cha Michezo na Chuo cha Sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya vituo vya michezo siyo mazuri, mfano kituo cha michezo cha Songea (Ruvuma) ofisi zao hazina sehemu ya kutosha na vyoo wanavyotumia ni vilevile ambavyo vinatumiwa na watu wote ndani ya uwanja wa Majimaji. Hali hii haitoi hadhi kwa afisa michezo wa mkoa kupata motisha katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vingi hivi sasa vinamilikiwa na Chama Tawala, , karibu vyote vinazungukwa na maduka ya biashara ambayo mapato yake yote yanachukuliwa na Chama Tawala, lakini cha ajabu japokuwa mapato yanachukuliwa na chama hicho bado mazingira ni mabaya mno, hakuna mabomba ya maji, hakuna vyoo, walinzi na matatizo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kuwa japokuwa mapato kidogo yanayopatikana katika viwanja hivyo, hayatumiki katika kuendeleza michezo na badala yake yanatumika kuimarisha siasa katika maeneo husika. Kama ambavyo tumekuwa tukiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa viwanja vya michezo kuwa chini ya Wizara husika, tunarudia tena kuwa kwa kuinua ari ya Watanzania na wanamichezo, viwanja hivi vimilikiwe na Serikali na pato linalotokana na viwanja hivyo lisaidie kuinua michezo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoongea hapo mwanzo, Tanzania inarejea katika sayari ya michezo Duniani kwa kasi na hilo ni jambo la kupongezwa. Hii inadhihirishwa na ushindi uliopatikana kwa timu yetu ya Taifa (*Taifa Stars*) katika michezo yake mbalimbali na hasa ule ushindi uliopatikana dhidi ya *Burkinafaso* ushindi wa goli moja kwa bila. Kutokana na ushindi huo wa timu ya taifa, nchi yetu imekuwa katika nafasi nzuri katika takwimu ya Shirikisho la soka la kimataifa *(FIFA*) katika takwimu hizo Tanzania imepanda mpaka nafasi ya 105 kutoka nafasi ya 118 katika takwimu zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu za soka Afrika Tanzania imekuwa katika nafasi ya 28. Kwa upande wa Afrika Mashariki imekuwa nafasi ya pili ikiwa tumewapita majirani zetu wa Kenya. Kupanda huko kwa kasi kwa kiwango cha soka cha Tanzania hivi karibuni kumechangiwa na ushindi wake dhidi ya timu ya *Burkinafaso*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindi wa *Taifa Stars* umekuwa ni mojawapo ya vitu ambavyo vinaashiria Umoja na uzalendo kwa Watanzania na hii inadhirika pale ambapo Watanzania wote huwa kitu kimoja katika kuiombea na kuitakia mafanikio mema timu yetu bila kujali tofauti zilizopo katika itikadi zao za kidini, au kisias. Wadau wa michezo na Serikali kwa ujumla wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa taifa letu linaondokana na dhana nzima ya kuitwa kichwa cha mwendawazimu katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatambulika kuwa kuna mchango mkubwa sana kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza michezo kupitia Serikali ya Awamu ya Nne. Hili ni jambo la kupongezwa sana, lakini pamoja na juhudi za Mheshimiwa Rais katika kuifanya Tanzania inarudia katika kiwango chake cha soka cha miaka ya themanini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na fungu maalumu kwa ajili ya mkakati wa kuiwezesha *Taifa Stars* kwenda Ghana na pengine Afrika ya Kusini, kuliko kutegemea Kamati Maalumu ambayo inasaidia kufadhili timu. Tunaitaka Serikali isitimize dhamira ya Mheshimiwa Rais kupitia kwa wafadhili bali liwe ni jukumu la Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano yameweza kwa kiasi kikubwa kusaidia kuibua vipaji vya vijana katika mpira wa miguu nchini kwetu. Hili ni jambo muhimu sana kwani kwa nchi yoyote ile inayohitaji kuendeleza fani ya michezo huanzia kutafuta vipaji katika ngazi ya chini kwa vijana wenye umri mdogo kupitia mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulipongeza shirika la vinywaji la *coca cola* kwa kuanzisha mashindano hayo ili kuweza kupata vijana wenye vipaji na hatimae kupata timu ya Taifa. Katika mashindano hayo ili tuweze kupata kile tulichokitarajia, Kambi ya Upinzani inapenda kupendekeza mambo ya kuzingatia katika kuboresha mashindano ya soka kwa vijana kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na wadau wote wa michezo kwa ujumla:

(i) Mashindano ya soka katika ngazi yatanguliwe na ngazi ya Mikoa na Wilaya ili kuwa na mfumo unaoeleweka wa kutambua vijana wengi zaidi wenye vipaji vya soka, vyama vya soka Wilayani na Mikoani viratibu mashindano hayo.

(ii) Serikali itekeleze kikamilifu ahadi ya kurudisha mashindano hayo ya michezo mashuleni kwa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya sabini na themanini mikoa mbalimbali ndani ya Tanzania ilikuwa ikishika nafasi nzuri sana kwa kuwa na watoto wenye vipaji katika riadha. Kwa mfano, mikoa kama Kigoma, na Singida ilishika nafasi za juu kwa kuwa na watoto wanaoweza kukimbia na hivyo kushika nafasi za kitaifa, lakini hali ya sasa katika mikoa hiyo inasikitisha kwa kiasi kikubwa hasa katika mkoa wa Kigoma, hii yote ni kutokana na kutokuwa na mbinu za kuendeleza mchezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo wa riadha ni mchezo ambao unahitaji jitihada za mtu mmoja yaani mchezaji na sio mchezo wa utegemezi, hivyo basi ili mchezaji

aweze kupata ushindi anatakiwa ajitume kweli kweli kwa sababu akiharibu ameharibu mwenyewe na hakuna wa kumlaumu zaidi ya kujilaumu mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kwa mchezaji wa riadha aweze kuwa na uwezo wa kushinda anatakiwa awe amepata mafunzo ya uhakika kwa takriban miaka kumi, hivyo basi ni jambo la muhimu wachezaji hao wakapata mafunzo katika umri mdogo ili waweze kuwa na uwezo zaidi na kuweza kuliwakilisha Taifa katika mashindano mbalimbali yanayofanyika duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa mchezo huu ni kwa juhudi za mchezaji mmoja mmoja, lakini mchezaji hawezi kuwa na uwezo unaotakiwa kama hatapata visaidizi kama vile wakufunzi, vifaa vya mazoezi pamoja na viwanja vya mazoezi. Jambo la kujiuliza ni kwa nini nchi za Kenya na Ethiopia zimeweza kuwa maarufu katika mchezo huu? Kwa kuangalia karibu nchi hizo jamii ambazo zinatoa wakimbiaji maarufu na Tanzania inazo jamii hizo katika mikoa ya Singida na Arusha. Kambi ya Upinzani inadhani sasa ni muda mwafaka wa kujiuliza swali la kwa nini sio sisi? Bila ya dhana hii kuingia kuanzia kwa viongozi hadi kwa Watanzania basi wanamichezo wetu wataendelea kuitwa watalii pindi wataposhiriki mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kwamba kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imeonyesha nia ya kurudisha michezo shuleni, mchezo wa riadha utakuwa ni moja ya changamoto ya kuweza kuibua vipaji kwa watoto, kwani kwa utafiti uliofanywa mchezo huu umeonekana kupendwa na watoto walio wengi hasa katika ngazi ya Shule za Msingi, hivyo watoto hawa wanahitaji kujengewa misingi bora na imara, na jamii ikishirikiana na Serikali ili kuendeleza vipaji vya watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha hilo Serikali inaweza kuwatumia wakufunzi wa mchezo wa riadha ambao waliweza kuliwakilisha vyema Taifa na kuliletea sifa katika mchezo huu miaka iliyopita, kuwafundisha na kuwapatia mbinu za mchezo huu kuliko kuacha vipaji vya maveterani hao katika riadha kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha ile mikoa au wilaya zisizo na shule maalumu kwa watoto walemavu, wenye mtindio wa ubongo na kadhalika na wao wanapata fursa za kushiriki michezo ya Olimpiki maalumu ambayo hufanyika kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ni ukweli usiopingika kuwa maeneo mengi ya wazi ambayo lengo lake hasa ni kwa ajili ya watoto kuchezea, kwa sasa umezuka mtindo wa Serikali kupitia CCM kuhodhi maeneo hayo ya wazi kwa kujenga majengo ya biashara, vilevile maeneo mengine kuyafanya sehemu za kuegesha au kulaza magari huku wakichukua ushuru na kodi ya pango. Mtindo huu umekuwa sugu hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hii siyo haki, na Kambi ya Upinzani itaendelea kuyaongelea upungufu huu wa CCM kupora maeneo haya ya wazi ambayo ni msingi

mzuri kwa watoto wetu kuanza kushiriki katika michezo. Hivyo basi tunaitaka Wizara husika suala hili la viwanja vya wazi kulingalia kwa makini na kulitolea kauli.

. Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya habari ni moja ya sekta muhimu sana katika huduma za jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya kila raia kama invyotamkwa kwenye Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 18, ambayo inasema: "Mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; anayo haki ya kutafuta, kupokea, na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi; anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inategemewa sana katika kufikisha habari za matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii. Kwa kiasi kikubwa taarifa zinazotolewa na vyombo hivi zinatakiwa kuwa za uhakika ili zisiweze kuwapotosha wananchi wanaopokea habari hizo. Hivyo basi ili jambo liweze kufanikiwa ni muhimu waandishi hao kupata ushirikiano kutoka kwa viongozi na kutoka katika jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyojulikana waandishi wa habari wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kuiarifu jamii juu ya mazuri na mabaya yanayotokea katika jamii, ila inakuwa vigumu kwao kutoa mabaya yanayowasibu katika kazi zao, na hii ni kutokana na wenye vyombo vya habari na wahariri kutokuwa tayari kuandika malalamiko ya waandishi ambao hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sisi Wabunge ni wawakilishi wa matatizo na kero za wananchi wetu kama ilivyo kazi ya uandishi basi nina sababu zote za kulifikisha suala hili mbele ya Bunge lako Tukufu ili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya waandishi wa habari hawana ajira za kudumu, nao wanakadiriwa kufikia asilimia 70 na huwa wanalipwa kulingana na habari walizoziandika na asilimia 30 tu ya waandishi ndio wenye ajira za kudumu (walioajiriwa). Kuwepo kwa idadi kubwa ya waandishi ambao hawana ajira ya kudumu kunatokana na wamiliki wa vyombo vya habari kukwepa majukumu ya msingi ya waandishi kama wafanya kazi na pia kunatokana na kuiona taaluma hii kama sio taaluma rasmi kama zilivyo taaluma nyingine.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 55 fasili ya (1). Mchangiaji anayeendelea sasa hivi kuzungumza amesema kwamba CCM inapora maeneo kwa ajili ya manufaa yake.

Kauli hii kwa wananchi wanaotusikiliza Mwenyekiti ni kauli nzito na mimi ninaomba Mbunge kwa kutumia Kanuni ya 50 fasili ya (1) athibitishe hayo anayoyasema kama kweli CCM imepora maeneo kwa ajili ya manufaa yake, ahsante.(*Makofi*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa sababu anataka nitoe, nitatoa lakini ukweli ndiyo huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanawetu, labda ukae kidogo. Kilichozungumzwa hapa na Mheshimiwa Zambi ni Kanuni ya 50 (1) inayosema: "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni…" na ulichokiongea ni jambo lipo kwenye Hotuba yako kwamba CCM inapora maeneo. Mheshimiwa Zambi anataka ama utoe ushahidi wa hilo au uliondoe kama huna ushahidi katika maelezo yako. Kwa hiyo, kati ya hayo mawili fanya mojawapo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naliondoa.

**MWENYEKITI:** Unaweza kuendelea.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaniongezea muda wangu kwa sababu nimeshafika katikati. Malipo ya waandishi wengi yanasikitisha sana na suala hili linashindwa kujulikana kwa wananchi kwa kuwa wahusika hawana njia mbadala ya kupitishia machungu yao zaidi ya vyombo wanavyofanyia kazi. Na kwa kawaida mtu huwezi kujisemea mwenyewe mpaka mwingine akusemee. Je, ni chombo gani kinaeleza matatizo ya ajira kwa waandishi wa habari? Mfano, wale ambao hawakuajiriwa wanapokea kati ya shilingi 1000/- na shilingi 10,000/= kwa habari moja kulingana na kuwa habari hiyo imechapwa ukurasa gani katika gazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa viwango hivyo vya ujira na kwa asilimia kubwa iliyopo ya waandishi ambao hawana ajira ya kudumu katika vyombo vya habari (hawana mkataba wowote wa kazi), ni kweli maadili ya taaluma hiyo yatakuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na sekta ya habari kuweka utaratibu utakaokuwa unatumiwa na wamiliki wa vyombo vya habari katika kuhakikisha maslahi ya waandishi yanalingana na taaluma yenyewe, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa litaondoa malalamiko ya waandishi kupokea rushwa na wengine kudhalilishwa na watoa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa kutokana na hali kama hiyo harakati za kupambana na rushwa hazitafanikiwa kwani waandishi walio wengi watashindwa kuripoti matukio yanayohusu rushwa kwani nao ili kuishi wanategemea kupewa rushwa

ili habari itoke kwa matakwa ya mtoaji habari yenyewe na sio kwa mtazamo wa mwandishi na mazingira husika ya habari yenyewe. Hivyo nao watakuwa ni sehemu ya rushwa. Rushwa ni kwa mtoaji na mpokeaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mpya wa TVT, Ndugu Danstun Tido Mhando kwa kazi yake anayoifanya na kuifanya TVT kwa kipindi kifupi alichofika kuwa na vipindi vingi vinavyopendwa na watanzania wengi. Tunampongeza kwa ubunifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kituo hicho cha televissheni ya Taifa kuna majengo ambayo yamekuwepo bila kukamilika kwa kipindi kirefu sana. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga fungu maalumu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo hayo ili kituo hicho kiwe na hadhi ya kubeba dhana ya kuitwa Televisheni ya Taifa na vilevile kuwa kama motisha kwa watendaji wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, majengo ya *Radio* Tanzania yaliyo barabara ya Nyerere nayo kwa kweli yanatia aibu kubwa kwani ni muda mrefu tangu yafanyiwe ukarabati. Msimu wa mvua huwa na hatari sana kutokana na nyaya za umeme na nyingine za mawasiliano kutokuwa katika mpangilio unaoeleweka. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa ujumla itenge fedha kwa ajili ya ukarabati wa jumla kwa kituo hicho cha Radio Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa lolote liweze kuheshimika, ni lazima liwe na utamaduni wake unaoendana na mila na desturi zake za asili katika masuala mbalimbali yanayolihusu na tamaduni hizo haziwezi kuathirika kwa kuingia kwa tamaduni za kigeni. Idara ya maendeleo ya utamaduni kazi yake ni kukuza, kuendeleza, na kueneza utamaduni kwa ujumla wake, haya yanapatikana katika nyanja mbalimbali kama vile ndani yake utakuta: Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA); Bodi ya ukaguzi wa filamu na michezo ya kuigiza; Baraza la Sanaa la Taifa; Mfuko wa utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni uendane na mila na desturi zetu. Hivi sasa kumekuwa na tabia ya kuiga utamaduni wa Magharibi hasa katika mavazi. Mfano mzuri ni pale yanapofanyika mashindano ya kumtafuta mrembo wa wilaya au kitongoji fulani. Sio kila utamaduni wa Magharibi ni mzuri na unapaswa kuigwa, bali tuwe waangalifu katika kuiga tamaduni ambazo hazina athari kwa tamaduni zetu za asili. Kambi ya Upinzani inahoji, hivi vigezo vya mtu kuitwa mrembo wa Taifa ni nani hasa anaviweka? Na je, vinaendana na mila, desturi na tamaduni zetu? Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kuhusiana na jambo hili.

Tanzania ni mwalimu wa Kiswahili, hivyo basi tunategemea Kiswahili fasaha kizungumzwe katika nchi hii na si vinginevyo. Kumezuka tabia ya kubadili maneno ya Kiswahili fasaha na kuweka katika maneno yasiyohusika. Kwa mfano, neno *shoga* ni neno linalotumika kwa marafiki wawili wa jinsi ya kike ambao ni marafiki walioshibana. Neno hili hutumika kama si urafiki tu bali ni kama ndugu wa kuzaliwa. Lakini hivi sasa neno *shoga* au *mashoga* hutumika kwa wanaume wanaokuwa wanajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na wanaume wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanaume hawa wenye uhusiano wa kimapenzi wasiitwe kama vile wanavyostahili kuitwa? Wanaonewa aibu au ndiyo njia ya kupotosha Kiswahili fasaha. Mfano mzuri upo hapa hapa Bungeni tunapoongelea neno *kukazana*, hutafsriwa tofauti na maana halisi ya neno lenyewe. Huu ni upotoshoshaji wa lugha ya Kiswahili. Katika kuzungumzia suala zima la Kiswahili katika nafasi 200 za walimu kwenda kufundisha Kiswahili nje ya nchi, Kambi ya Upinzani ingependa kujua ni Watanzania wangapi wamefanikiwa kwenda kufundisha Kiswahili nje?(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri, Serikali kuliangalia Baraza la Kiswahili na kuliwezesha ili liweze kufanya kazi zake ipasavyo za kukiendeleza Kiswahili fasaha katika nchi yetu. Baraza hili kama linavyojieleza katika Hotuba zilizotangulia, limeundwa kwa sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1984 ili liweze kuhimiza maendeleo ya sanaa na muziki, maonesho na sanaa za ufundi wa mikono. Eneo hili ukiliangalia tu utafahamu kuwa asilimia kubwa ya wahusika ni wananchi au watu wa aina gani, katika eneo hili utakuta vijana, wanawake wanaotafuta maisha katika kujiajiri katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inaishauri Serikali kuwa makini kuongeza bajeti ili huduma ziweze kuwafikia wajasiriamali hawa, kwani eneo hili ndilo hasa mfuko wa utamaduni hutumika kwa kiasi kikubwa ili kuinua kiwango cha maisha ya wasanii hawa katika sekta mbalimbali.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa Wizara na Serikali kwa kuweza kufikia asilimia 60 ya ujenzi wa ukumbi wa wazi wa maonyesho *(open air theatre)* pia BASATA linawakaribisha wananchi wote kupeleka vijana wao ili wakapate mafunzo ya sanaa, uongozi bora kwa wasanii binafsi wa vikundi na vyama vya sanaa yanayoendeshwa na BASATA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1998 na Serikali, ni mojawapo ya asasi iliyoanzishwa ili kuimarisha na kuwezesha sekta ya utamaduni, kuchangia kufanya shughuli za utamaduni zenye kuchochea ubunifu wa bidhaa bora na huduma ili kuongeza pato la jamii na kuhimiza ajira binafsi. Mfuko huu pia hufadhili miradi na shughuli za utamaduni na kutoa tuzo kwa kazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nyingi za mfuko huu, bado una matatizo mengi ya kifedha hivi sasa, kwani kihistoria mfuko huu ilikuwa na wafadhili maalumu. Kwa ufupi mashirika ya kitaifa yaliyokuwa mstari wa mbele kufadhili mfuko huu ni shirika la maendeleo la *Sweden* (*SIDA*), *Norway* (*NORADI*), na *Denmark* (*DANIDA*). Mfuko huu kwa sasa wafadhili wamejitoa, na sio kwa kuwa wanaohudumia ni wabadhirifu wa fedha bali ni kwa sababu mtoto akizaliwa hubebwa kwa kuwa hajaweza kujitegemea lakini anapokuwa na kujua jinsi gani ya kujilinda yeye mwenyewe inabidi asibebwe tena, bali ajibebe mwenyewe. Mheshimiwa Mwenyekiti, mzigo huu wa mfuko wa utamaduni ulikuwa ubebwe na serikali lakini ukasaidiwa na wafadhili ambao nimewataja na hivi sasa kama nilivyosema wafadhili hao wamejitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2006/2007 Idara/Taasisi ilitengewa fedha na kati ya hizo sh: millioni 96, ambazo katika harakati za kipindi cha matatizo ya njaa zilichukuliwa katika kuokoa janga hilo. Na mwaka huu wametengewa shilingi millioni 200, hii si haba. Kambi ya Upinzani bado inatilia msisitizo wa Serikali kuiongezea fedha wizara ili iweze kujikimu na matatizo yanayoikabili na kufanikisha yale yote iliyokusudia katika kuendeleza mfuko wa utamaduni. Tunaiomba Serikali fedha hizo zibaki kama zilivyo katika mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ya filamu na michezo ya kuigiza ndiyo iliyounda Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ili kulinda utamaduni kwa kuhakikisha kwamba sanaa ya filamu na michezo ya kuigiza inazingatia maadili ya Taifa. Hii ni sekta ambayo huweza kuwavutia wananchi wengi na ina uwezo mkubwa katika kuelimisha au kupotosha jamii. Hivyo basi Kambi ya Upinzani tunashauri waigizaji wawe makini kuona kwamba filamu zinazoigizwa na zile zinazotengenezwa zinakuwa na maadili ambayo hayaharibu tamaduni zetu na jamii kwa ujumla. Pia bodi hiyo isimamie katika kulinda na kutetea haki za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zilizoendelea wasanii ni matajiri sana na huyamudu maisha yao bila matatizo. Tunaiomba serikali iwapatie elimu wasanii ili waweze kutenda kazi zao kwa ufasaha na kuweza pia kujua haki zao za msingi kwa kile wanachokibuni na kujitetea pale haki zao zinapohujumiwa na wajanja kwa kutumia jina la promota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi na majukumu makubwa ya Wizara hii fedha zilizotengwa kwa mwaka shilingi 16,021,476,000/- kwa kweli ni kidogo mno kulingana na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Mnyaa!

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Kanuni ya ngapi?

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirejea Kanuni ya 50, Mbunge akithibitika kusema uongo Kanuni hii mwishoni inaeleza hivi: “Mbunge yeyote aliyetakiwa kufanya hivyo atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili hiyo.” Sasa nataka kujua ule muda wa kuthibitishwa aliopewa Mheshimiwa Zarafi aliokuwa akitoa maelezo ilikuwa ni pale pale au anaweza kupewa muda baadae kuthibitisha usemi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa aliyepaswa kuomba muda ni yeye mwenyewe, kusema uthibitisho ninao, nitauweka mezani wakati fulani. Nipe muda na angepangiwa huo muda. Vinginevyo kama ametereza ulimi, anafanya kama alivyofanya kwa kurekebisha jambo ambalo alikuwa ameliweka kwa kusema isivyo kuwa kweli. Tunaendelea kwa sababu muda wetu ni mdogo na wachangiaji ni wengi sana kama nilivyosema mwanzo tunaanza na Mheshimiwa George Mkuchika, anayefuata ni Mheshimiwa Richard Nyaulawa ajiandae.

**MHE CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kukushuruku kunipa nafasi kusema kuchangia Wizara hii. Kabla sijasema nataka nitangulize kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri kwa Kiswahili chake kizuri na sisi tutajitahidi kuzungumza kama yeye na natumia pia nafasi hii kuipongeza Serikali jinsi inavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika Wizara hii. Tumepata gazeti la Serikali, tumepata mafanikio katika uwanja wa michezo wa kisasa ambao unakamilika na Serikali imetuletea walimu wa michezo wa mpira miguu. Timu yetu ya Taifa inafanya vizuri na pia nataka niwapongeze vijana wa *Taifa Stars* kwa kazi nzuri waliyoifanya na sisi Mtwara tuko tuna fahari kwamba kwamba ndani ya Taifa *Stars* tuna mtoto wetu Nizar Khalfan. Goli lile nadhani mnalikumbuka ambalo Nizar alilifunga likatusogeza mbele. Kwa hiyo, napenda kupongeza sana.(*Makofi*)

Baada ya kusema hayo nataka nichangie kwanza kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Taasisi ya Utangazaji. Kwa kweli sisi tuliopo vijijini tunategemea sana redio kujua kinachoendelea katika nchi yetu na wale wanaoona TV kule inakowezekana. Nashukuru kwamba wanatambua kwamba Televisheni ya Taifa inafanya vizuri. Nataka nitumie nafasi hii kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuiruhusu TUT kujiingiza katika biashara. Mimi nimesoma katika Magazeti nikashangaa. Tumewaruhusu watu kujenga shule za binafsi lakini hatuwapangii karo. Tulipowaruhusu kujenga shule za binafsi hamjatuambia tufunge shule za Serikali.

Sasa leo Taasisi ya Utangazaji imepata zabuni ya kuwatangazia Watanzania ligi ya Uingereza imekuwa nongwa! Mimi naunga mkono kwa sababu gani? Bajeti ya Taasisi ya Utangazaji mwaka huu imepungua kwa shilingi bilioni 2. Lakini ni jambo la kawaida katika nchi zinazoendela vyombo hivi vya habari vya Serikali kuingia katika ushindani. Kenya *Broadcasting Cooperation* wanafanya, Afrika Kusini wanafanya. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba uamuzi uliochukuliwa na Serikali kuruhusu Taasisi ya Utangazaji kuingia katika Ushindani na vyombo vingine ni uamuzi sahihi, tunauunga mkono na ni mategemeo ya nchi hii kwamba vyombo vya Taasisi ya Utangazaji vinatakiwa viwe bora na madhubuti kuliko vingine vyovyote katika nchi hii. (*Makofi*)

Baada ya kusema hilo, nataka kuzungumza juu ya usikivu wa Redio Tanzania na kuonekana kwa Televisheni ya Taifa katika Jimbo langu la Uchaguzi Newala na Mtwara. Niliuliza swali hapa, kwamba Serikali itachukua hatua gani kuona kama Redio Tanzania inasikika nyakati zote. Katika Jimbo langu la Uchaguzi Redio Tanzania inasikika vizuri sana usiku. Lakini asubuhi utaanza vizuri na majira, lakini sidhani kama utamaliza. Inapofika taarifa ya habari tayari sauti imepotea na vijijini kule wengi tunapenda kusikiliza kipindi kile cha magazetini leo. Maana unayajua mambo yaliyoandikwa katika

magazeti, hatusikii. Kuna masomo ya kwenye redio ambayo vijana wa shule za msingi wanayapata kupitia *redio* hawayasikii, tunawanyima nafasi watoto wetu kusoma kama wanavyosoma watoto katika mikoa mingine. Namwomba Mheshimiwa Waziri na wala sina mpango wa kuzuia mshahara wake, lakini atakapozungumza jioni atueleze tatizo ni nini? Nachingwea kuna *Booster Station* si mbali na Newala, Lindi kuna *Booster Station* si mbali na Newala, kwa nini Radio Tanzania haisikiki Newala, haisikiki Mtwara saa zot? Saa nne yanapotokea matukio ya kitaifa ambapo zamani ulikuwa unasikia tunakupelekeni uwanja wa Taifa kusikiliza sherehe za Uhuru na Jamhuri, hatusikii! Lakini zamani tulikuwa tunasikia, kama kuna mushkeri umeingia basi tunaomba marekebisho yafanyike ili sisi wakazi wa Newala tupate kusikia.

Kwa upande wa Televisheni ya Taifa hali kadhalika nilieleza kwamba kule Newala hatuwezi kuona mpaka watu wameweka ungo. Sasa walio na uwezo wa kuweka ni wachache, tunaomba Serikali iangalie hio. Kwa sababu ndani ya Ilani tumesema hivi, "kueneza *RTD* na *TVT* nchi nzima kwa kuwa hewani kwa saa 24." Saa 24 ambazo hazisikiki ni sawa sawa hazipo. Kwa hiyo, tunaomba suala la usikivu mlitilie mkazo, Serikali ichukue hatua kuhakikisha kwamba RTD na TVT zinasikika na kuonekana vizuri kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa lugha ya Kiswahili, nataka nichukue nafasi hii kuupongeza Umoja wa Afrika kwa kukubali Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Umoja huo. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama walivyoeleza wenzangu Tanzania ndiyo Mwalimu wa Kiswahili. Tutumie fursa hii kufundisha Kiswahili katika nchi zinazotuzunguka. Tujitahidi kusema na kuandika Kiswahili fasaha na Kiswahili sanifu. Tusipotoshe maneno. Yapo maneno tumeazima katika lugha zingine. "Baiskeli", "skauti", "saa", sasa yale tuliyoyaazima *rule* yake ni hiyo hiyo tu. Husemi masaa 24 ni saa 24, baiskeli 200 husemi mabaskeli 200, Skauti 500, husemi maskauti 500. Sasa tunaomba na vyombo vya habari mtusaidie kuwa na watu wanaitwa *Language Supervisor*. Wakati mimi nasoma *University* nilikuwa nafanya *temporary employment* Radio Tanzania. Ubora wa Kiswahili cha Radio Tanzania ukoje? Mzee Karume alikuwa anasikia Kiswahili, akaona hakiko sawa sawa, alimleta *Language Supervisor* pale *News Room,* Mzee Jongo, nilifanya naye kazi. Mkishatafsiri, mnampa yeye anapitia kabla hakijaenda hewani, wanahakikisha kinatoka Kiswahili sahihi. Tunaomba vyombo vingine vya Habari waige mfano huu. Muwe na *Language Supervisors* ambao watahakikisha kwamba magazeti yanayotoka yanatoka katika lugha nzuri na kama ni taarifa za habari ziwe zinatoka vizuri. Katika fasihi *(literature)* kuna kitu wanaita *code switch*. *Code switching* yaani unahama kwenye lugha hii unazungumza Kiswahili lakini unapachika maneno mengi ya Kiingereza yaani uonekane kama wewe umekwenda shule basi kuchanganya changanya lugha! Unajua nakwenda kumwona *friend* wangu fulani ananisubiri hapo nje. Badala ya kusema nakwenda kumwona rafiki yangu ananisubiri hapa nje. Mnatuharibia lugha! Kwa hiyo, tunaomba vyombo vya habari wahakikishe wanakuwa na *Language Supervisors* na watangazaji na nyinyi mhakikishe pia mnatangaza lugha yetu vizuri. Kwa sababu tukiharibu sisi tunaiharibu na lugha. Ukienda Uingereza wanasema Kiingereza kinachozungumzwa *London Square* ndiyo Kiingereza sanifu. Sasa katika *East Africa* Kiswahili kinachozungumzwa Tanzania ndiyo Kiswahili kizuri, tukiharibu sisi tutawaharibu na wanafunzi wanaokuja, Rwanda, Burundi,

Msumbiji na wapi.Sasa nataka nizungumze kuhusu vyombo vya habari. Nataka niipongeze Serikali kutoa uhuru kwa vyombo vya habari na utendaji wao. Lakini mimi nasikitika sana kama kuna fani imevamiwa na watu ni fani ya uandishi wa habari; na tumeiharibu hii fani wakati tuliopo…..! Sasa nilikuwa nakemea lile lile, nilitaka kusema tulipo- *liberalize. (Kicheko)*

Tuliporuhusu watu kuwa na vyombo vya habari binafsi mara vilipoanza, kila mmoja anayejua kuandika akaenda kuandika habari. Sasa mimi naomba fani hii lazima tuirekebishe, Wizara lazima iweke kiwango cha taaluma cha uandishi wa habari ambacho mwandishi wa habari anatakiwa kuwa nacho kabla hajaitwa mwandishi wa habari. Vilevile kama ilivyo mwalimu, huwezi kuwa mwalimu bila kuwa na *certificate in education*. Sasa uandishi wa habari ulivyo hivi sasa, utakuta karibu kila siku magazeti yetu yanaishia kuomba radhi, kwa wanaenda Waandishi wa Habari katika Mkutano mmoja lakini wakitoka pale kila mmoja anakwenda kuandika tofauti utafikiri wametoka katika mikutano tofauti. Kesho yake wanaishia kuomba radhi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atumie nafasi yake kurekebisha dosari hii. Pia yapo magazeti ambayo yanapotosha maadili. Magazeti hayo yanatumia lugha chafu, picha chafu za ngono. Mheshimiwa Waziri mimi nafahamu anaouwezo wa kuyafungia magazeti yanayodhalilisha utamaduni wa nchi hii. Yale magazeti machafu machafu wanaweka picha ya mtu wanamfunga tu uso lakini huku chini wamemwonyesha kama alivyo. Huyo Msajili wa Magazeti haya anafanya nini? Funga magazeti haya ya matusi, Tanzania ni nchi ya wastaarabu sio nchi ya wahuni. Mnawaharibu watoto wetu kwa kuwaonyesha magazeti ambayo yana picha na lugha chafu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atekeleze Ilani. Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM tumesema kwamba tutaimarisha mafunzo ya Uandishi wa Habari yanayotolewa na Wizara ya Habari. Kuhusu michezo, nimepongeza pale mwanzoni kwenye Ilani ya Uchaguzi wa CCM inasema hivi, "kuvitambua, kuvikuza na kuviandaa vipaji vya wanamichezo na wasanii kwa kuunda timu za michezo, za sanaa za aina mbalimbali katika ngazi ya vijiji, wilaya, kata hadi taifa. Mheshimiwa Waziri hili halifanyiki. Lazima Wizara iweke utaratibu nchi nzima, tuwe na ratiba ya michezo. Miezi fulani mashindano kwenye kijiji, miezi fulani tunatafuta Bingwa wa Kata, mwezi fulani Tarafa, mwezi fulani Wilaya hadi nchi nzima. Watu wawe wanacheza sio tu kila siku Taifa *Stars*. Tunataka na Newala *Stars,* Tandahimba *Stars.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba Sekretarieti za Mikoa hazina Afisa Utamaduni wala Afisa Michezo. Hawa ndio wanaomshauri Mkuu wa Mkoa. Ninaomba Serikali ichukue hatua kuhakikisha katika Sekretarieti za Mikoa wanakuwepo Maafisa Uatamaduni wa Mikoa watakaoratibu shughuli za Utamaduni na wawepo Maafisa Michezo wa Mikoa wakaoratibu shughuli za michezo ndani ya Mkoa na kumshauri Mkuu wa Mkoa ipasavyo. Hapa juzi kuna Mkoa wameulizwa mbona hujaleta timu? Nina uhakika pengine Mkuu wa Mkoa yule hakuwa na taarifa. Lakini angekuwa na Afisa Michezo pale ndiyo alikuwa wa kumuuliza timu umeiandaa vipi? Kwa hiyo, nataka nimalizie kuitaka Serikali haraka sana rudisheni michezo ya UMISETA na UMISHUMTA. Wachezaji wazuri wa nchi hii walipatikana huko. Sielewi ni kitu gani kilisababisha? Wakati wa kucheza upo, ratiba ipo naomba michezo kwa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari irudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mnajua Mbunge wa Newala mstaarabu hapendi kupigiwa kengere mara ya pili. Naomba nikushukuru sana kunipa nafasi hii. Nasema naunga mkono hoja ya Ndugu yangu, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Kabla ya kuanza kuchangia, ninataka kueleza wazi kwamba, mimi ni mhusika katika vyombo vya habari, ni mmiliki mojawapo wa vyombo vya habari. Kwa hiyo, ninataka kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa hotuba nzuri aliyoitoa na kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii. *(Makofi)*

Lakini vile vile, ninataka kuipongeza Serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kuendesha biashara ya vyombo vya habari. Kuna uhuru mkubwa ingawa kuna matatizo hapa na pale. Lakini kutokana na uhuru huo, kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika hotuba yake, kuna Magazeti mengi ambayo yameanzishwa, kuna Redio nyingi zilizoanzishwa, kuna Televisheni nyingi zilizoanzishwa. Inawezekana kabisa kwamba, kwa upande wa Vyombo vya Habari ambavyo kwa Tanzania mwaka 1993 ndipo tulipoanza kupewa uhuru huo, katika kipindi hiki kifupi tumeweza kujenga Vyombo vya Habari vingi sana na inawezekana kwamba ni vingi zaidi kuliko sehemu yoyote ya Afrika Kusini mwa Sahara. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuweka mazingira hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira hayo hayo, ajira ya moja kwa moja ya waandishi inaweza kufikia kama 2,500. Vilevile kuna ajira za mikataba ambazo zinaitwa *correspondents*, hizo zinaweza kufika kwenye 3,000. Pia kuna watu ambao wanauza magazeti, ambao wametapakaa nchi nzima, hao wanaweza kuzidi zaidi ya watu 4,000. Kwa maana hiyo, ni kwamba, Vyombo vya Habari vina mchango mkubwa sana katika kuongeza ajira katika nchi hii na yote haya yamewezekana kwa sababu ya kuwa na mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kutoa pongezi kubwa sana kwa kazi nzuri ambayo Vyombo vya Habari, vinafanya kwa kutoa habari na kuwaelimisha wananchi kwa kiasi kikubwa sana. Lakini, vile vile ningetaka kusema kwamba, katika hizi shughuli za Vyombo vya Habari kwa wakati huu, kuna ushindani mkubwa sana.

Kuna ushindani baina ya Vyombo Binafsi vya Habari na upinzani huo tunaukubali na ni mzuri kwa maana ya kwamba, kila chombo cha habari kinajitahidi sana ili kiweze kuwa kinatoa habari ambazo ni sahihi, nzuri na kamilifu kwa wananchi. Kwa hiyo, ushindani ni mzuri baina ya vyombo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ushindani wa kibiashara baina ya vyombo binafsi na vyombo vya Serikali. Sasa katika eneo hilo, ninafikiria kwamba, ushindani huu wa pili baina ya vyombo binafsi na vyombo vya Serikali si sahihi na ni kinyume cha Sheria ya *Fair Trade*. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu biashara kubwa ya Vyombo vya Habari inatokana na matangazo na sehemu kubwa ya matangazo

yanatoka Serikalini. Kwa hiyo, matangazo yanayotoka Serikalini kama Serikali ikiwa na vyombo vyake, maana yake ni kwamba, matangazo mengi yanakwenda kwenye vyombo vya Serikali na matangazo machache yatakwenda kwenye vyombo binafsi. Sasa hapo panaanza kuwa na uwanja ambao unapishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema vilevile si sahihi? Nasema si sahihi kwa sababu vyombo binafsi baada ya kupata biashara vikiwa vimepata faida, vinalipa kodi. Kodi ambayo inapatikana na kupelekwa Serikalini, hutumika kutoa kama ruzuku kwenye vyombo vya habari vya Serikali. Kwa hiyo, mfanyabishara binafsi anatoa kodi, kodi hiyo inatumika kutoa ruzuku kwenye chombo cha Serikali na hicho chombo cha Serikali kinatumika katika kuinua biashara ya yule anayetoa kodi. Sasa hapo napata matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, kwa maana hiyo ni kwamba, vyombo vya habari binafsi vinalazimika kujikaanga kwa mafuta yake yenyewe, kwa maana ya kwamba, vinatoa kodi, halafu ile kodi inatumika na vyombo vya habari vya Serikali katika kufanya ushindani na labda hata kuviua kibiashara na kuvifanya vyombo binafsi visiweze kufanya kazi hiyo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya vyombo binafsi siyo makubwa sana, lakini bado vina mchango mkubwa katika nchi hii katika kutoa kodi, lakini vile vile katika kuongeza ajira. Kama vyombo hivi binafsi vitakufa, tujue kabisa kwamba, hata ajira zitapungua kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo, katika suala hilo, ningetaka kusema kuwa, uwanja wa ushindani baina ya vyombo vya Serikali na vyombo binafsi, siyo sawa sawa. kwa sababu vyombo vya Serikali baada ya kupata hizo ruzuku, mara nyingi hutumia hizo hela kuingia katika mikataba ambayo ni aghali zaidi, kuliko gharama ambazo vyombo binafsi vingeweza kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini hapa mwenzangu alikuwa akieleza kuhusu labda chombo cha Serikali kilipokuwa kimenunua ruhusa ya kuweza kutangaza mchezo wa mpira. Vyombo binafsi vilikuwa vimetaka kununua ile michezo kwa shilingi milioni 70, lakini chombo cha Serikali kilinunua kwa shilingi milioni 200, hela za walipa kodi, ambazo zingetumika kwa ajili ya mambo mengine. Kwa sababu katika eneo la biashara, natumaini vyombo vya habari binafsi vina nafasi nzuri kabisa ya kuweza kufanya kazi hiyo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, kazi ya TUT ni nzuri na ningetaka kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kutaka kukiimarisha chombo hiki. Lakini pamoja na hayo, nilikuwa nafikiria kwamba, tungejaribu kuangalia sisi ambao tuko katika vyombo vya habari binafsi na vyombo vya Serikali, tunaweza kushirikiana namna gani ili kuweza kuifanya kazi hii sawa sawa. Kuna maeneo ambayo vyombo vya habari binafsi vinaweza kufanya kazi vizuri zaidi, nayo ni kufanya biashara. Lakini kuna maeneo ambayo ni ya maendeleo, vyombo binafsi vinafanya kwa udhaifu mkubwa sana. Vyombo vya Serikali vina nafasi kubwa zaidi kufanya kazi hizo za maendeleo kuliko za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali ni kujenga mazingira mazuri kuiwezesha sekta binafsi kufanya kazi vizuri. Kazi ya Serikali ni kufungua masoko, kazi

ya Serikali siyo kufanya biashara, ndiyo mwongozo wetu. Tunasema Serikali haingii katika kufanya biashara, kazi yake kubwa ni kujenga mazingira mazuri ya kuiwezesha sekta binafsi, kufanya kazi sawa sawa ili iweze kutoa mchango mzuri ndani ya Serikali katika kulipa kodi, katika ajira na vitu vingine. Kwa hiyo, tunapofanya ushindani huo, hatufanyi kazi ambayo ni sahihi.

Kwa hiyo, kwa ushauri wangu, katika hali ya kutaka kushirikiana, nilikuwa nafikiria kwamba, uwezo wa Serikali ambao ni mkubwa sana ungeweza kutumika katika kufanya kazi nyingine tofauti katika jamii yetu. Wananchi wengi wanaokaa vijijini, hawapati habari ya aina yoyote na wanataka, wana kiu ya habari hizo. Lakini ni nani atakayepeleka habari hizo kijijini? Vyombo binafsi haviwezi kupeleka habari hizo vijijini, kwa sababu hakuna maslahi ya kibiashara. Lakini Serikali ambayo inahusika na suala la maendeleo, kazi yake ni kujaribu kuamsha na kutoa tarifa kwa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kama tungefika mahali ambapo Serikali inafanya kazi ya aina fulani ambayo ni tofauti na vyombo vya biashara, basi jamii nzima, Tanzania nzima tungekuwa tunaweza kupata habari ambazo zinahitajika na watu wote kwa ujumla wetu. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kuwe na *specialization*. Vyombo vya Serikali vifanye kazi ya kutoa habari kuhusu sera, kwa sababu kuna mambo mengi sana, tunazungumzia kuhusu sera za kila aina. Lakini ni wananchi wangapi wanaozielewa; kweli wananchi wa vijijini wanazielewa hizo sera au zinaishia hapa hapa mjini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyombo vya Habari vya Serikali vitoe elimu ya afya huko vijijini, watu wengi wanakufa, kwa kukosa taarifa/habari za kiafaya. Kazi ya Serikali, ifanye kazi. Vyombo vya Habari vya Serikali vitoe elimu ya kilimo vijijini. Ni nani anayetoa habari hizo? Vyombo vya Habari vya Serikali vitoe tafsiri ya sheria mbalimbali, tuna sheria nyingi sana ambazo wananchi hawazijui na kisha tunawachukulia hatua na kuwatia ndani kwa sababu tu hawafuati sheria hizo. Ni nani anayejaribu kuwaelimisha hao wananchi ili wawe na haki yao ya msingi?

Kazi ya Vyombo vya Habari vya Serikali ni kutoa mikakati na mipango ya maendeleo huko vijijini. Kwa hiyo, mchango wa Vyombo vya Habari vya Serikali ni mkubwa, kama tukiweza kujipanga sawa sawa na wakaacha biashara ikafanywa na vyombo binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, kuna upungufu na udhaifu katika vyombo vya habari. Ni kweli kwamba, waandishi wa habari wanahitaji kupata mafunzo na hii inatokana kwamba, katika kipindi kifupi kumekuwa na ongezeko kubwa sana la Vyombo vya Habari, kama nilivyoeleza hapo mwanzo. Kwa hiyo, tunahitaji mafunzo, ambayo yanaweza kuboresha utoaji wa habari wa vyombo hivi.

Katika misingi hiyo, ningependa kuchukua nafasi hii, kuipongeza sana Serikali kwa kujenga na kutaka kuimarisha Chuo cha Habari. Lakini vilevile tungekuwa na

mafunzo ambayo yangeweza kutolewa na Serikali katika kuviboresha vyombo vya habari, kungekuwa na mafunzo ambayo ni *tailor made*, mambo ya *investigative journalism* yako wapi?

Tunakuwa na matatizo ya kutoa taarifa za Bunge hapa. Kungekuwa na mafunzo maalum, ambayo yanatolewa kwa waandishi wa habari, ambao watakuwa wanakuja hapa Bungeni na kutoa habari za Bunge. Kama tungeboresha huko, nina imani hata malalamiko ya Wabunge wengi katika kutoa taarifa ambazo labda siyo sahihi, yangekuwa yamepungua sana kwa sababu Vyombo vya Habari vingekuwa imara zaidi katika kutoa taarifa za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia kwa kirefu, ninataka nizungumzie kidogo kuhusu upande wa michezo. Ninachukua nafasi hii, kuipongeza sana Serikali kwa kufanya kazi kubwa katika kuendeleza michezo. Lakini labda tatizo moja kubwa tu ni kwamba, mkazo mkubwa uko kwenye mpira wa miguu, lakini sehemu nyingine za michezo kidogo hakuna mkazo mkubwa sana. Kwa hiyo, ningetaka kutoa rai kwamba, michezo iimarishwe na kama ikiwezekana, viwanja vya michezo mbali ya vile vya mpira navyo vingeweza kujengwa sehemu mbalimbali ili kuwafanya watu wengine ambao hawachezi mchezo wa mpira, waweze kushiriki sawa sawa katika shughuli za michezo. Lakini vilevile kama Serikali inaweza kutoa ruzuku kwenye upande wa mpira wa miguu, basi nilikuwa nafikiria kwamba, ingekuwa ni vizuri hata kama ni kidogo, ingeweza kutoa ruzuku hiyo ndogo kwenye michezo ya aina nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo, ninataka kuunga mkono hoja. Ningeomba Serikali iangalie jinsi ambavyo kunaweza kuwa na mtazamo wa kuhakikisha kwamba, vyombo vya habari vya kibiashara vinafanya kazi ya biashara na vyombo vya habari vya Serikali havijiingizi katika biashara, kwa sababu hizo ndizo sera zetu na mtazamo wetu. Vinafanya kazi za maendeleo kuelimisha wananchi sehemu za vijijini na sehemu nyinginezo katika maeneo ambayo vyombo vya kibiashara haviwezi kufanya vizuri. Kufanya hivyo, tutakuwa tumekuwa na umoja na ushirikiano katika kuwaelimisha, kuwafurahisha, kutoa habari kwa wananchi wote wa Tanzania na kwa usawa unaostahili.

Kwa hayo, ningependa kuunga mkono hoja. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, iliyoko mbele yetu. Naomba pia nitumie nafasi hii kutoa pongezi nyingi sana kwa timu yetu ya *Bunge Sports Club,* kwa kutuletea ushindi ambao ni wa nguvu kwa kuitandika timu ya *NSSF* na hivyo, kuonesha kandanda nzuri sana kwa Wabunge kwamba, siyo kazi ya kuisaidia jamii tu, pia kwenye michezo tupo. Pia naomba nitoe pongezi kwa timu yetu ya *Taifa Stars,* kwa ushindi waliotuletea dhidi ya timu ya Bukinafaso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba niende kwenye mchango wangu, uendelezaji wa michezo hapa Tanzania. Suala la Michezo hapa Tanzania kama

tutaliwekea mikakati ya nguvu na iliyo imara, ni sehemu nzuri sana ya kutoa ajira kwa vijana, akina mama na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma kwenye hotuba yake, lakini bado suala la kuimarisha hivi vyama vya michezo, kuanzia ngazi za Wilaya ni muhimu sana. Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, ametoa rai kwa Halmashauri kuweza kuzisaidia kuzifadhili, lakini kwa kweli ukiangalia Halmashauri zetu, zina uwezo mdogo sana. Tukiziachia Halmashauri unakuta kwamba, Vijana wanashindwa kupata nguvu ya kutosha kuweza kuendesha vyama vyao na hivyo kutokuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, mimi ningeiomba Wizara, iingilie kati suala la vyama hivi ili iweze kuwezesha, itoe fungu kidogo kuwezesha vyama hivi ili wafanye kazi kwa ufanisi na hivyo kuweza kujenga vyama vizuri vya michezo, vitakavyoleta ufanisi na kuleta ajira kwa vijana na watu wengine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni viwanja vya michezo, viwanja vingi vya michezo vimekuwa vinavamiwa sana maeneo mbalimbali hapa nchini. Watoto wetu wametengewa viwanja maeneo ya makazi, lakini vimechukuliwa vimefanyiwa shughuli tofauti. Matokeo yake watoto wanacheza barabarani na wapo ambao wameshawahi kugongwa na magari, kwa sababu hawana maeneo ya kuchezea. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara ihakikishe kwamba, maeneo ya michezo ambayo yanatengwa kwa ajili hiyo popote pale, kwenye makaazi, yaheshimiwe na yafanye kazi ya kusaidia watoto na asitokee mtu yeyote kwa ajili ya shughuli tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kunyanyua soka na mpira hapa nchini. Sasa hivi tunazungumzia tu mpira wa miguu. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunyanyua soka hapa nchini, sasa mpira amefanya imekuwa ni chachu, kila mmoja hapa nchini anapenda mpira wa miguu. Lakini, naomba tusiishie kwenye mpira wa miguu, twende kwenye michezo mingine kama *Volleyball, Basketball, Netball* na *Table Tennis*. Yote ni michezo mizuri, ikiwa itapewa mafungu, ikiwa itanyanyuliwa na ikiwa itapewa kipaumbele. Mpira wa miguu ambao kila mmoja ana *interest* ya kuungalia, unahusisha vijana tu na akina baba; je, akina mama mbona hatuoni wakinyanyuliwa jamani? Tunaomba Waziri wetu, aangalie sana michezo mingine hasa *Volleyball* na *Netball* ili pia akina mama siku moja na sisi tukijua kwamba tunacheza na timu za nje, tunapambana kwa ajili ya kuleta sifa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Taasisi ya Utangazaji ya Taifa. Kwanza, niipongreze Taasisi hii kwa kujitahidi kuweza kupeleka shughuli zao sehemu mbalimbali hadi vijijini imefika. Lakini bado kuna maeneo ambayo mpaka sasa hivi wananchi hawapati habari yoyote, siyo Redio Tanzania, si nyinginezo, hawajui kinachoendelea. Wangependa sana wapate kujua hata sasa hivi Bunge linafanya nini, lakini wanashindwa kutokana na mitambo ya matangazo kuwa mbali sana na jamii inakokaa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iharakishe kuhakikisha kwamba, mitambo ya utangazaji iko maeneo mbalimbali ili wananchi wapate huduma. Eneo mojawapo ni Tabora, Urambo, Kata nyingi tu ikiwepo Kata ya Kaloleni, wananchi hawajui kinachoendelea huku Duniani. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie suala hilo, mtambo upelekwe jirani ili wananchi waweze kupata huduma ya matangazo,

kujua nini kinachoendelea ikiwa ni haki ya kimsingi ya kila mwananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la wafanyabiashara kufungua kumbi za muziki, pamoja na starehe maeneo ya makazi ya watu. Suala hili limekuwa ni kero sana si Dar es Salaam tu kwenye watu wengi, kila mahali, Mikoa yote sasa hivi kumekuwepo na uhuru kupita kiasi. Mfanyabiashara anaamua tu kufungua *bar*, anafungua bila kujali kwamba, pembeni kuna mtu huyu, maadam kiwanja ni chake, anafungua biashara ambayo haiendani na watu wanaoishi pale. Ningependa kujua Wizara imeweka utaratibu gani, watu hawa wanafungua *bar*, kumbi za muziki, starehe, wametengewa maeneo gani au kuna sheria gani inayowadhibiti?

Tukiangalia maeneo ya makazi kuna shughuli mbalimbali zinafanyika; kuna watoto wadogo wanahitaji utulivu, kuna watoto wanaosoma wako *Day School*, wanahitaji utulivu usiku wasome, kuna watu ambao hawataki bughudha tu, lakini unakuta wanashindwa kufanya shughuli zao mpaka muziki uishee, unaisha saa kumi, unaisha saa nane, wanabaki macho kusubiria uishe ndio wafanye shughuli zao. Huku ni kuwanyima wananchi haki. Wizara tunaomba ifuatilie ihakikishe kwamba, sehemu zote ambazo wananchi wanaishi zisifunguliwe kumbi za starehe, ni kuwanyima wananchi haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la watu kuvuta sigara kwenye maeneo ya mikusanyiko ikiwepo sehemu za starehe na burudani. Serikali ilishatoa tamko kwamba, wanaomiliki maeneo ya starehe na burudani, wajenge vibanda kwa ajili ya wavuta sigara ili kutoa *privacy* kwa mtu ambaye hapendi harufu na wala hapendi kuona mtu akiwa anavuta. Lakini mpaka sasa hivi, sidhani kama hiyo sheria imefuatiliwa, sidhani kama hilo tamko limechukuliwa hatua kama inavyotakiwa. Unaweza ukatoka ukaenda hotelini unakula, jirani yako anavuta sigara. Mtu mwingine kama mimi sitaki kusikia harufu yake hata mita 100 na wengine hawapendi kwa sababu tunajua madhara yake. Kwa wale ambao wanavuta basi wafuate taratibu. Napenda Mheshimiwa Waziri, aliambie Bunge hili kwamba, wale ambao mpaka sasa hivi wanaendelea kukaidi tamko la Serikali, wale wamiliki wa *bar* ambao bado hawajajenga hivi vibanda na wale wananchi ambao wanavuta sigara hadharani kati kati ya watu, hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la upungufu wa bajeti kwa Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Kila mmoja anatambua kwamba, Chuo hiki ni Chuo pekee ambacho kinatoa fani ya sanaa kwa kusaidia kuendeleza sanaa ya Watanzania hapa nchini. Chuo hiki kimekuwa kinapewa bajeti ndogo sana na wakati mwingine kama mwaka 2006/2007, hakikupewa bajeti kabisa. Tusipoangalia kama Serikali itakwenda kwa mwendo huu, kwa kweli tutakuwa tunaua ufanisi wa Chuo hiki, matokeo yake ni kuua usanii, kwa sababu hakuna ufanisi wa kazi kusipokuwa na utaalam. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe kwamba, inatoa fungu la kutosha kwa Chuo hiki ili waweze kujiendesha vizuri na waweze kutoa wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza sanaa yetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Mfuko wa Utamaduni wa Taifa. Mfuko huu ni muhimu sana kwa kutambua kwamba, bila kuwepo Mfuko huu, utamaduni wetu utakuwa unaishia pasipoeleweka. Mfuko huu wa Utamaduni una akina mama ambao wanasuka vitu vidogo vidogo vya mikono, ambavyo vinahitaji gharama ndogo sana, ambavyo vinadumisha utamaduni wetu, lakini uwezo wao ni mdogo. Mwanzoni Mfuko huu ulikuwa unapata ufadhili, lakini kwa sasa hivi kutokana na kwamba umesaidiwa kwa muda mrefu, wafadhili wameondoka na sasa wamebaki wanajiendesha wenyewe. Lakini hawawezi kujiendesha kwa sababu wenyewe hawajasimama kikamilifu. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali sasa baada ya wafadhili kuondoka, ianze kutenga fungu kwa ajili ya Mfuko huu ili iwezeshe akina mama wale wanaojishughulisha kwenye shughuli ndogo ndogo kwa ajili ya kusaidia kuimarisha sanaa yetu ili waendelee kutengeneza vile vyombo vya kudumisha utamaduni wetu uendelee kuwepo na pia kuwasaidia kupata ajira ikiwa ni sehemu mojawapo ya kuleta maisha bora kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba nizungumzie suala la upotoshaji wa jamii, unaofanywa na magazeti hapa Tanzania. Mimi ninakerwa sana ninapoona gazeti, mwandishi wa habari pengine ameenda kwenye kumbi za muziki, amechukua watu ambao wamelewa, wanafanya vituko vya ajabu, wanaweka kwenye *Press*, wanalitoa ni gazeti linalotapakaa mitaani. Tunaifundisha nini jamii? Lile gazeti halisomwi na mtu mmoja tu, wala halisomwi na walevi, linasomwa na watu wenye akili zao, linasomwa na vijana, linasomwa na watoto na sana sana unakuta wanapenda kuyasoma magazeti ya udaku! Tunawaambia mataifa mengine kwamba tunafundisha nini? Watu wanatoa picha za uchi, ambazo kwa kweli hazifai hata kuzitamka, ukiziangalia kwa mtu ambaye unamheshimu, ukifunua unaacha. Lakini Serikali imenyamaza, yanaendelea kutoka na yanauzwa mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweza kupambana na vijarida ambavyo vilikuwa vinapotosha jamii huku nyuma vikaweza kuzuiliwa. Ni kwa nini mpaka sasa hivi magazeti haya yaachiwe yaendelee kutoa picha kama hizi? Mimi naiomba sana Wizara hii ichukue hatua za Haraka, vinginevyo tunawapotosha vijana na watoto. Tunakuta watoto wanazungumza mambo ya ajabu mitaani, wanafanya vituko vya ajabu, kumbe sisi wenyewe ndio tunaowafundisha kupitia Vyombo hivi vya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, asante. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naipongeza bajeti ya Wizara hii. Kwa kweli naipongeza sana, nampongeza Waziri mwenyewe, nawapongeza Manaibu wake wawili, ambao wako *active* kwenye masuala ya Wizara hii. Siku zote tunamwona Mheshimiwa Joel N. Bendera na Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, namna wanavyoihangaikia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Bunge lako hili Tukufu, mimi nina ombi binafsi kwa Mheshimiwa Waziri. Ombi hili ni kutokana na kauli yake ya jana ya kuwa Uwanja wa Taifa haujakabidhiwa kwa Serikali. Ombi hili namwomba Waziri akubali *match* ya Mozambique na *Taifa Stars* ichezwe kwenye Uwanja huu. Hii *match* ni vita, wala si *match* ya kuanza kuzungushwa zungushwa au kutafutiwa viwanja. Kuwe na maandalizi maalum ya kufanya *match* hii ichezwe kwenye Uwanja huu ili tupate mashabiki wengi wa kuweza kuingia na kuweza kuisadia na kuipatia ushindi Timu yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya michezo, bado sijaona mpango wa Serikali au mpango wa watu binafsi, kuanzisha *Sports Academy* katika nchi yetu. *Academy* hii ina nafasi kubwa sana ya kuchangia michezo ili iweze kunyanyua vipaji. *Academy* hii inaeza vilevile ikafundisha makocha, wachezaji na hata kuuza wachezaji nje ya nchi kwa mpango ambao utawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli licha ya kuwa hatuna *Academy*, tulishaanza kuwa na Kijiji cha Michezo, lakini Kijiji hiki kiko Kurasini na mpaka sasa hivi kimekufa na hakitamaniki na pembeni yake kuna Uwanja Mpya wa Taifa, ambao ni mzuri na ni wa kisasa. Ninaiomba Serikali ianze kuchangia au iwe na mchakato maalum wa kuweza kuhakikisha kijiji hiki sasa hivi kinaanza kutengenezwa upya na kuweza kutumiwa na wanamichezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanja vingi Jangwani, bado hatujakuwa na programu yoyote ya Serikali ya kusaidia viwanja hivi ili viweze sasa kuwa imara na viweze kutumika na wachezaji wa timu zetu katika Mkoa wa Dar es salaam na Mikoa ya Jirani na Tanzania kwa ujumla. Viwanja hivi ambavyo tuna nafasi kubwa sana ya kujenga *Sports Academy*, si lazima Serikali ichangie peke yake, tunaweza tukawapa wafadhili wakakubali kutumia majina yao katika *Academy* hii na wako tayari kuweza kuchangia na kuweza kujenga *Academy* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja huu wa Taifa mpya ambao tunaujenga, hautaweza kupokea wachezaji kwa kufanyia mazoezi. *Product* itakayoingia kwenye uwanja ule, lazima itoke kwenye viwanja vya chini. Kwa maana hiyo, kuna umuhimu sana sasa hivi wa kuviendeleza viwanja ambavyo tunavyo ili wachezaji waweze kwenda katika uwanja huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine binafsi kwa Uongozi wa *NSSF* na najua wapo hapa Bungeni ni kuhusu namna ya kuendeleza Uwanja wa Karume. Uwanja huu wa Karume una *sentimental value* kubwa sana kwa nchi hii. Ni Uwanja wa zamani, lakini ni uwanja ambao vilevile unaweza ukapunguza msongamano au ukapunguza pilika pilika za kutumia Uwanja wa Taifa. Uwanja huu ukiboreshwa. unaweza ukalipa, wakati *NSSF* wakikaa na *TFF*, waandae programu nzuri, namna gani uwanja huu unaweza kutengenezwa na kurudisha pesa ambazo *NSSF* au Shirika lingine litatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Civic Centre*. Nchi nyingi zimejenga *Civic Centre*, sisi Tanzania bado hatuna. *Civic Centre* ni maeneo ambayo tunaweza

kuweka vijana wakaweza kujadili mambo yao, wakaweza kuwa na maadili mazuri kutokana na *Centres* hizi, wakawa na *Theatres* ambazo wanaweza kuonesha michezo yao au wakaonesha mambo mbalimbali ya kiutamaduni ambayo wanayaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze *Coca Cola - Copa Cup* kwa mfano mzuri, waliloonesha nia ya kuanzisha mashindano ya vijana na kuweza kupata vipaji vipya ambavyo vilikuwa havionekani sababu walikuwa hawana uwezo, lakini sasa tumeviona vipaji hivi na nina hakika Kocha wa Timu ya Vijana ya Taifa, amepata wachezaji wazuri, ambao baadae watakuwa ni tegemeo la Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Kocha wa Timu ya Taifa, Maximo pamoja na Ally Bushiri, kuweza mpaka sasa hivi kuifikisha Timu yetu katika sura ya Dunia na sura ya Afrika. Tanzania sasa inaogopwa. Sasa hivi huko Ghana tayari wameshaanza kujua kwamba, Tanzania inakuja na kwa kweli tunakwenda. Kwa hiyo, mimi nafikiri niwapongeze, lakini niipongeze vilevile Serikali kwa mchango wake na hii Serikali ione namna tu walivyochangia mpira huu, timu hii imeweza sasa kupata mafanikio. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali pamoja na Rais wetu, kwa kuona umuhimu wa mchezo huu wa mpira wa miguu. Mimi natetea mpira wa miguu kwa sababu ni mdau wa mpira wa miguu. Waheshimiwa Wabunge wengine, wanatetea michezo ambayo wao ni wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa changamoto kwa Serikali, ikishirikiana na *TFF* na kwa wafadhili mbalimbali wa michezo, kwa mfano, wafadhili wa mpira wa miguu. Timu hizi zinapata gharama kubwa sana kujiendesha na wafadhili pesa wanazotoa mpaka sasa hivi ni ndogo sana, kufuatana na faida wanayoipata na matangazo ya timu hizi katika *Premium League* na timu nyingine ambazo zinashiriki katika mashindano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua kwenye Makamupuni ya Simu, ikifika shilingi 200, simu yako inakata hizi shilingi 200 kwa wateja milioni mbili ni shilingi milioni 400. Kwa hiyo, kwa mwezi una nafasi ya kuchangia si chini ya shilingi bilioni tatu ili kwenye timu hizi ziweze kushiriki na zipate faida kwa mchango wao wanaotoa kwa kuzitangaza biashara ya makampuni ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa changamoto nyingine kwa *Bongo Flavour,* miziki hii ya kisasa ni mizuri, inafurahisha, inapendekeza na inaonesha namna vijana wanavyoweza kuimba na kuwa na vipaji vikubwa sana. Tatizo kubwa vijana wengi wanafikiri uwe mwimbaji wa *Bongo Flavour* kutokuwa na elimu. Mastaa wengi Marekani akina *II PAC* na wengine wote, wamepata elimu ndio wanaweza kuimba nyimbo nyingi zika-*sustain* kwa kipindi kirefu sana. Waimbaji wetu sisi wakishatoa nyimbo moja basi anafifia kwa sababu hakuwa na elimu ya kutosha ya kuwafikihia ujumbe wale ambao wanataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali nayo iwasaidie vijana hawa katika kulinda haki miliki za nyimbo zao. Hizi nyimbo nyingi zinauzwa mitaani, mwimbaji anaimba lakini faida anayopata ni ndogo sana, kutokana na muda anaotumia kutunga nyimbo hizi

au kushirikiana na wenzake. Kwa kweli wanapata gharama kubwa sana. Tunaona mitaani namna tunavyopigwa mizinga, kuwasaidia katika kurekodi nyimbo zao au kuwasaidia katika mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi binafsi kwa Ndugu Tido Mhando. Aliyemrudisha Tido Mhando Tanzania, Mungu atamlaza pema. Wazungu wanasema Tido ame-*captivate contrast*, Tido ameifanya TVT sasa ni kivutio kikubwa na TV nyingi sasa hivi na vyombo vya habari, vinaona wivu namna TVT inavyofanya kazi. *Quality* ya vipindi vyake imeboreshwa, *quality* ya *transmission* zake imeboreshwa na haya yametokana na Tido kuchukua *station* hii.

Nampongeza sana na naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, tusiipige vita *station* hii. Hii ni *station* ya Kitaifa. Ili nayo ijiendeshe, inataka ifanye biashara. *BBC* inafanya biashara; kwa nini TVT isifanye biashara? Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Ndugu Tido Mhando na tuisaidie TVT, tuipatie fedha zaidi iwe na *back system,* ifanye kazi mpaka wengine waone wivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza nimeshapigiwa. Baraza la Kiswahili, sasa liandaliwe lipewe kazi ya kutafsiri sheria zetu kwenye Lugha ya Kingereza kuja kwenye Lugha za Kiswahili, ili ziweze kuwafikia wananchi, wajue sheria kwa lugha yetu hii ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, wengi wamezungumzia kuhusu magezeti lakini mimi ninachoshangaa na kunisikitisha sasa hivi kwenye kila *traffic lights* kuna *CD* za pilau zinauzwa. Unafuatwa kabisa unaambiwa kuna pilau na kuna biliani. *CD* hizi zinadhalilisha taifa hili na *CD* hizi kuwe na *operation* maalum ya kuwatafuta na kuwakamata wote wanaouza *CD* hizi za X ambazo sasa hivi watoto wengi wanajifungia vyumbani na *DVD* zao kutazama *CD* hizi. Hili ni ombi langu maalum, pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge, tujaribu kuwakamata wote wanaouza *CD* za ngono, *CD* za maadili mabaya, *CD* ambazo zinapotosha jamii na *CD* ambazo si nzuri kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeneo hayo machache, nakushukuru. Namwachia ndugu yangu, Shehe Mudhihir, naye aweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ningependa nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe pongezi za dhati kwa Serikali hii inayoongozwa na CCM, kwa kuruhusu watu binafsi kuanzisha Vyombo vya Habari na hatimaye wameweza kuunda umoja wao *(MOAT)*.

Naipongeza Serikali kwa sababu vyombo hivi binafsi vinakuja kusaidiana na TUT kupitia vyombo vyake vya RTD na TVT. Vinasaidia vyombo hivi katika kuelimisha jamii, kuburudisha jamii na kuisogeza dunia yote hii hadi katika vijiji vyetu. Lakini kama alivyosema msemaji mmoja kwamba, vyombo vimeongeza vilevile ajira, sio kwa wanahabari tu lakini kwa wasanii wetu, wauzaji wa magazeti na ni msaada mkubwa kwa wafanyabiashara katika kutangaza bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa fursa hii, Redio Tanzania Dar es Salaam na Television ya Taifa, vikajikuta vinashindwa kuhimili ushindani, kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, aina ya vipindi ambavyo tulikuwa tunavitoa katika RTD na TVT vilikuwa havina mvuto kwa jamii ya kisasa.

Pili, Serikali kwa sababu si mfanyabiashara, ilishindwa kukidhi mahitaji ya kifedha kwa ajili ya kuviendesha vyombo hivyo. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka huu 2007/2008, TUT imepunguziwa bajeti yake kwa shilingi bilioni mbili. Katika mazingira hayo ni dhahiri, hata hilo jukumu la kufikisha tu huduma za afya kama tulivyoambiwa hapa na sheria vijijini isingeweza kufika. Kwa kuliona hili, Serikali ikaamu kuiruhusu TUT kuingia katika ushindani wa kibiashara. *(Makofi)*

Hatua hii mimi nasema si dhambi wala sio ngeni Duniani, tumepewa mfano hapa na kaka yangu, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, South Africa wanaruhusiwa *South African Broadcasting Cooperation* kuingia kwenye ushindani, hata jirani zetu tu hapa Kenya, *KBC* tunaona *BBC*, jambo hili halipaswi kuwa geni na kituko na kiroja kufanyika katika nchi yetu ya Tanzania. Hivi karibuni kumejitokeza hoja nzito nzito za *MOAT* dhidi ya TUT, wanasema TUT haiendeshi ushindani wa haki kwa *MOAT*, ati kwa madai yao sababu inapata ruzuku toka Serikalini. Kwamba, katika zabuni inaweka pesa nyingi ili ishinde kuliko vyombo binafsi vya *MOAT* na hivyo kufuja pesa za walipa kodi wa nchi hii.

Msemaji aliyepita ambaye alitangaza ana *interest* zake kwamba, naye ni mmoja wa *MOAT*, alisema wao walitenda ile zabuni kwa shilingi milioni 70, TUT ikatenda kwa milioni 200. Unaposema sisi tumetenda kwa shilingi milioni 70, hiyo ni *cartel*, ni kupanga bei na hizi *cartel*, ndio zinatuumiza sana sisi Watanzania.

Kule Lindi na Mtwara korosho zetu *cartel*, hazinunuliki, uagizaji wa mafuta hapa *cartel*, mafuta hayanunuliki na hivi sasa hata *TPDC* kuruhusiwa kuingiza mafuta tayari imeanza kupigwa vita. Sasa TVT, Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, tunatakiwa tuiunge mkono TUT, walau kwa kuvunja huu mwiko tuwakatae wafanyabiashara kupanga bei. Ninashangaa sana miongoni mwetu tunapotokea kuipiga vita TUT, inashangaza sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wa mambo bwana ni kama hivi ufuatavyo; matajiri wa *MOAT* wametanguliza mbele faida, sio dhambi, maana biashara siku zote ni faida. Kwa hiyo, mimi nasema mtu anayeingia kwenye biashara, anatarajia kupata faida,

haki yao, lakini kutarajia kwao kupata faida, kusiwe sababu ya kuzuia ushindani wa TUT. *(Makofi)*

Kwa upande wake TUT inafikiria zaidi utoaji wa huduma bora na muhimu kwa wananchi wetu. Faida ndogo wanayopata TUT ni kwa ajili tu ya kuviwezesha vyombo vyake kuweza kujiendesha. Mishahara wanayopata wanahabari wa TUT, haifikii hata robo ya vile vyombo binafsi, ni kwa kuikuza tu TUT ndiyo wanahabari wa vyombo hivyo na wao wanaweza kuja hapa Dodoma wakaingia Chako ni Chako kama wanavyoingia wenzao. *(Makofi)*

Ushindani huu wa TUT umeleta mambo yafuatayo: Umejenga umaarufu mkubwa sana na umaarufu huu wa TUT ndiyo unaotia hofu, homa na kihoro *MOAT*, lakini umeleta unafuu vilevile kwa wananchi wa kawaida, ambao baadhi ya vipindi kuviona kwa mwananchi wa kipato cha chini ilikuwa ni adimu kama jasho la kuku, kabisa kabisa. Kuna vipindi hapa mpaka ulipie bwana ndiyo unaweza kuviona, kupitia TUT sasa hivi hata ndugu yangu aliyekuwa Mchinga, akiwa na jenereta tu pale mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Ruzuku ya Serikali kwa TUT, ni ya muda na kwa huu mpango wa utendaji ulioandaliwa na TUT mimi naamini ndani ya miaka mitatu mpaka mitano Serikali ruzuku yake itaelekezwa katika maeneo mengine na TUT itakuwa imejiandesha kwa ukamilifu kabisa. (*Makofi*)

Huyu mtu anayeitwa Tido Mhando, kwa kweli si mchezo amekaa kwenye vyombo vya nje, amejua maana ya habari kwa nchi, mtu amesema Serikali hapa kazi yake sio kufanya biashara ni huduma tu. Lakini kuna maeneo Serikali haiwezi kutoa tu, tumekataa sisi kubinafsisha bandari tumejua umuhimu wa bandari kwa Serikali, tumekataa kubinafsisha *National Housing,* tumejua umuhimu wa makazi ya watu na habari ni moja ya sekta hiyo. Hatuwezi tukaiacha habari holela holela tu nchi itateketea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuiunge mkono Serikali katika hili, tuiunge mkono TUT katika hili, matajiri hawa wa *MOAT*, wameingia katika biashara hii kwa hiari yao wenyewe. Kama walivyoingia wafanyabiashara wengine kwa hiari yao wenyewe katika sekta mbalimbali, hebu tuulizane maswali machache yafuatayo, tuone majibu yake yanakuwaje:-

Hivi kwa watu binafsi wenye uwezo, walioamua kufungua shule binafsi, tuwaruhusu kutupangia karo za watoto kwenye Shule za Serikali na mishahara ya walimu wetu ili wao wasiumie; inaingia akilini? Tuwaruhusu watu ambao wamefungua hospitali binafsi, watulazimishe Serikali kupunguza bei ya huduma ya matibabu na dawa katika zahanati zetu, vituo vyetu vya afya na hospitali zetu? Tuwaruhusu waagizaji wa mafuta waizuie Serikali kwamba, *TPDC* isilete mafuta nchini?

Anayeingia kwenye biashara ajue hii ni dunia ya ushindani lazima awe tayari kukabiliana nao ushindani. Tusifanye mchezo na TUT, duniani kote huko habari

kipaumbele chake cha kwanza ni uzalendo, duniani kote na mimi nitawapeni mifano hapa. Wengine walikuwa wadogo sana, mimi nilikuwa *Middle School*. Wakati Ian Smith kule Zimbambwe anawapopoa Wazimbabwe kama Ngedere, kuwafukuza katika ardhi yao, vyombo vya magharibi vyote vilikuwa kimya. *(Makofi)*

Mugabe leo anapambana kutaka kuwarudishia ardhi wale wale waliokuwa wanapopolewa kama ngedere na Ian Smith, vyombo hivyo huko ndiyo vinapiga kelele kumlani Mugabe. Bila TUT hatuna wa kutusemea na tunaona sasa hivi, watu badala ya kulaumu *cartel* ya mafuta, wanalaumu bajeti kwa kuongeza shilingi 124, halafu Wabunge tunapigia makofi na kuikandamiza TUT, inatisha sana. Korea ya Kaskazini na Iran kuwa na mtambo wa *Nuclear*, vyombo vya huko vya wakubwa ni nongwa, lakini Israel imetangaza juzi inatengeneza mtambo wa *Nuclear* kimya! *(Makofi)*

Wakiingizwa kuku hapa na vyakula vya kopo kutoka duniani huko, magazeti ya wakubwa kimya huko, likitokea suala la minofu ya samaki hapa vyombo vya habari humu humu ndani ndiyo vinakuwa vya kwanza kupiga debe tufungiwe biashara! TUT ndiyo mkombozi wetu sisi hatuna kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kabla kengele ya mwisho haijalia. Ninawaomba radhi sana *TFF, TFF* ni imara na ina viongozi madhubuti sana, lakini isifanye kazi kwa jazba, kuna mashindano ya *TUSKER* yanaendelea Mwanza, Athuman Idd Chuji, amevunja heshima kwa kuonesha ishara ya matusi. Kamati inayosimamia mashindano yale imemwadhibu kwa kumpa onyo, *TFF* inasema hapana tunakufungia mechi sita, *TFF* hawasimamii mashindano hayo. Swali langu, kama mchezaji huyu angekuwa ametoka Kenya au Uganda, *Villa* au *Tusker; TFF* wangepata wapi nguvu ya kuwafungia michezo sita kule kwao? *(Makofi)*

Sasa mimi siwaombi Serikali, maana hatutaki muingilie michezo, lakini nafikiria wale watu wangeangalia saikolojia ya mchezaji huyu, ambaye amekaa nje muda mrefu bila kucheza mpira, ameingia pale mashabiki wanamdhihaki hata wachezaji wakubwa kule Ulaya wanalalamika akina Thiery Henry kwamba, wanaitwa nyani, saikolojia ni kitu kingine. Lakini vilevile tufuate na utawala wa sheria, unapotaka kumhukumu mtu, mwite kwanza umpe nafasi ya kujieleza umsikilize na yeye, huyu alijieleza kwenye Kamati kule wakaona adhabu anayostahili ni kupewa onyo, *TFF* hawakumwita kujieleza, kisheria hilo ni jambo gumu sana. Hata Mwenyezi Mungu, alipokuwa anataka kumwadhibu Adam alimwita kwanza na kumwuliza kwa nini umekula tunda la mti huu, alimwuliza kwanza, ndiyo na hili si jambo la porojo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, ume-*declare interest*?

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Nime-*declare interest,* mimi ni *senator* wa Yanga. Nasema hili kwa sababu katika kesi ya Khamis Rajab Dibagula; Majaji Samatta, Mroso na Jaji Munuo, walizungumzia suala hili la umuhimu wa mtu kupewa nafasi ya kusikilizwa kabla ya kuhukumiwa.

Nami ningependa *TFF* wa-*review* tena jambo lao na ningeomba kuwanukuu hao wazee waliposema hilo: "*The laws of God and man both give the party an opportunity to make his defense if he has any, I remember to have had it observed by a very learned man upon such an occasion that even God himself did not pass sentence upon Adam before he was called upon to make his defense. Adam says, God, where are you? Has you not eaten the fruit of the tree where off I commanded you not to eat and the same question was put to Eva also."*

Sasa *TFF* sitazamii kama inaweza kuwa mkubwa kuliko Mungu, kama Mungu aliona umuhimu wa kumsikiliza mkosaji, nategemea kwamba na mtoto huyu atatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga tena mkono hoja, asante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa haya machache, napenda kuomba hiyo *message* yangu iwe *sent and delivered* kuhusiana na suala la utamaduni. *(Makofi)*

Kwanza, nawashukuru kabisa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kipindi hiki, inaonekana na ningependa tuwape moyo na tuweze kuwasaidia zaidi. Mimi nilikuwa na angalizo tu kidogo, kuangalia sehemu ambayo tumeiacha ambayo ni muhimu sana. Kwanza kabisa, katika kuadhimishwa kwa Siku ya Utamaduni Ulimwenguni, tarehe 21, kauli mbiu iliyotumika ni kwamba, utamaduni ni uhai. Hiyo nakubaliana nayo kabisa, nafikiri sote tunakubaliana nayo. Pia ningependa kukubaliana na Mwenyekiti wa Kamati hii, Bwana Komba kwa matamshi aliyoyatoa hapa, ambayo mimi yamenigusa sana. Ame-*define* utamaduni akasema ya kwamba, utamaduni ni mchanganyiko wa mambo mengi yakiwemo ya kiroho, kimwili, kifikra na kihisia, ambayo huitambulisha jamii. Hii ni pamoja na mifumo ya maisha, haki za msingi za binadamu, mifumo ya maadili na imani. Hiyo ni kweli kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Tanzania hapa tumefanya kosa moja kubwa ni kwamba, Sera yetu ya Habari na Utamaduni, inaua utamaduni wa kiasili wa Kiafrika, ambao ndiyo msingi wa utamaduni wa Kitanzania. Kwa sababu tumepuuza mambo mengi. Kwanza kabisa, nataka ku-*define* lugha ni nini? Lugha ni chombo cha mawasiliano, ni kitu kama gari, baiskeli kwa ajili ya kuwasiliana. Pamoja na hayo ni chombo ambacho pia kinasaidia kuelimisha kutokana na hayo mawasiliano, vilevile kinaweza kutoa tahadhari mbalimbali kwa mfano, tahadhari kama za Ugonjwa wa UKIMWI, zinaweza kutumika katika lugha.

Lugha vilevile *is an expression of culture,* ndipo unapoeleza ni kielelezo cha utamaduni fulani. Sasa utamaduni wa Tanzania au utamaduni wa Mtanzania ni upi. Kama tunasahau ya kwamba, kuna lugha za asili na utamaduni wa asili, ambao ndiyo chimbuko la utamaduni wa Tanzania, kwa sababu wakati wa michezo ikifika kwenye sherehe tunapeleka ngoma za Msukuma, ngoma za Mndengereko, lakini tunasahau ya kwamba, zile lugha ndizo ambazo zinaihifadhi ule utamaduni.

Kwa hiyo, nilipenda hii Wizara iangalie wengine katika nchi nyingine wametuzidi. Kwa mfano, Kenya, sasa hivi inaongoza katika kufundisha Kiswahili, walimu wengi wanaokwenda kufundisha nchi za nje Kiswahili ni Wakenya. Wao wako *serious* na Kiswahili kuliko sisi, pamoja na kwamba sisi tunafikiri ni mali yetu, lakini Kiswahili sasa hivi mpaka Cameroon na Afrika Kusini wanazungumza. Kwa hiyo, Kiswahili ni lugha ya kuunganisha watu wote wa Afrika na ni lugha iliyokuwa inatumika wakati wa biashara tangu enzi za utumwa, kwa hiyo, kitakua.

Lakini sasa hizi lugha za kienyeji tunapozipuuza kwa mfano, sasa wanasema lugha ya Wahadzabe imepotea, haitakuwepo tena. Sasa fikiria lugha kama ya Wasukuma na wingi wao na Wanyamwezi ipotee; hiyo itakuwa ni faida au ni hasara? Kwa nini tusiihifadhi, tuiandike ili wale wanaozaliwa pale nao wajue kwamba, mimi kwa *identity* ni Msukuma? Lakini pia ni Mtanzania, lugha yetu ni Kiswahili na ninazungumza Kingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kihispania na lugha nyingine zote. Hivi ndiyo Wazungu wanavyofanya, anazaliwa ni Mwingereza, anajua yeye ni Mwingereza, halafu anaendelea kufanya mambo ya tamaduni nyingine.

Kwa hiyo, mimi ningeomba kwamba, Serikali yetu iangalie kwa mfano, mifano kama ya Wamishenari, walipokuja hapa waliona umuhimu wa kuandika lugha za kienyeji, waka-*translate* mpaka Biblia katika lugha za kienyeji ili *message* ifike. Sasa *message* kama ya UKIMWI, inashindwa kufika kwa wananchi kwa sababu hapa Tanzania kuna watu hawawezi kuzungumza Kingereza na Kiswahili. Nenda hata hapa Usukumani ukizungumza Kiswahili wanasema huyu ni Mswahili wanazungumza lugha yao. Amesema hapa Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya kwamba, kuna watu wengine hata redio hawasikii, haifiki kule waliko.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naiomba Serikali kwa kuangalia mifano kama ya Wakenya na Waganda, jinsi ambavyo wameendeleza elimu na utangazaji, kila lugha ina *broadcasting station* yake ya lugha yao. Kuna ubaya gani kama Mmasai au Mndengereko anakaa asubuhi anasikiliza Kimasai kwenye redio jioni, anarudi anasikiliza Kimasai?

Atafurahi sana kuwa Mtanzania, kwa sababu atajiona kwamba yeye ni sehemu ya Tanzania kwa sababu Mzungu anatoka Ulaya kuja kuangalia Mmasai. Sasa lakini sisi yule Mmasai hatuoni kana kwamba ana utamaduni wake unaostahili kuandikwa na kuzungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama ya Nigeria, imepiga hatua kubwa sana katika kuendeleza sinema, wana-*compete* na *Hollywood* na ile ya India. Sasa utamaduni wetu wa Kiafrika unaonekana katika dunia nzima, kwa sababu wameu-*value* lakini ukiangalia hata kwa Kingereza wao wako mbele. Kwa hiyo, tukiangalia mfano kama wa Afrika Kusini, kwa miaka 400 wamekuwa wakizungumza Kingereza na Kidachi, lakini utamaduni wao uko pale pale. Ukiangalia hata lugha, ile lugha ya *Africans* imechanganyikana na lugha za kienyeji, wameweza kutunza utamaduni wao na pia wakaendelea ku-*acquire* vitu vingine vya watu wengine. Kwa hiyo, sisi tunapopuuza lugha za kienyeji, tunafanya makosa sana na inaonekana ya kwamba, ile dhana ya

kusema ya kwamba eti tukifanya lugha za kienyeji tunafanya ukabila, hii ni dhana potofu na tutakuja kulaumiwa sana na vilevile tutakuwa tunawakosea sana mababu na mabibi zetu. Kwa sababu zile lugha ziliendelezwa, zikawa *perfected* na zikatumika kwa miaka mingi.

Sasa kwa nini tuzionee haya lugha hizi, kwa nini tamaduni zetu za Kiafrika zisiandikwe? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nina mapendekezo kidogo. Napendekeza ya kwamba, kwanza kuwe na taasisi au asasi ambayo itashughulikia masuala ya *African linguist experience,* tuweze kuziandika zile lugha zote za Tanzania, kwa sababu ukienda Marekani, *Library of Congress,* wamerekodi lugha zote hata lugha zetu hizi zote ziko kule. Labda sasa hizi lugha zitakuwa zinazungumzwa Ulaya baadaye, kwa sababu inaonekana sisi hatuzitaki. Lakini sasa tukifanya kitu kama hicho ni kwamba tuweze kuwa na magazeti ambayo yanaandika lugha za kienyeji kwa kuwasiliana na wananchi. Vilevile kuwa na *FM Radios* zinazozungumza Lugha za Kienyeji, tuweze kuwa na machapisho mengine na lugha za asilia ziruhusiwe nchini kote, kwa sababu ni lugha zetu wala tusizionee aibu.

Tuwe na *National Museum,* ambayo itakusanya tamaduni zote za Kiafrika lakini tuwe na *museum* ambazo ziko katika maeneo mbalimbali, wawe na *pre-servation* ya vitu vyao ambavyo vizazi vijavyo vije kuona ya kwamba, hapa kweli tulikuwa sisi ni Wahadzabe au sisi ni Wagogo. Kwa mfano, Wagogo kazi ambayo imefanywa na Marehemu Mzee Zewose ni nzuri sana, lakini haijawa *preserved* mahali popote. Kwa mfano, ingekuwa rahisi sana kuelewa makabila mengine kwamba, yakoje na yana msimamo gani na yana tamaduni. Sijui utamwelewaje Mkurya, kama huwezi kusikiliza kile Kikurya ukakizungumza na ukamwelewa. Kwa sababu yeye *expression* yake na mambo yake yote ni katika lugha yake na yeye anaona yuko sawa. Lakini wewe unaweza ku-*judge* kwamba, huyu mtu pengine yeye ni mtu pori, kumbe yeye anakuona kwamba wewe ndiyo humwelewi. *(Makofi)*

Haya ndiyo machache niliyokuwa nayo, lakini pia ningependa kuzungumza kuhusu suala la kuendeleza muziki wa kiasili. Kuwe na asasi au pengine kama ni taasisi yetu ya Chuo cha Sanaa Bagamoyo, ipewe nguvu ya kuweza kuendeleza michezo yetu, kuiandika miziki na kui-*modernize* na pia michezo ya asili kama mieleka, ambayo pia tunaweza tukaieneza duniani, kwa sababu ilikuwa ni michezo mizuri. Sasa tusipoiendeleza sisi; nani atajua kwamba, kulikuwa na mieleka hapa ambayo ilikuwa inafurahisha watu?

Pia, ningependa kutoa rai ya kwamba, jamani tuangalie Katiba yetu katika ibara 18, inayozungumzia kuhusu uhuru wa mawasiliano na imewekwa iko bayana na *free* kwamba, kila mwananchi ana haki ya kuwasiliana na mwingine na kutoa mawazo yake bila kuzuiwa na mtu yeyote.

Kwa hiyo, tusije tukaingiza mambo ya siasa katika kutaka kuzuia uhuru wa habari kwamba, sasa tuanze kuminyaminya uhuru wa habari. Tutaonekana sisi ni watu wa ujima, kwa sababu hayo mambo yalipitishwa katika enzi ya karne ya 19 huko nyuma kwamba, *freedom of expression* ni kitu ambacho kinaruhusiwa kabisa. Kwa hiyo,

ningependa Serikali iache kufikiria namna ya ku-*control* yale maeneo ya uhuru wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Asante sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, sasa niseme tu kwamba, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameomba kuchangia kwenye hoja hii ni wengi na si rahisi kuwapa nafasi wote, kama mnavyojua tatizo letu ni muda.

Kwa hiyo, jioni ya leo, tutakuwa na dakika 45 za uchangiaji zaidi, ambapo matarajio yetu ataanza Mheshimiwa Idd M. Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynab M. Vulu na Mheshimiwa Suileman O. Kumchaya. Kama muda utaruhusu kuna watakaochangia pungufu ya muda huo, huenda na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, akapata nafasi pia. Baada ya hapo atafuata Naibu Waziri, kama itakavyokuwa imepangwa na Mheshimiwa Waziri, halafu baadaye Naibu Waziri wa Pili na Mheshimiwa Waziri, atajibu hoja zetu. Vinginevyo, kwa kazi ambazo zimepangwa hapa asubuhi ya leo zimekamilika, naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi ya kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza kabisa, nachukuae nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya tangu walipopewa dhamana ya kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Nafahamu kabisa wakati wanapewa dhamana ya kuongoza Wizara hii, tulikuwa na matatizo mengi sana ama migogoro mingi sana, katika vilabu vyetu na vyama mbalimbali vya michezo. Lakini wameweza kuongoza kwa umakini kabisa na hivi tunavyozungumza ni kwamba, migogoro mingi katika vyama vya michezo na vilabu imeisha. Nitolee tu mgogoro ambao ulisumbua sana Klabu ya Yanga kwa muda mrefu, lakini kwa kweli busara ambazo viongozi hawa walizitumia, ziliwezesha kupatikana muafaka ambao leo hii Yanga wamekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwapongeze pia wale ambao walisaidiana kuleta muafaka katika Klabu ya Yanga. Mpira wa Tanzania una vilabu viwili vikubwa. Vilabu hivi vinapokuwa na matatizo, basi soka la Tanzania lazima litayumba. Lakini wapo watu ambao wamejitahidi sana, pamoja na Wizara kuhakikisha kwamba, wanatatua migogoro iliyokuwepo katika vilabu hivi. Nampongeza sana mzee wangu, Rignald

Mengi, ambaye alianza kutafuta muafuta Klabu ya Yanga kabla ya ndugu yangu Manji, kuja kumalizia na muafaka kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata Simba na kwenyewe nako kesi zilikuwa nyingi sana, lakini tunavyozungumza Simba nao wako vizuri na ndiyo maana wamechukua ubingwa hivi karibuni. Kwa hiyo, niwapongeze wote ambao kwa kweli wamejitahidi kuondoa migogoro katika vyama na hivi vilabu vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niitumie nafasi hii pia, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada alizozifanya kuhakikisha kwamba, ama kuhamasisha Watanzania waipende Timu ya Taifa, kuhamasisha wachezaji wetu wafanye vizuri na kweli wamefanya vizuri, mpaka hivi sasa Timu yetu ya Taifa inafanya vizuri kutokana na jitihada ambazo Mheshimiwa Rais, amezionesha kwa timu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Wadhamini wa Timu ya Taifa, ambao nao wamejitahidi sana kutoa motisha na misaada mbalimbali, kuhakikisha timu yetu inafanya vizuri, wakiwemo *Serengeti Breweries,* kwa kweli udhamini wao ni wa muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Shirikisho la Soka Tanzania *(TFF),* kwa kuanzisha mashindano ya vijana chini ya miaka 17. Huwezi kuwa na Timu ya Taifa nzuri, kama hujawaandaa wachezaji tangu wakiwa wadogo. Kwa kitendo cha kuanzisha mashindano haya ya vijana chini ya miaka 17, kimeibua vipaji vingi sana na tunategemea baadaye tutakuwa na Timu ya Taifa, itakayokuwa na wachezaji wazuri sana. Mashindano hayo ambayo yalijulikana kama *Copa Coca Cola* yalidhaminiwa na Kampuni ya Soda ya *Coca Cola,* ambao udhamini wao umehamasisha sana na umefanikisha sana mashindano haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili pia ni vyema nikachukua nafasi hii kuwapongeza vijana wangu wa Kinondoni, ambao ndiyo wamekuwa mabingwa wa kombe hili, ambalo limeshirikisha takriban mikoa yote ya Tanzania Bara. Nawapongeza sana vijana wangu wa Kinondoni, kwa kazi nzuri waliyoifanya na hii inaonesha ni jinsi gani Kinondoni inapiga hatua katika michezo na mambo mengine mbalimbali, ikiwemo Utawala Bora na Uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwapongeze Simba kwa kuchukua ubingwa wa Tanzania, lakini niwapongeze na Yanga kwa kuchukua nafasi ya pili. Nawapa hongera sana Yanga kwa kufungwa na Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Michezo ya Mwaka 1995 ni Sera nzuri sana, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua, siyo mzuri. Labda niseme kwa sababu haujatungiwa Sheria, lakini nafikiri Wizara sasa ihakikishe kwamba, Sera hii inatekelezwa kama ambavyo imeainishwa katika kitabu kile. Lakini hata suala la Sheria ya Michezo basi ni vyema nalo likafanyiwa uharaka ili liweze kupitishwa kuwe na Sheria hiyo ya Maendeleo ya Michezo ili tuweze kuondoa migogoro na kuhakikisha Taifa letu linafanya vizuri katika michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la michezo mashuleni. Naishukuru sana ama naipongeza sana Serikali kwa kuirudisha. Lakini niseme tu kwamba, hakuna kitu kinachofanyika kule shuleni. Serikali imesema michezo irudi shuleni, lakini kule kwenye shule za msingi na za sekondari hakuna maandalizi ya kutosha. Hatuna walimu ambao wamesomea, ama wana taaluma ya michezo. Kwa hiyo, niiombe Wizara hii ya Michezo, pamoja na Wizara ya Elimu, wajaribu kuangalia uwezekano kuwa na walimu ambao wanaelewa michezo ambayo watakuwa wanawafundisha vijana wetu pale. Hawawezi vijana wetu wakawa wanacheza mpira kwa maana ya kukimbizana tu kiwanjani. Ni lazima atokee mwalimu ambaye atakuwa anawaelekeza. Kwa hiyo, nafikiri ni vyema Serikali ikaliangalia hilo kwa umakini kwamba, mashuleni basi angalau walimu wawepo ambao wana taaluma ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nizungumzie michezo. Mchezo wa ngumi na mchezo wa *kick boxing* ni michezo ambayo imejitokeza hivi sasa inapendwa sana na kwa kweli imeweza kuiletea sifa nchi yetu katika kipindi kifupi sana, lakini sijui kama Wizara inafahamu hilo. Kwa sababu vyama vyenyewe vya michezo hii vinasajiliwa ama Wizara ya Mambo ya Ndani au kwenye Msajili wa Makampuni na siyo kwenye Vyama vya Michezo. Kwa hiyo, niiombe Wizara, ijaribu kuangalia ama kuvipitia vyama hivi kuhakikisha kwamba shughuli zao zinafanyika vizuri. Maandalizi ya mabondia wanaokwenda kupambana nayo yanakuwa mazuri ili waendelee kutuletea sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nichukue nafasi pia kumpongeza bingwa wa Afrika Mashiriki, ambaye ni juzi tu alichukua ubingwa wa uzito wa juu, ndugu yangu Awadhi Tamimu, baada ya kumpiga kwa *knock out* ya *round* ya kwanza Mkenya. Lakini pia nimpongeze bingwa wa *kick boxing* Tanzania, ambaye pia naye amekuwa ni bingwa wa mabara juzi juzi naye alimpiga Mkenya katika *round* ya kwanza kwa *knock out.* Kwa hiyo, inaonesha ni jinsi gani michezo hii inavyoiletea sifa nchi yetu. Kwa hiyo, niiombe Serikali ijaribu kuvitupia macho na kutoa msaada pale ambapo inahitajika ili michezo hii nayo iweze kupanda chati kama ilivyo kwa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa michezo hii niliyozungumza, sijui kama wanajua hata sheria zao kama wanazo, kwa sababu nilisema mwanzo kwamba, inasajiliwa kwenye Msajili wa Makampuni na kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani. Sasa sijui kama Wizara wanazo Kanuni ama sheria za michezo hii? Naomba Wizara ijaribu kuitupia macho sana michezo hii, kwa sababu tumekuwa na mabondia ama tumekuwa na vyama vingi vya kulipwa vya michezo hii, mara kwa mara utasikia mabondia wetu wanakwenda kupigana nje, lakini hatujui wamejiandaa vipi. Hatujui matayarisho yao yakoje! Sasa wanachukuliwa watu wanakwenda kupigana saa nyingine maandalizi siyo mazuri, anakwenda kupigwa kule mradi tu yule aliyempeleka amepata pesa. Naogopa na nina wasi wasi, isije siku moja ikaletwa maiti ya bondia aliyekwenda akiwa hakujiandaa vizuri ikawa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo suala la makocha hawa wa kigeni, ambao hivi sasa wamekuwa wakipenda sana kuja kufundisha mpira hapa Tanzania kwenye vilabu vyetu hivi. Kwanza, niipongeze Serikali kupitia Wizara hii kwa kufanya mchujo na kupata kocha mzuri sana wa Timu ya Taifa, pamoja na kocha mzuri sana wa Timu ya Vijana. Utaratibu uliotumika kuwapata makocha hawa, basi ungetumika pia kupata makocha kwa ajili ya hivi vilabu vyetu. Nina wasi wasi, makocha wanaokuja kufundisha vilabu vyetu sijui kama kweli wanao uwezo wa kufundisha vilabu hivyo, isiwe tu kwamba mradi kaja Mzungu anafundisha basi, hata kama uwezo wake ni mdogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Wizara ijaribu kushirikiana na vilabu hivi, kuwatafutia makocha ambao wana uwezo wa kufundisha michezo hii kuliko kujichukulia tu makocha ovyo ovyo, mradi tu pale kuna Mzungu anafundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie suala la haki miliki. Wenzangu wamelizungumza, lakini niseme kwamba, tunao vijana wengi Tanzania, tunalo tatizo kubwa sana la ajira. Vijana wamejitokeza wenyewe, wameweza kujiajiri kupitia sanaa mbalimbali, zikiwemo michezo ya kuigiza, muziki, kwa mfano, *Bongo Flavour.* Vijana wetu wanafanya vizuri sana. Niseme miziki hii ambayo wanapiga vijana wetu, inapendwa sana katika Ukanda huu wa Afrika ya Mashariki na Kati. Kila nchi unayokwenda katika nchi hizi utakuta muziki wa vijana hawa unapendwa sana, lakini vijana wenyewe ukiwakuta wako kwenye hali mbaya sana. Wananyonywa na wanadhulumiwa sana. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kupitia Wizara hii, tujaribu kuangalia uwezekano wa kuwasaidia hawa vijana wetu ili wasiendelee kunyonywa kwa kiasi cha namna hii. Inasikitisha sana kuona kanda iko dukani inauzwa shilingi 1,500, lakini yule kijana yeye anaambulia shilingi 100 ama 150 tu. Kwa kweli hiyo ni dhuluma iliyo wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Wizara na Serikali, wahakikishe kwamba, haki miliki inatekelezwa lakini kuhakikisha vijana wetu hawa wanapata stahili zao kama ambavyo wanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la muziki linajulikana. Wapo wanamuziki wengi sana duniani ni matajiri sana na katika Afrika pia, kwa ajili ya muziki huu lakini utakuta vijana wetu sisi wanaendelea kuwa maskini, wanaganga njaa, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya. Hii ni kwa sababu ya kudhulumiwa na baadhi ya watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali tuangalie jinsi gani tutawasaidia vijana wetu ili waweze kukwamuka kiuchumi. Serikali kupitia Wizara hii, iangalie basi hawa wanaosambaza kazi za vijana hawa, hata vile viwanda vyao wanavyotengenezea hizo *CD* na kanda viko wapi na wanapomwambia kijana kwamba tunatengeneza kopi 1,000 ama 10,000 ni kweli 10,000 ama wanamwambia kijana kopi 10,000 lakini wao wanatengeneza kopi 100,000. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwasaidie vijana wetu ili kwa kweli tuondokane na umaskini na vijana waweze kujiajiri na kufaidika na jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la Vyombo vya Habari na kwanza navipongeza sana vyombo vyetu vya Habari vyote, *Radio Tanzania,* TVT, *Star TV, Channel Ten, ITV* na *Redio One,* kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya ya kuelimisha wananchi wetu na kutoa habari mbalimbali kupitia vyombo hivyo. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. Natumia nafasi hii kuipongeza kwa pekee kabisa, *ITV* na *Redio One,* hasa pale ambapo waliwahamasisha Watanzania kuwachangia mama zetu ambao walikuwa na tatizo la kansa ya matiti au saratani ya matiti. Vituo hivi vimefanya kazi nzuri sana, hata ambaye alikuwa hajui suala la ugonjwa huo amefahamu na watu wengi wamechangia sana kuwasaidia mama zetu kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme ni kazi nzuri sana ambayo imefanywa na vituo hivi na kwa kweli vinastahili pongezi sana, kwa sababu wameweza kuokoa maisha ya Watanzania wengi ambao walikuwa hawana uwezo wa kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niendelee tena kuipongeza Wizara na niseme tu kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Zainab M. Vulu, nafikiri Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya anaweza kufikiwa.

**MHE. ZAINAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nami naomba niungane na wenzangu waliotangulia kusema, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, kwa hotuba yao nzuri waliyoitoa na kwa usimamizi mzuri wa Ilani ya Uchaguzi, ambayo inaambatana na Habari na Michezo na hasa katika michezo kwa sababu wameweza kusimamia suala la mpira, Watanzania tumetoka kwenye kuwa kichwa cha wendawazimu sasa tumekuja kwenye kuwapa raha Watanzania. Kwa kweli hilo nawapongeza. *(Makofi)*

Hali kadhalika, napenda nichukue nafasi hii kuvipongeza Vyombo vyote vya Habari kwa umahiri wao wa kuweza kutoa taarifa za habari wakati Mheshimiwa Rais, alipoamua kuwa mfano kwa nchi zote za Afrika, kwenda kupima virusi vya UKIMWI. Vyombo vya Habari vilikuwa mstari wa mbele, vilitoa taarifa, kila mtu alipata habari na tumeona jinsi gani Mheshimiwa Rais, ameweza kuhamasisha na jinsi gani tumeona umuhimu wa vyombo vya habari kwa jamii yetu ya Tanzania, watu bado wanaendelea kujitokeza kupima japokuwa katika mikoa ambayo wapo haijazinduliwa rasmi kampeni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, mcheza kwao hutunzwa. Naomba nichukue nafasi hii, niipongeze TUT kwa kazi nzuri inayoifanya na kwa juhudi zao wanazozionesha na hasa pongezi hizi zianze moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa TUT, Bwana Tido Mhando. *(Makofi)*

Napenda nami niungane na wenzangu katika kumpongeza Bwana Tido Mhando, yeye alikuwa anafanya kazi *BBC,* lakini aliona bora arudi nyumbani. Ni Watanzania wachache sana wenye moyo wa uzalendo na wenye kupenda kurudi nyumbani na kufanya kazi. Hii yote amekuja ili kutaka kuleta maendeleo na mageuzi katika vyombo vyetu vya habari. Kwa hiyo, napenda nimpongeze yeye pamoja na timu yake. Tumeona ni jinsi gani ameweza kuhamasisha na kuweza kuleta mabadiliko na kuna vipindi vya aina mbalimbali, ambavyo amevibuni na wananchi wengi wanavipenda. Kwa kweli anastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niipongeze tena TUT kwa kuweza kushinda katika Zabuni ya kuonesha mpira. Waswahili wanasema "kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza." Kwa hiyo, kuna kila sababu, Watanzania tujivunie chombo chetu cha televisheni ya Serikali, kama imeshinda basi ni wajibu wake na ni haki yao kama vyombo vingine, ambavyo vinatoa habari. Kwa kweli kwa hilo, mimi naipongeza sana TUT na naitakia kila la kheri na kwa kuwa TUT sasa hivi inaonekana hata nje ya mipaka ya Tanzania, kwa kweli tuna kila sababu ya kujivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna vyombo vingi vya habari na hivi vyombo vyote vimepewa leseni au vimepewa madaraka ya kutoa matangazo na Serikali, sasa wao wasiogope ushindani. Kama TUT imeamua kutoka kwenye ujamaa na kujitegemea, imeamua kuingia kwenye ushindani wa kibiashara, wakubali kupokea ushindani, wasije wakafanya mambo ya ngamia. Ngamia aliomba aingize pua, baadaye akataka kiwiliwili chote kiingie. Sasa hiyo haiwezekani, lazima vyombo binafsi vikubali kuingia ushindani na vikubali vinaposhindwa viwaachie wenzi wao walioonekana wanaweza na wanafaa, wakafanye hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina hakika TVT au TUT inaweza ikafanya hiyo kazi kwa umahiri kabisa na wananchi wakayaona hayo matangazo. Kule sisi Mkoa wa Pwani TVT tunaipata vizuri sana na wananchi wengi wamefurahi sana kusikia watauona mpira kwa kupitia TVT.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba hilo nalo waliangalie. Lakini mimi naomba niiulize Wizara; hivi hii Sheria itakuja lini? Naomba nipatiwe majibu na Mheshimiwa Waziri. Kuna Sheria Mpya ya Habari ni lini itatufikia hapa Bungeni? Hii Sheria itakapoletwa hapa Bungeni, huu utata wote utatoka. Kwa sababu huu ndiyo mwongozo wa vitu vyote. Itakapokuja Sheria hii ya Vyombo vya Habari, inawagusa Watanzania wote, kwani wana haki ya kupata habari. Si kwamba, Sheria hii inayokuja ya chombo kimoja cha habari au watu binafsi, wenye vyombo vya habari, hii sheria ni ya Wananchi wa Tanzania, ambao na wao wana haki na wanapaswa wapate habari zote zinazoletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapokuwa kimya, sheria inapokuwa bubu, ndiyo hao wenzetu wanatanua misuli. Sisi tunataka ushindani, wao waukubali. Wanalalamika kwamba vyombo vya Serikali ndiyo vipite vijijini, vikatoe taarifa za habari iwe za afya, siasa, mimi sielewi. Mheshimiwa Waziri, naomba hapa nipatiwe majibu. Hivi kweli hawa watu wamepewa leseni waoneshe *ikibindankoyi,* waoneshe

sinema za kutoka nje, badala ya kuwaelimisha Watanzania, badala ya kwenda vijijini na kuangalia Watanzania wameleta maendeleo gani, wana matatizo gani, watu wakahabarishwa, watu wakaelimishwa, watu wakaburudishwa na tamaduni zetu. Lakini sasa wao wamekazana kutuonesha sinema, wamekazana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde, Kiswahili kina maana nyingi.

**NAIBU SPIKA:** Kiswahili kina maana nyingi, wewe endelea tu, wala usiwasikilize. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ZAINAB M. VULU:** Asante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri, atakaposimama atuambie sheria hii italetwa lini na itakapoletwa itaondoa utata wote. Sote tuna wajibu wa kuwaelisha Watanzania, iwe vyombo binafsi, iwe vyombo vya Serikali, viende huko kwenye majimbo yetu, vikaone wananchi wetu wanachacharika vipi, wananchi wetu wana matatizo gani, wananchi wetu wanataka nini cha maendeleo. Je, dunia inasema nini ili watu wapate habari. Sio wao wakazane baada ya kutoa habari, watoe taarifa ambazo hazina maendeleo na kusema mzigo huu ni wa Serikali na wao vyombo hivi vinafaidika sana kwa sababu mpaka sasa hivi ninapozungumza hapa, kwa takwimu nilizokuwa nazo, sina uhakika kama ni sahihi, tuna vituo 15 vya Televisheni, tuna vituo 15 vya Redio na tuna majarida na magazeti yasiopungua 450. Hakuna nchi nyingine yoyote ya chini Kusini mwa Bara la Afrika, yenye idadi ya vyombo vya habari kama hivyo. Lakini je, wananchi wananufaika navyo au vinatumia nafasi hii kupoteza mwenendo na mwelekeo wa maadili ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ni hivyo, kama tunaona magazeti tunapiga kelele tu kila siku humu ndani. Hii ni bajeti yangu ya pili tangu niwe Mbunge na inapofikia Wizara hii, Wabunge wanasimama kukemea na kulalamika juu ya magazeti ambayo yanatoa picha za ngono, yanatoa picha ambazo zinapotosha maadili ya Watanzania, lakini sijaona hatua yoyote iliyochukuliwa. Sasa Mheshimiwa Waziri atakaposimama, atatusaidia kutufafanulia ni lipi ambalo anaona linastahili kufanywa na Serikali ina wajibu wa kukichukulia hatua chombo chochote kinachokwenda kinyume na maadili ya Watanzania na kupotosha wananchi badala ya kuelimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo, naomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie kunipatia ufafanuzi kama siyo majibu. Lakini bado tuangalie utata huu unatokana na nini au tatizo hili linatokana na nini?

Mwaka 1976, kilianzishwa chombo cha habari ambacho kilikuwa kinahariri karibu habari nyingi za hapa nchini, kilikuwa kinaitwa SHIHATA. Ilipofika mwaka 2000, SHIHATA ikawa marehemu. Kwa maana ya kwamba, ikafa. Sasa tuna Idara ya Habari. Mimi hapa sielewi, sijui kama kuna uwezekano kukaangaliwa kama hiyo Sheria bado, ni nini kinaweza kikafanyika aidha Idara ya Habari iimarishwe, iweze kufanya utaratibu wa kuangalia hivi Vyombo vya Habari au Idara ya Habari iwezeshwe katika vipengele ambavyo pengine imebanwa kwa sababu kuna Kitengo cha Habari ambacho kiko Ikulu. Sasa sijui kati ya chombo hiki cha Habari ambacho kiko Ikulu na Idara ya Habari; zinafanyaje kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani anamwangalia nani na nani anafanya nini? Naomba hili nalo nipatiwe ufafanuzi.

Kwa kuwa kengele ya kwanza imekwisha gonga, naomba niende kwenye hatua nyingine kuhusu Wizara hii hii ya Habari. Wizara ya Habari ina Waandishi wa Habari, ambao mara nyingi wanatumwa maeneo mbalimbali kwenye matukio mengine ya kutisha. Wizara ya Habari ilituma Waandishi wa Habari, wakati wa Vita vya Uganda vya Nduli Iddi Amini. Waandishi wa Habari walikwenda wengi kule, walituletea habari, wengine wamekufa, wengine wapo mpaka leo. Sijui hata kama siku za mashujaa wanakumbukwa na kuitwa au wamepewa tuzo zozote? Hata wale waliokufa, inawezekana hawakufa katika vita, lakini wapo waliokufa baada ya kurudi walipatwa na maradhi. Wizara imewachukuliaje hao, imewapa tuzo gani? Juzi tumeona siku ya mashujaa, je, imewakumbuka au tunakaa tu tunangoja Waandishi wa Habari waandike habari zetu, wasipoandika tunawalalamikia? Hili nalo nataka tuliangalie kwa umakini, kwa sababu vyombo vya habari ndiyo vinatusaidia kufanya kazi zetu. Vyombo vya Habari ndiyo vinatuwezesha kututolea elimu kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naib Spika, labda tu nikumbuke majina ya Waandiashi wa Habari, ambao kwenye kumbukumbu inaonekana na ninaowakumbuka inawezekana wapo wengine walishiriki kwenye Vita vya Uganda, kuna Juma Dihule, Ben Kiko na Marehemu Vincent Urio, inawezekana na wengine wapo basi Wizara itajua na ifikirie hilo itafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta nyingine ambayo nataka niigusie ni suala la michezo. Michezo ni kwa wote, michezo hii naomba ianzie kwenye Shule zetu za Msingi, ikibidi hata kwenye Kata zetu. Huko ndiyo tunaweza tukainua vipaji na vipaji tunavyotafuta basi Wizara isiangalie tu *under 17* kwenye *football* au chini ya miaka 17 kwenye mpira wa miguu. Kuna michezo ya aina nyingi, tunalalamika masuala ya watoto wetu kujiingiza kwenye ngono, hawana vitu vya kufanya huko wanakoishi. Hakuna michezo, hebu Wizara irudishe tena michezo mashuleni.

Watoto wakiwa na michezo wakirudi nyumbani wamechoka, hakuna atakayefikiria tena kwenda kutafuta mchezo mwingine ambao utamponza yeye apate mimba au apate magonjwa ya zinaa au apate maradhi mengine yoyote.

Hii itamfanya mtoto atakuwa na akili, atajenga mwili na pia sisi tutapata kuona ni wapi kuna watoto wenye vipaji tutawaibua kama wakimbiaji, tutawaibua wa netiboli, wa mipira wa miguu tutawaibua, hali kadhalika na michezo mingine ambayo naona kwamba inaweza ikapotea ni michezo yetu ya jadi. Hili nalo lazima tuliangalie na Wizara iweze kutusaidia tutainuaje michezo yetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine cha mwisho nimekikumbuka, naomba Wizara iangalie na ikiwezekana iongee na watu wenye vyombo vya habari, hasa wenye televisheni. Tunao watu wana *television stations* chungu nzima, wanaajiri watu wengi, wengine wanashindwa kuwalipa, lakini wanashindwa kuajiri mtu mmoja au wawili

wakawa wanaweza kuwasaidia kutoa ile elimu ya walemavu, kwa sababu tunao watu hawasikii na tuna watu ambao hawaoni.

Kwa wale wasiosikia, kukiwa na mtu ambaye yuko pale, wakati taarifa ya habari ikisomwa, yeye atakuwa anaeleza kwa vitendo, wenzetu tutakuwa hatuwaachi nyuma.

Naomba Wizara katika hili, wanapotoa leseni zao kwenye vyombo vya habari, waliangalie na wasikae tu wenye vyombo vya habari binafsi, wakaa wao kuandika habari za majungu tu kila siku, habari za uzushi. Wakae waandike habari ambazo zitaleta maendeleo Tanzania, zitawasaidia wananchi wa vijijini na hii itasaidia kuwajenga wao na hata Waandishi wa Habari wanaoandika hizo taarifa za habari ili waweze kuelimisha jamii badala ya kuleta utata na kuleta mgongano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kusema, TUT iendelee na ninaisifu sana na ninaipongeza sana kwa jitihada zake ilizofanya na Mwenyezi Mungu, amjalie kaka Tido Mhando, afanye kazi zake vizuri. TUT nayo itambe kwa sababu ndiyo TV tunayoitegemea nchini. Asanteni sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwe mchangiaji wa mwisho katika hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi zangu kwa Wizara kwa hotuba yao nzuri, yenye kuleta matumaini katika mustakabali wa kukuza habari zetu, utamaduni wetu na michezo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Vyombo vya Habari iwe TV, kwa maana ya televisheni ama kionea mbali, magazeti na redio, vina kazi kuu tatu; kuelimisha, kuburudisha na kutoa habari, hakuna kinyume cha hicho. Mtu yeyote wa habari, asiyejua kazi hizi tatu, yeye hafai kuendesha chombo cha habari. Ili uweze kufanya kazi hizi tatu, unahitaji mambo yafuatayo:-

Unahitaji elimu, vifaa bora vya kisasa, uongozi bora na ubunifu. Mimi nimetokea utangazaji, haya ninayoyasema ninayaelewa. Katika ubunifu hapa ndipo tunapopata hamu na bashasha ya kuipongeza TUT na Mkurugenzi wao Mkuu, Ndugu Dunstan Tido Mhando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Dunstan Tido Mhando namfahamu, nilipokuwa naingia Redio Tanzania yeye aliyenipokea akanifundisha kazi. Ni mbunifu kweli kweli na anapenda kazi ya utangazaji kuliko uhai wake na ndiyo maana ameweza kuyafanya yote haya. *(Makofi)*

Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumrudisha Dunstan Tido Mhando, nyumbani, Waingereza walikuwa bado wanamuhitaji na ndiyo maana walimpa kuendesha Idara ya Habari ya Kiswahili ya *BBC,* London na kurudi kwake tumeona matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote hapa mashahidi kabla Dunstan Tido Mhando kurudi, watazamaji wa televisheni ya TVT walikuwa wachache kweli kweli, kati ya nyumba kumi ni nyumba mbili tu ambao walikuwa wanaangalia TVT, iwe katika taarifa ya habari ama vipindi vyoyote vile, kwa sababu kama nilivyosema mwanzoni kulikuwa hakuna mtu mbunifu kama alivyokuwa Dunstan Tido Mhando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ninavyozungumza *graph* ama *chart* inaanza kupanda juu, watu wengi sasa hivi wanaangalia TVT kwa sababu ya mabadiliko yaliyofanyika. Leo amekwenda mbali zaidi amepata zabuni ya kutangaza ligi ya Uingereza ya kutangaza mpira wa miguu kati ya Tanzania na Mozambique, jamani haya mambo hayakuwepo huko nyuma na juzi nilikuwa nasoma katika gazeti kwamba kitengo chao hicho TUT tayari imeshapata *order* ya matangazo yanayofikia kiasi cha shilingi milioni 895 kama sikosei, haijapata kutokea, haijawahi kutokea na ndiyo kwanza inatokea katika kipindi hiki ambacho Tido ni kiongozi wa TUT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa hapa kwamba TUT itafika mahali ianze kujitegemea yenyewe na kwa kufanya hivi maana yake itasimamia kila kitu na maana nyingine itaisaidia Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mapato kama inavyofanyika katika idara nyingine katika utaratibu wa *ventetion scheme*. Kwa hiyo, si kweli hata kidogo kwamba eti wao wanapata pesa za kodi ndiyo iwe basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napiga mahesabu hapa ya haraka haraka shilingi milioni 895 hazitapelekwa tena TUT, baadaye zitabaki Serikalini, zikibaki Serikali zitaweza kujenga madarasa 127. Madarasa haya yatawachukua wanafunzi 5,615 kazi hiyo iliyofanywa na TUT kwa hiyo, kusema kwamba wanapewa kodi halafu wanashusha bei wataharibu vyombo binafsi si kweli hata kidogo, wote hapa tunaangalia *BBC* ni chombo cha Serikali cha Waingereza. Kina vipindi vizuri, kina matangazo mazuri mengine tunayoyafanya sisi kwa sababu *BBC* wanatoa matangazo ya kibiashara. Haitatokea hata siku moja Mwingereza aipige vita *BBC* hata kama Mwingereza huyo atakuwa na *TV Station* yake ama *Radio Station* yake, hapa wanalinda uzalendo wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo cha habari ni ulinzi katika nchi, kwa wale vijana mwaka 1978 Baba wa Taifa alitangaza vita dhidi ya Nduli Idd Amini wa Uganda, wakati ule kulikuwa na *radio station* moja tu, Redio Tanzania. Alipotangaza pale *Diamond Jubilee*, watu wote tulipata habari kwa mara moja kwa sababu hakukuwa na njia nyingine tena ya kusikiliza isipokuwa Redio Tanzania. Leo kuna vyombo vingi vya habari, kuna uwezekano mkubwa kwamba inaweza yakatangazwa mambo muhimu wengine wasisikie. Lakini kwa sababu chombo chetu cha TVT na Redio Tanzania kinaboreka, wengi watabaki katika vyombo hivyo. Kwa hiyo, kama Serikali itatangaza mambo yake hata kama ni *breaking news* watu wote wa Tanzania watasikia kwa mara moja na wataweza kubaki hapo kwa sababu vipindi vya TVT na Redio Tanzania sasa vinaboreka, nawaombeni sana Watanzania, malumbano haya tuyaache kwa nia njema tu, tuingie katika ushindani mzuri, kinachojieleza hapo ni kwamba vyombo vingine vya habari

vimtafute Dunstan Tido Mhando mwingine ili na wao waweze kuingia katika ushindani huu katika kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, nina hakika wenzetu wametuelewa na wametusikia naomba TUT chini ya uongozi wa Dunstan Tido Mhando, msikate tamaa endeleeni kuyafanya hayo makubwa zaidi na sisi tuko nyuma yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hapo zamani tulikuwa na *press attach* katika Balozi zetu huko nje, na *press attach* hizi zilikuwa zinasaidia sana na ziliweza kutoa maelezo yanayohusu nchi yetu. Naomba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, turudishe utaratibu huu unasaidia sana kwa sababu juzi hapa tulikuwa na matatizo ya ile sinema ya Mwanza, ile ingeweza kabisa ikajibiwa huko huko nje kama tungekuwa na *press attach*, tungeongeza nguvu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba pamoja na uhaba wa pesa tuliokuwa nao, lakini naomba suala hili tulitazame kwa mara nyingine tena ili tuweze kurudisha *press attach* hasa katika Balozi zile ambazo tunaona zitatusaidia katika kuchangia uchumi na tunaziona kwamba zinaweza zikachafua jina letu katika baadhi ya maeneo fulani fulani ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, hapa yamezungumzwa mambo ya uandishi wa habari, mimi naomba sana waandishi wa habari wenzangu wawe na baraza lao wao wenyewe. *MOAT* ni chombo cha habari cha wamiliki, sio chao, waanzishe Baraza lao ili waweze kulinda taaluma yao hii waweze kutetea maslahi yao. Kama walivyosema wenzangu hapa kuna wengine wameingia kuwa waandishi wa habari si waandishi wa habari hata kidogo, hawakupata mafunzo mahali popote, lakini kwa sababu hakuna chombo cha kusimamia na kukemea wao wenyewe hawa wanajitokeza kila siku, wanaomba radhi kila siku wanaandika mambo ya ajabu ajabu kila siku katika vyombo habari. Basi nawaomba ndugu zangu mimi ni mwandishi mwenzenu hapa tuanzishe chombo chetu cha waandishi wa habari sio *MOAT, MOAT* sio chombo chao kile, kile ni chombo cha matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua kengele ya kwanza imeshapiga, nisingependa nigongewe nyingine tena, lakini narudia tena kuipongeza TUT isirudi nyuma, ikaze uzi huo huo ili TVT iendelee kuwa chombo imara madhubuti katika nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale niliosema watachangia mchana huu wamechangia na bahati nzuri tuna Naibu Mawaziri wawili kwa hiyo, hatuwezi kuongeza idadi ya Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa zamu aje, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nianze

moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Lakini kabla sijatoa ufafanuzi wa majibu na baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba na mimi nitoe pole kwa wote waliopata misiba na nitoe pole pia kwa Mheshimiwa Spika, kwa msiba wa Mzee Chifu Abdallah Fundikira. Mzee Chifu Abdallah Fundikira namfahamu, nilifanya naye kazi miaka ya 1990 wakati wa kuanzisha mchakato wa kuanzisha vyama vingi vya siasa na nilibahatika kusafiri naye nje ya nchi yetu kwa hiyo, namfahamu sana yule mzee na Mungu amrehemu. Lakini pia nimpe pole Mheshimiwa John Magufuli, kwa kufiwa na baba yake mzazi, tunaomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na uvumilivu katika kipindi hiki. *Amin.*

Naomba nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri na kunihamishia katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo, namshukuru sana kwa imani yake kwangu. *(Makofi)*

Vile vile naomba niwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi walionipokea katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo, walinipokea kwa heshima na wanaendelea kunipa ushirikiano mkubwa sana nawashukuru sana. Aidha, kwa namna ya pekee naishukuru sana familia yangu na hasa mke wangu Midlasta na watoto wetu kwa uvumilivu wao kwangu. *(Makofi)*

Naomba pia niwashukuru sana wananchi na wapiga kura wa Jimbo langu la Kasulu Mashariki kwa ushirikiano wanaonipa na mimi nawahakikishia kwamba nitaendelea kuwa kiongozi mtumishi na nitafanyakazi bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi naomba nitoe majibu na ufafanuzi wa baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilikuwa nyingi na wachangiaji walikuwa wengi na kama atakavyoeleza baadaye Mheshimiwa Waziri hoja nyingi zitajibiwa kwa maandishi kwa utaratibu ule ule. Hapa tunafanya mapitio ya zile chache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Mheshimiwa Ali Said Salim, yeye alijielekeza kwenye kitu chetu cha hotuba akasema kwamba kiwango kilichotajwa kukusanywa na Wizara ni kidogo mno na maoni yake anasema anaomba Waziri ampe maelezo ni kwa nini kiwango hiki ni kidogo? Sasa ufafanuzi ni kwamba Mheshimiwa Ali Said Salim, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara itakusanya jumla ya shilingi milioni 229 katika vyanzo vilivyoidhinishwa na Serikali, hili ni ongezeko la takribani asilimia 130 ukilinganisha na lengo la shilingi milioni 98 tu zilizoidhinishwa kwa mwaka 2006/2007. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ali Said Salim nilikuwa naomba usome vizuri jedwali letu linaloonyesha makusanyo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Capt. John Komba, kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, alitoa ushauri akishauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa mwaka 2008/2009 kwa ajili ya TUT, ushauri wake bila shaka ni mzuri na umezingatiwa na mwaka ujao wa fedha *Inshallah* hali ya fedha Serikali inaweza ikawa nzuri. Vile vile

Mheshimiwa Capt. John Komba aliuliza TUT itafute wabia kama *NSSF* ili kumalizia ujenzi wa ofisi zake kule Mikocheni Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tayari majadiliano yanaendelea kati yaTaasisi ya Utangazaji ya Taifa (TUT) na shirika la wenzetu wa *NSSF. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika Mheshimiwa Capt. John Komba kwa niaba ya Kamati alitaka kujua tovuti ifanye kazi mapema. Hii ni tovuti ambayo imeanzishwa kama mkakati wa kupokea maoni ya wananchi moja kwa moja na niseme tu kwamba kupitia Bunge hili kwamba tovuti ya Taifa tayari imeanzishwa na imeanza kazi tarehe 1 Julai, 2007. Tayari maoni mbalimbali toka kwa wananchi wetu yameanza kupokelewa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi kutoka Kilwa alisema waandishi wengi takriban asilimia 70 hawana ajira za kudumu na malipo yao ni kidogo sana. Tunasema yote hayo yatazingatiwa katika mchakato wa sheria mpya ya habari itakayoletwa Bungeni mwezi Novemba, 2007.*(Makofi)*

Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa alizungumzia kuhusu matangazo ya biashara na mgogoro uliopo kati ya TUT na *MOAT*, suala la kisera Mheshimiwa Waziri atakuja kulitolea ufafanuzi wa kina ili tuweze kuelewana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum alitoa hoja kwamba mitambo ya utangazaji ya TUT isambazwe nchi nzima. Napenda kumweleza Mheshimiwa Magdalena Sakaya kuwa ni azma ya Serikali na mpango umeanza kwa mwaka huu wa fedha mitambo itawekwa katika mikoa kumi kama hatua endelevu kuelekea katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alizungumza maswali mengi ya kisera, Mheshimiwa Waziri atakuja kuyafanyia ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir ametoa ushauri kwamba Wizara na Serikali iwe macho na uandishi mbaya na uandishi usiozingatia maadili, kwa kweli ushauri huu ni mzuri umezingatiwa. Lakini nimkumbushe tu kwamba imekuwa kawaida ya Wizara yetu kila mara kufuatilia mwenendo wa vyombo vyake vya habari na kila mara maandishi ambayo hayazingatii maadili yamekemewa yameonywa na baadhi ya vyombo vingine vimefikia hata kufungiwa. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, amezungumza kuhusu mambo mengi kuhusu vyombo vya habari akisema Serikali iwape mafunzo waandishi ili waweze kuwajibika zaidi, hilo nalo limezingatiwa. Lakini naye pia naomba afahamu kwamba waandishi wengi wa habari wameajiriwa katika sekta binafsi na kwa kweli majukumu ya sekta hizo ni kuendesha mafunzo hayo. Lakini hata hivyo sheria mpya ya habari ambayo inakuja itazingatia yote haya.

Pia Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, alizungumzia Serikali iweke tena utaratibu wa *mobile cinema* kwa ajili ya mafunzo vijijini kama kilimo, afya, ufugaji na kadhalika. Niseme tu kwamba Wizara yetu kwa sasa haina mpango wa kuanzisha *mobile cinema* lakini Wizara nyingine kama vile Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wamekuwa wakifanya namna hiyo na bila shaka Wizara zingine zinaweza zikaendelea kufanya hivyo, lakini sisi wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa sasa hatuna mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa George Lubeleje, alizungumzia shida ya usikivu wa *RTD* na TVT na kushauri kwamba ni vema hivi vingesikika nchi nzima kwa kweli ni mkakati wa Wizara kufanya *RTD* na TVT isikike nchi nzima. Kama nilivyosema tayari mkakati umeanza mwaka huu wa fedha tutafika katika mikoa kumi ambayo kwa hakika Mikoa hii itakuwa na usikivu ambao ni mzuri sana.

Halafu Mheshimiwa Susan Lyimo Mbunge wa CHADEMA, Viti Maalum amezungumzia umuhimu wa habari kutolewa bure kwa kuwa ni haki ya msingi ya Kikatiba na sisi tunakubaliana na yeye kwamba ni kweli, kwa kuwa ni haki ya msingi ya Kikataba na sisi tunakubaliana na yeye kwamba ni kweli Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 18 imetamka haki hiyo na wala haki hiyo haibishaniwi. Lakini Mheshimiwa Susan Lyimo pia amezungumzia juu ya TUT isifanye biashara, Mheshimiwa Waziri atalizungumza hilo kwa sababu ni la kisera pia. Lakini Mheshimiwa Susan Lyimo amezungumzia Serikali inakaa kimya wakati vyombo vya habari vinapokashifu na kudhalilisha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, siku zote iko macho na zipo njia mbili, akikashifiwa na chombo cha habari hakuridhika anaweza kwenda mahakamani na watu wengi wamekwenda mahakamani mnafahamu lakini sisi pia kama Serikali tuna utaratibu wetu kila mara kuvikumbusha vyombo vya habari kuzingatia maadili yake na vyombo vingine mbalimbali ambavyo vimeonywa na vingine hata kufungiwa. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Felix Kijiko, amezungumzia mitambo ya Redio Tanzania, Kigoma ni mibovu. Mheshimiwa Felix Kijiko, ni kweli mitambo hiyo ni mibovu na ni ya zamani lakini Mheshimiwa Felix Kijiko wewe poa tu, mwaka huu TUT inafunga mitambo mipya kule Kigoma na Mikoa ya jirani kutakuwa na usikivu ambao unafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Esther Nyawazwa, amezungumzia Serikali kudhibiti vyombo vya habari kwa sababu vinajiingiza kwenye uchochezi. Ushauri huu umezingatiwa na kwa kweli sheria mpya ya habari inayokuja itatoa majibu mbalimbali kwa matatizo mengi katika sekta hii ya habari. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya, amezungumzia juu ya mgogoro kati ya *Mbeya City FM* na *Generation FM* juu ya mgogoro wa matumizi ya masafa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Benson Mpesya wewe mwenyewe anafahamu kwamba tarehe 15 Juni, 2007 ujumbe wa *TCRA* au Tume ya Mawasiliano ifika Mbeya na kufanya mazungumzo kati ya *Mbeya City FM* na *Generation FM* na uamuzi Mheshimiwa Benson

Mpesya unakumbuka ulikuwa ni *Mbeya City FM* watumie masafa ya *MH 100* na *Generation FM* watumie masafa ya *FM MH 97.2* na Mheshimiwa Benson Mpesya kama mgogoro unaendelea baada ya maelekezo na hukumu ya Tume ya Mawasiliano basi tuwasiliane kama lipo jambo tuweze kulifuatilia kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ametoa hoja kwamba Wilaya ya Kilindi ina utajiri mkubwa wa utamaduni na vionjo vya asili lakini haina Afisa Michezo wala Afisa Utamaduni, Serikali inasema nini juu ya jambo hili?

Kwanza Mheshimiwa Beatrice Shellukindo tunakushukuru sana kwa kutambua utajiri na vionjo hivyo vya utamaduni kule Kilindi na ombi hili tumelipokea na sisi Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na wenzetu wa TAMISEMI tutashirikiana pamoja kuhakikisha kwamba anapatika Afisa Utamaduni katika Wilaya yako ya Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu ametoa hoja nzito kwa nini Serikali inashindwa kutoa maamuzi ya kufanya Kiswahili kuwa lugha ya masomo kutoka ngazi ya awali. Mheshimiwa Dr. Slaa, hoja hii ni hoja ya msingi na hoja hii inajadiliwa karibu nchi nzima. Lakini nikubaliane na wewe tu Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba sera yetu ya mwaka 1997 kifungu cha tatu kinaeleza mkakati huo wa kutumia Kiswahili katika ngazi zote za mafunzo kuanzia chekechea hadi Chuo Kikuu. Lakini basi kwa sababu jambo lenyewe ni gumu kidogo na wala haligusi Wizara yetu peke yetu, jambo hili tunalifanyia maandalizi ya kutosha ikiwa ni pamoja na kuandaa vitabu ili hatimaye kuandaa kamusi, kuandaa maneno sanifu yatakayotumika katika maneno ya sayansi na kadhalika ili hatimaye mchakato huu uweze kuendelea. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Dr. Slaa, niseme tu ni nia ya Serikali hatimaye kutumia Kiswahili kuanzia chekechea hadi katika elimu ya juu, ndiyo mtazamo wetu na ndiyo mkakati wetu endelevu. Pia Mheshimiwa Dr. Slaa amejikita katika Kiswahili na ameulizia kuna mpango gani wa Kitaifa wa makusudi wa kukuza Kiswahili ikizingatiwa kwamba ni lugha mojawapo rasmi katika *AU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Kiswahili ni lugha mojawapo ya Umoja wa Afrika, Kiswahili kinatumika katika Bunge la Afrika na Kiswahili sasa kimeridhiwa katika *SADC* na sasa pia kinatumika rasmi katika *East African Community*. Kwa hiyo, niseme tu Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba mkakati uliopo wa Wizara ni kuandaa wakalimani wa kutosha, kuanda wafadhili wa kutosha na kuandaa vifaa vya kutosha kama vile kamusi, msamiati na marejeo mbalimbali ya lugha na mkakati huu katika kitabu chetu cha maendeleo utaona kwamba tayari tumetenga fedha kupitia Baraza letu la BAKITA ili kuweza kuandaa wakalimani na wafasili wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Mbunge wa Jimbo la Donge, ametoa maelezo ambayo nakubaliana nayo kwamba utamaduni wa Taifa lolote utambuliwe kwa mambo muhimu kama nguo na mavazi ya wananchi, lugha, ngoma na hata vyakula hivyo nakubaliana na yeye na tafsiri yake hiyo na sisi katika tafsiri pana ya utamaduni tunathamini kwamba utamaduni ni uasilia wetu lakini pia katika tafsiri hiyo nguo,

mavazi, lugha na ngoma ni vielelezo tosha kabisa kwa utamaduni wa Taifa lolote na hilo tunakubaliana na yeye Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, anasema wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu kulijitokeza mchakato wa kutafuta vazi la Taifa, sasa analiza je, mchakato huu umeishia wapi? Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, mchakato huu unaendelea vizuri na sisi katika ngazi ya Wizara tumeshabainisha mavazi matatu ambayo tunafikiri ni rasmi, lakini kwa utaratibu wa Serikali kama hufahamu Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, tumeafiki tayari matayarisho ya waraka wa Baraza la Mawaziri yameandaliwa ili tuweze kuwa na uamuzi wa pamoja kama Serikali kwa kusema sasa hili ndilo vazi la Taifa kwa sababu kuna mambo mengi ya kuangalia katika uchaguzi ule, Baraza la Mawaziri hatimaye litatoa uamuzi wa vazi la Taifa, lakini mchakato unaendelea vizuri na umefika mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda bado amekumbuka wapiga kura wake, je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kumwezesha Afisa Utamaduni Wilaya ya Chunya kupewa pikipiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo jema hili na tutalifikisha kwa wenzetu wa TAMISEMI waweze kulifanyia kazi. Lakini Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, akumbuke tu kwamba maafisa utamaduni hawa wengi wako chini ya Halmashauri zile, kwa hiyo, Halmashauri ya Chunya pia inaweza ikawekwa kwenye Bajeti yenu mnaweza mkaweka pikipiki, pikipiki sio gharama kubwa ili afisa utamaduni pale kwenu aweze kupita kupita vijijini. Lakini jambo hili ni jambo jema sana, wewe na sisi tusaidie na wenzetu wa TAMISEMI hatimaye tuone tunaweza tukafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, wao wameonesha hofu kubwa waliyonayo namna gani maadili ya Taifa yanavyomomonyoka na wala hawaoni kama kuna hatua madhubuti zinazofanyika na wamebainisha kwamba Tanzania sio kisiwa tunaishi katika dunia ya utandawazi. *(Makofi)*

Lakini wameweka angalizo muhimu sana kwamba Tanzania isiwe dodoki la utamaduni wa kigeni, hoja hii naiafiki kabisa, ni kweli upo umuhimu wa kulinda maadili yetu. Lakini Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maadili kwa kweli linaanzia kwenye ngazi ya familia, haliwezi kuanzia juu sana, lazima lianzie kwenye ngazi ya familia na hakika vijana wetu katika ngazi za familia, katika ngazi za shule kwa kweli hawana budi kufundishwa maadili mema ya Taifa yetu. Lakini ni kweli Mheshimiwa Said Arfi, Tanzania hatuwezi kukubali likawa dodoki la kuchukua kila kitu, hatuwezi kukubaliana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga, anauliza hivi ile Bodi ya Filamu bado iko au ilishakufa? Mheshimiwa Paul Kimiti hiyo bodi ipo tena ipo kweli kweli, isipokuwa tu ile sheria yake iliyoianzisha Sheria Na. 4 ya mwaka 1976 ni kweli ni sheria ambayo imepitwa na wakati na sasa hivi pale Wizarani tumeshaanza mchakato wa kuiangalia upya sheria ile kwa sababu kwa kweli haifanani na mazingira ya sasa. Hali

kadhalika sheria ya michezo ya kuigiza hali kadhalika inaangaliwa kwa mujibu wa sheria hii ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, anauliza ni mkakati gani wa kukitumia Kiswahili katika shughuli mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa, niseme tu kwamba lugha hii sasa inatumika katika vyombo vyote *AU*, *SADC*, Bunge la Afrika, *East African Community* hata juzi tulipokuwa kwenye Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki mwezi wa nne zilitumika lugha zote mbili lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kweli Kiswahili kinatumika na labda angalizo la muhimu tu ni kwamba katika Kikao cha *AU* kilichofanyika Januari, 2006 Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika hotuba yake aliyoitoa kule Khartoum, Sudan alitumia lugha ya Kiswahili na lugha ile ilivutia watu wengi sana na mwenyewe Mheshimiwa Rais ni mpenzi na mdau sana wa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa alizungumzia maslahi ya wasanii dhidi ya matajiri wanaowaibia wasanii wetu, niseme tu kwamba Serikali imeliona jambo hili na Sheria Namba Saba ya mwaka 1999 ya Hati miliki na hati shiriki imelizingatia jambo hili. Lakini nitoe wito kwa wasanii wenyewe watambue kwamba zipo sheria mahususi zinazowalinda na chombo chao kinachowalinda ni Baraza la Sanaa la Taifa pamoja na wenzetu wa *COSOTA,* kwa hiyo, na wao pia wachangamkie fursa hizo.

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Ali Said Salim na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, wote wamezungumzia mavazi yasiyokuwa ya heshima ikiwemo nguo fupi, vichupi kwa warembo wetu na kadhalika. Maelezo yake ni kwamba Serikali inalitambua sana jambo hilo na kwa kweli kuna maelekezo ya Serikali kwamba wananchi na wasanii wanaelekezwa kuvaa nguo za heshima zinazostahili maungo yao na kama ni wasanii pia wanahimizwa kutilia mkazo nguo zinazoleta heshima wanapokuwa kwenye majukwaa yao ya sanaa na kupitia Baraza letu la Sanaa tumetoa maelekezo ya kupiga marufuku kwa kweli nguo ambazo hazina heshima wala staha kwenye majukwaa kama vile nguo fupi sana na nguo za mipasuo ambazo zinakiuka maadili yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Ame Pandu Ame na Mheshimiwa Godfrey Zambi wamezungumzia umuhimu wa kutukuza na kufufua vikundi vya ngoma zetu za asili, tunakubaliana na nyie na kwa kweli hapa hoja ni kuviendeleza na kuviimarisha, kwa kweli suala hili tunalifanya Wizarani, pale kwenye Wizara yetu kuna kitengo maalumu kinachoshughulikia masuala haya lakini pia tunashirikiana kwa karibu na wenzetu wa Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Capt. John Komba, katika mchango wako wa maandishi umekumbusha Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo kitengewe Bajeti ya kutosha, hoja imezingatiwa lakini niseme tu kwa sasa Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo sasa kinakuwa wakala, kina *agency,* kwa hiyo, kitakuwa na wigo mpana zaidi wa kutafuta fedha zake. *(Makofi)*

Kuhusu ruzuku ya BAKITA hiyo nayo imezingatiwa, hoja zilikuwa ni nyingi Mheshimiwa Juma Njwayo, Mbunge wa Tandahimba alizungumzia Bodi ya Filamu, Serikali iboresha Baraza lya Kiswahili la Taifa na kulipa jengo na vifaa vinavyostahili. Mchakato huu wa kupata jengo la BAKITA unaendelea na kwenye Bajeti yetu ya Maendeleo tumetenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la Baraza la Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi sana lakini kama nilivyosema mwanzo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya na kuniwezesha kutekeleza majukumu mbalimbali ya kutumikia wananchi katika kulijenga Taifa na kuendeleza Taifa letu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kwa dhati ya moyo kumpongeza Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wangu wa Wizara kwa kunilea na kunifundisha kazi hasa ukizingatia uzoefu wake mkubwa na kuwa katika Baraza la Mawaziri kwa muda mrefu, hakika yeye ni hazina kubwa na nimechota maarifa na uzoefu mkubwa kwake. *(Makofi)*

Pia napenda kumshukuru Naibu Waziri mwenzangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kwa ushirikiano mzuri ambao tunao Wizarani, pia napenda nimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara, mama Kijakazi Mtengwa, Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Taasisi, wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao mzuri ambao wanauonyesha katika kusaidia kutimiza majukumu yetu katika Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee ninawapongeza na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Korogwe Mjini, kwa imani yao kwangu ya kuendelea kuniunga mkono katika kuleta maendeleo ya dhati katika Wilaya ya Korogwe hasa ukizingatia kwamba hiki ni kipindi cha tatu wamenipa kura na kuniamini, ninawahakikishia utendaji mwema katika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima ya pekee naomba nimshukuru mke wangu Florah na familia yangu kwa jinsi wanavyonisaidia na kunipa moyo katika kutekeleza majukumu ya wananchi na naomba muendelee kunivumilia na kuniombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa. Marehemu Amina Chifupa kwa sisi wanamichezo tunaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa wa kuhamasisha maendeleo ya michezo. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa nia yake

nzuri ya kutaka kuendeleza michezo hapa nchini bila shaka kutokana na jitihada hizo za Mheshimiwa Rais kiwango cha michezo hapa nchini kinaendelea kupanda na kuleta changamoto kubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutoa pongezi kwa wadhamini wote wa michezo nchini hasa *Serengeti Breweries* kwa umahiri wao mkubwa wanaoutoa katika kuihudumia Timu yetu ya Taifa. Aidha, pia napenda kupongeza vyombo vingine vyote ambavyo vimetusadia lakini naomba nirudie kwamba Serengeti kwa kuhamasika wameongeza mkataba kwa kuihudumia Timu ya Taifa mpaka mwaka 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu pia nazitoa kwa waandishi wa habari hasa magazeti, redio na televisheni kwa jinsi wanavyosaidia kuelimisha jamii kutumia vyombo vya habari katika kuhamasisha maendeleo ya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kutoa pongezi hizo naomba kabla sijaendelea kujibu hoja za Wabunge kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye hoja ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi na napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge michango ilikuwa mizuri sana kuanzia kwenye Kamati yetu na hata katika Kambi ya Upinzani wametusaidia sana kutoa changamoto na kutusaidia katika suala zima la jinsi gani tutaendeleza michezo katika nchi yetu. Kijumla ni kwamba yapo mambo 11 na ningependa niyazungumze ili kutokana na muda angalau tuweze kufahamu ni mambo gani. *(Makofi)*

La kwanza ambalo limezungumzwa sana ni kuboresha viwanja Wilayani na Mikoani hilo tumelichukua, la pili ni ujenzi wa viwanja katika miji mikubwa hasa Kikanda na wametamka katika baadhi kila Kanda kuwa na Uwanja wa Kimataifa, la tatu kubwa ni viwanja vya michezo vinavyoporwa au vinavyobadilishwa kiwanja cha michezo lakini kinabadilishwa kufanyiwa shughuli nyingine labda baa inajengwa au wanafanya vitu vingine, la nne ni viwanja viwe vya Serikali badala ya viwanja kuwa vya Chama cha Mapinduzi hilo limezungumzwa na wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano kubwa ni kuendeleza michezo mbalimbali badala ya mchezo wa mpira peke yake, hilo nalo limezungumzwa sana, la sita kuendeleza michezo vijijini, wilayani, mikoani kwa kupitia Halmashauri zetu na katika Serikali za Mitaa, la saba wazo zuri limetolewa kwamba badala ya kutegemea Serikali peke yake basi kuwe na mfuko maalumu wa kuendeleza michezo nchini, hilo ni suala zuri sana, lingine ambalo limezungumzwa karibu na Waheshimiwa Wabunge wote ni saula zima la michezo shuleni kwamba lirudishwe kwa sababu bila kufanya hivyo michezo haitaendelea katika nchi yetu. Pia yapo mambo mengine ya moja moja mfano jina la uwanja mpya liwe nini? Na *parade* isichezwe katika kiwanja kipya halafu na mechi ya Msumbiji ichezwe katika uwanja mpya, pia limechangiwa lingine la jumla la sera ya maendeleo ya michezo nchini uhuwishwe, iliyopo imepitwa na wakati, pia lingine ni kuhusu mafunzo ya makocha, waamuzi, madaktari wa michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo la mtu binafsi kabisa hili la Mhehsimiwa Said Amour Arfi ambalo Bendera ya Taifa haiko katika mashindano ya *Tusker* yanayochezwa Mwanza, nataka hili nilijibu moja kwa moja, ipo na nimepiga simu hata sasa hivi inapepea mpaka tunaingia humu ndani kwa hiyo, hilo tumeweza kulitatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la 11 ni michezo ya walemavu na maandalizi ya *Special Olympic* kule China mwezi Septemba, 2007. *(Makofi)*

Sasa baada ya kuzungumza haya yote naomba sasa nipitie hizi hoja za Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja kutokana na muda ambao nimepewa, naomba nianze na Kamati yetu, Kamati yetu imewasilishwa na Mheshimiwa Capt. John Komba, yeye amezungumzia la kijumla kwamba Serikali iwe na mpango madhubuti wa kuendeleza michezo, nataka nimhakikishie kwamba Serikali tupo imara, tuna mkakati maalumu na kufuata sera yetu ya kuhakikisha kwamba tunaendeleza michezo katika nchi yetu kwa kupanga mikakati kuanzia kijijini mpaka Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani amezungumzia Wizara haina makazi ya kuaminika na yaliyopo yamechakaa ni vyema Wizara ikatafuta makazi ya kuaminika katika jengo moja ili idara zote ziwekwe katika jengo hilo, Wizara ina makazi ya kuaminika yapo jengo la *Holland House,* mtaa wa Samora. Aidha, Wizara inafanya mawasiliano na *National Housing* ili kupata jengo moja ambalo Wizara inaweza kuwa hapo kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo amezungumza Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi ni Ofisi ya Wizara haikidhi mahitaji, hilo nimeshalijibu, dira ya michezo haikidhi mahitaji, jitihada zinafanywa kwa ajili ya kuboresha taratibu zote za kuendesha michezo. Viwanja vya michezo vya Serikali kujengwa kila Kanda, hilo nimeshalizungumza na limezungumzwa na Wabunge wengi, ushauri tunaupokea, uwezo ukiwepo tutajitahidi, sasa hivi kama mnavyofahamu tunajenga uwanja changamani pale Dar es Salaam, ni gharama kubwa ule uliopo pale sasa hivi shilingi bilioni 58 na sasa hivi tunahangaika tuweze kupata awamu ya pili ambayo ni muhimu kujengwa nayo inahitaji shilingi bilioni 62. Kwa hiyo, unaona bado tuko katika kuujenga Uwanja wa Taifa, uwezo wa Serikali ukiwepo tutaendelea kujenga viwanja vingine katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Pia ofisi za vituo vya michezo zina hali mbaya, ofisi zinaendelea kufanyiwa ukarabati na kuwekewa mazingira mazuri hasa ofisi ya Songea na Arusha ili ziweze kutoa huduma zinazostahili. Viwanja vya CCM virudishwe Serikalini, hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, limezungumziwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Susan Lyimo na wengine wengi hasa Wapinzani. *(Makofi)*

Nataka nijibu kama ifuatavyo, hilo ni suala ambalo wote mnalifahamu nimekuwa nikilijibu katika maswali yangu kila wakati, nataka niseme ni vizuri mkafahamu kwamba viwanja vyote ambavyo vinamilikiwa na CCM ni mali yao, walihamasisha wananchi wakajenga viwanja hivyo na ndio ambao wana hati miliki na hata ukienda kwa Waziri wa

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yeye ndio ambaye anashughulika na masuala haya ni kwamba viwanja vile vina hati miliki za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba michezo ilirudishwe shuleni, hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kama nilivyosema ni kwamba utaratibu uliopo sasa hivi ni kwamba tayari mchakato wa kurudisha michezo shuleni unaendelea sasa hivi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara yetu wanaandaa mkakati mzuri wa kuandika waraka ambao utapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri kuhakikisha kwamba suala la michezo mashuleni, sekondari na vyuo sasa linakuwa la kudumu kwa kuwa na utaratibu ambao ni maalumu na linaendelea na hivi karibuni litaanza.

Mheshimiwa Grace Kiwelu ametoa pongezi kwa Rais kwa jinsi anavyohamasisha michezo tunashukuru, tatizo la viongozi wa vilabu kudhulumu maslahi ya wachezaji lisimamiwe na Serikali tunakubaliana nalo maoni yanazingatiwa pamoja na kutoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadhamini kutotoa zawadi kama walivyoahidi Wizara ifuatilie, tunashukuru kwa ushauri huo tunafuatilia ili mambo yaweze kwenda. Mheshimiwa Susan Lyimo, amezungumzia Wizara ithamini michezo mingine hili limezungumzwa na Waheshimiwa wengi na naomba nilijibu kwa wote kwa sababu ya muda ni kwamba Wizara inazingatia michezo yote na tunajitahidi kuhudumia michezo yote na kama mnavyofahamu hata sasa hivi hatukuajiri *coach* wa mpira wa miguu tu sasa kuna *coach* wa *golf*, tunataka kuajiri *coach* wa *boxing*, tuna *coach* wa *tennis* ameshaajiriwa kwa miaka miwili, tunataka kuajiri makocha wa riadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kwamba tunajali mchezo wa mpira wa miguu peke yake na ni vizuri mkaelewa kwamba kila chama katika Tanzania kinaendesha mchezo wake wenyewe kwa kushirikiana na Baraza la Michezo na ndio maana nataka nitamke hapa kuisifia *TFF,* wao wanajitahidi wenyewe, mikakati yao ni mizuri na ndio maana wanapata wafadhili, wanapata watu wengi wa kuwasaidia fedha kwa sababu wanaandika maandiko wanayopeleka kunakohusika, Serikali tunaingilia ili kuwapa nguvu vyama vingine vyote vinatakiwa viige mfano wa *TFF*, hili lazima nilisema wazi kwa sababu iko tabia ya kusema kwamba sisi tunapendelea mchezo mmoja, hatupendelei mchezo mmoja ukiwa na mipango mzuri ya *volleyball*, ukiwa na mipango mizuri ya *handball*, ukiwa na mipango mizuri ya riadha utapata wafadhili. Naomba vyama vingine viige mfano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Susan Lyimo, amezungumzia si vema soka ikafanywa *issue* ya CCM na Ilani yao na hata Timu ya Taifa ikaitwa *JK Boys*, siyo kweli kuwa suala la soka ni la CCM. Mipango inayoendelea kutekelezwa inatokana na Ilani ya CCM, michezo ni kwa watu wote na CCM inazingatia maslahi ya watu wote. Aidha, Timu ya Taifa inaitwa *Taifa Stars* siyo *JK Boys* isipokuwa wapenzi wa michezo wenyewe na waandishi wa habari wamei-*nick name* kwa nia nzuri, ukienda Zambia timu yao inatwa *KK Eleven,* ni hamasa kwa sababu kiongozi wa nchi ameonyesha mfano kwa hiyo, watu wamejenga hamasa ya kuiita *JK Boys* kwa hiyo, si vibaya lakini jina rasmi ni *Taifa Stars*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba Serikali iwasiliane na Serikali za China ili mechi ya Tanzania na Msumbiji ichezwe Dar es Salaam kwenye uwanja mpya, hili limechangiwa na Waheshimiwa wengi na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu yeye ametoa ombi maalumu kama mlivyomsikia wakati anachangia pia ameandika ndugu yangu Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu kuomba kwamba mchezo ule uchezewe Dar es Salaam katika uwanja mpya. *(Makofi)*

Ningependa kujibu kama ifuatavyo, sheria za mchezo na zile za *FIFA* haziruhusu matumizi ya viwanja au majengo ambayo hayajakamilika hivyo ni busara tuendelee kusubiri hadi hapo utakapokabidhiwa uwanja ndipo michezo ifanyike pale, kwa sasa hivi uwanja hatujakabidhiwa kama Serikali, hatuwezi kucheza pale hata kama kuna *pressure* aina gani kwa sababu chochote kitakachotokea sisi ndio tutahusika na tunashirikisha nchi nyingine kwa hiyo hatutaruhusu mpaka tutakapokabidhiwa uwanja, nataka hili nilitamke wazi ili lisije likaleta utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Dorah Herial Mushi, Manyara pongezi kwa Waziri tunashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kanuni inatuambia tuseme Mheshimiwa halafu jina lake, sema Mheshimiwa Dorah Mushi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani. Mheshimiwa Dorah Herial Mushi amezungumzia Serikali ijenge hosteli na kijiji cha michezo, nataka kujibu kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Kijiji cha Michezo ambacho kiko Uwanja wa Taifa sasa kitaendelea kuwepo kwa sababu katika awamu ya pili inajengwa Kijiji cha Michezo, inajenga hoteli, zinajengwa *indoor games* ambazo kijiji hicho kitaweza kuchukua wanamichezo 750 au vyumba 750 kwa hiyo, jibu lake linajijibu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa amezungumzia kuwa Serikali haijawekeza vya kutosha katika michezo hali inayopelekea kufanya vibaya katika mashindano ya Kimaifa. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, hoja yako ni ya kweli, Serikali imeanza kuwekeza, imejenga uwanja wa kisasa na bado inaendelea kuajiri makocha na bado tuna mpango mkakati mzuri wa kuhakikisha michezo katika Wilaya, Kkata, Tarafa na Mkoa tunaiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, amesema ni vyema michezo mingine ikapewa nafasi, hilo nimeshalijibu tunatoa nafasi kwa michezo yote. Pia Mheshimiwa Paul Kimiti amesema je, katika kuamua jina litumike kwa Uwanja mpya wa Taifa baada ya kumaliza kujengwa wananchi na wadau wamehusishwa? Katika kujibu swali lake ni kwamba tunavyoenda katika mchakato wa kutafuta jina wananchi pia tutawashirikisha ili nao watoe mchango wao katika kutafuta jina, kwa hiyo, ushauri tunauzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi amezungumzia sera ya maendeleo ihuishwe, tunakubaliana na Mheshimiwa Profesa

Philemon Sarungi sera ya maendeleo ya michezo yote tujitahidi Serikali kuendeleza, *Simba Sports Club* inapoenda kwenye mashindano ya Taifa, Serikali iwasaidie, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, tutajitahidi na ni kawaida yetu timu zinaposhiriki katika mashindano ya Kimataifa Serikali inasaidia.

Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu amesema naomba Wizara ituletee walimu na makocha, tunakubaliana na ushauri wake lakini tunamshauri kwamba kila Wilaya ina chama chake kinachohusika cha mpira au chama cha mchezo husika, nashauri Mheshimiwa Dunstan Mkapa, uwasiliane na Afisa Michezo na chama husika muandae mafunzo mafupi mafupi ya *Preliminary, Intermediate* na *Advance,* ili muweze kupata makocha na walimu wa michezo katika maeneo yenu na ndio utaratibu unaofanyika na sisi Wizara kwa wale ambao wamepata mafunzo ya juu tutawaendeleza katika Chuo chetu cha Malya ambacho ndio kinatoa mafunzo kwa michezo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa amepongeza Wizara na tunashukuru. Mheshimiwa George Lubeleje amezungumzia viwanja vya Mpwapwa vina hali mbaya, tunamshauri ashirikiane na Halmashauri yake ya Mpwapwa ili waweze kuviboresha viwanja katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli amesema Serikali itoe mwongozo ili Halmashauri ziipe michezo kipaumbele kwa sababu hawachangii, Mheshimiwa William Shellukindo tunakushukuru sana na katika hotuba ya Waziri amesema michezo itiliwe maanani katika Halmashauri zetu na maafisa michezo waajiriwe katika Halmashauri zetu ili tuweze kuendelea. Pia Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, nimeshajibu Bendera inapepea kule Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili anauliza, Waziri anaweza kutufahamisha kama kuna kumbukumbu zozote za wachezaji wa zamani walio Timu ya Taifa? Mheshimiwa Nuru Bafadhili, kumbukumbu zipo ofisini, nakukaribisha ofisini ili uweze kuzipata kumbukumbu za wachezaji toka nchi hii imezaliwa wachezaji wote wameandikwa ambao wamechezea nchi hii katika michezo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe amesema mkazo usiwe kwenye mpira wa miguu, tumeshalizungumza michezo yote tunaipa kipaumbele Serikali inatilia mkazo kwenye michezo yote na siyo mpira wa miguu peke yake, imeanza kwa kuajiri makocha na tutaendelea kuajiari makocha katika sehemu mbalimbali. Lingine ni kwamba Serikali iwekeze kwenye viwanja vya michezo, hilo nimeshalijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, aliuliza Uwanja mpya wa Taifa ni mali ya nani, napenda kumjibu kuwa uwanja huo ni mali ya Serikali na utamilikiwa na Serikali. Timu za Dar es Salaam zinatakiwa kulipia kiasi gani? Kutakuwepo na ada na matumizi ya Uwanja mpya wa Taifa kama ilivyo kwa viwanja vingine vyote, Uwanja wa Taifa wa sasa unaotumika kila mechi inapochezwa maduhuli

ya Serikali ni asilimia 10 na huu nao utapangiwa utaratibu wake kwa jinsi itakavyoonekana. Je, mgao wa *FAT* unakuwaje? Nayo hiyo *TFF* wana utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa heshima hii jioni ya leo kumalizia ngwe hii ya mwisho ya siku yangu hii ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini Waheshimiwa Wabunge mmenisaidia sana katika michango yenu na mtaipitisha Bajeti hii bila shida yoyote nyingine hasa kwa sababu tumetekeleza kwa vitendo yale ambayo majukumu yetu katika nchi yetu hii. Kuifanya Timu ya Taifa kuvuka vigingi kwa 60 kuanzia 105 duniani si jambo dogo hilo, kuifanya Timu ya Taifa kuwa ya 28 katika Afrika si jambo dogo hilo, kufanya Timu ya Taifa kuwa ya tatu katika Afrika Mashariki na Kati si jambo dogo hilo, kwa hivyo nafikiri haya ni pamoja na mengine mengi mtasaidia kupitisha hoja hii haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sipati nafasi ya kuzungumza mara kwa mara ningependa niwapongeze sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Uzini. Kuna watu wanapita pita huku wanasema sionekani, nitakuja karibuni nipo Bungeni hapa, hawa watu hawana kheri na mimi, hawanipendi, niko hapa kufanya kazi ya CCM ambayo mmenichagua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa niwashukuru sana Naibu Mawaziri wangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kwa mchango wake mzuri na pia Mheshimiwa Joel Bendera kwa mchango wake mzuri na umenisaidia sana katika Wizara hii, mafanikio yote haya ni pamoja na mchango wao ndugu zangu hawa Naibu Mawaziri hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwongozo wake na msaada mkubwa alionisaidia mara kwa mara wakati nikiwa Bungeni na nje ya Bunge. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wengine wanaona wivu ukiondoka unanipa nafasi kukaimu, hawapendi kunipa nafasi, wewe nipe usiogope. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Joel Bendera, kwa kushinda kesi yake ya uchaguzi kule Korogwe Mashariki, kwa hiyo, sasa hivi anafanya kazi kwa moyo mkubwa kwa sababu hana wasiwasi anajua yupo hapa mpaka 2010 na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwataje waliochangia katika hoja yangu ya leo ni jumla ya Waheshimiwa Wabunge 67, waliozungumza ni 13 na waliobakia ni wa kuandika. Nao ni Mheshimiwa *Capt*. John Komba, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed

Mudhihir jirani yangu, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, hao ni waliozungumza hapa Bungeni leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Masolwa Cosmus Masolwa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Adam Malima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mtu nimemsahau naomba anisamehe sana niko tayari baadaye kutaja jina lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wakija hapa wanashukuru sana wake zao na waume zao lakini mimi nataka nimshukuru binti yangu Nawal Muhammed Seif, kwa sababu ananipenda sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ya leo nataka niongeee maeneo mawili ambayo nafikiri nitoe ufafanuzi kwanza ni kuhusu maadili ya uandishi wa habari. Uandishi wa habari ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni taaluma kama ilivyo taaluma nyingine yoyote kama ilivyo daktari, uhandisi, ualimu na hata uansheria. Ni kazi ambayo mtu anasomea, kwanza awe na kiwango cha juu cha elimu halafu anasomea taaluma yenyewe. Kwa hiyo, uandishi wa habari siyo kazi ile ya msaka tonge yaani *day*

*worker* unaamka asubuhi na kalamu yako unaandika tu, ni kazi ya taaluma ambayo inasomewa. *(Makofi)*

Pia ni lazima mwandishi ajue kwamba maisha ya Taifa lake yapo katika mkono wake ule. Kalamu ni hatari kuliko mzinga na kuliko bunduki. Inaweza ikaangamiza jamii mara moja kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu waandishi wa habari kwamba wazingatie maadili ya uandishi kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya Umoja wa Taifa letu na kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida, jamii au nchi inakuwa na maadili yake yatokanayo na maisha, utamaduni na desturi ya jamii ile ndiyo maana utakuta tofauti ya maisha ya Watanzania na Wakenya na Waganda kwa sababu kila mmoja anajengwa na taratibu za jamii yake ilivyo. Msingi mkubwa wa maadili ya jamii ya nchi ni kuzingatia amani, heshima, haki, uelewano, uhuru, umoja, uvumilivu, ustahimilifu na mshikamano. Hayo ni mambo ya msingi ya maadili ya nchi yetu hapa Tanzania. Kwa maana hiyo, waandishi wa habari lazima wazingatie hayo pale wanapofanya kazi zao ndani ya jamii yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mwandishi wa habari ni lazima aandike ukweli. Mwandishi yule mwenye heshima na jamii yule anaandika ukweli siyo anaamua leo nataka kumwadhibu Mzee Ngombale, basi atanitambua, akamata kalamu yake anaanza kumzulia uongo. Huyo hawezi kuwa mwandishi mwadilifu. Ni lazima uwe mkweli kwa jambo ambalo unaliandika, usizue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja hivi karibuni, mimi na wewe ni Wajumbe wa Kamati Kuu na Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mambo mengi yamezuliwa ambayo si ya kweli, hayakuzungumzwa ndani ya Kamati Kuu ya CCM, 99% ni ya uongo. Sasa huu ni uandishi gani? Tafuta ukweli uandike au usiandike kitu unachokitaka tu si lazima uuze gazeti kama huna cha kuandika. *(Makofi)*

La pili, mwandishi wa habari ni yule ambaye hana upendeleo anakuwa *fair* na *balance* kama wanazungumza watu wawili kati ya Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, nenda kwa Mheshimiwa Daniel Nswanzugwanko kamuulize habari ile na Mheshimiwa Joel Bendera muulize kila mmoja atakupa maoni yake, ndiyo uandishi wa habari unavyotakiwa. Kuna *balance and fair.(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaomba waandishi wa habari kwamba wafuate maadili ya waandishi kuwa *balance and fair* katika uandishi wao wa habari. *(Makofi)*

La tatu, mwandishi wa habari ni yule ambaye anaandika mwenyewe bila kushurutishwa na kulazimishwa ama kwa pesa au mwenye chombo hicho cha habari. Mimi najua waandishi wa habari wapo wanatumwa na waandishi wao, andika hili anaandika, sema hili anasema, huo si uandishi wa habari na hayo si maadili, maadili ya uandishi andika yale ambayo wewe mwenyewe unaamini hili na liandike au acha kazi, si

lazima uandike kama unalazimishwa. Lakini mwandishi wa habari pia unatakiwa uwe na uadilifu yaani ni muhimu sana. *(Makofi)*

Lakini jambo lingine kubwa ni kwamba kuandika kwa ukweli yaani *accuracy,* andika habari ya kweli lakini pia jambo kubwa la msingi ni kuheshimu mtu na utu wake *(privacy).* Watanzania tuna tabia ya kufuata watu na kuingia katika maisha yao ya binafsi, hii si haki na ni kinyume cha uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu alipotembelea kwenye Wizara yangu pale alitoa nasaha na mimi napenda nimkariri alichosema kuhusu uhuru wa waandishi wa habari usio na mipaka, akasema hivi; "Serikali tutasisitiza uhuru wa vyombo vya habari, tutahakikisha kwamba hatuwaingilii katika kutimiza wajibu wake, lakini rai yangu kwao wanahabari ni kwamba mtambue dhamana yao na watimize dhamana hiyo vizuri kwa sababu uhuru wa vyombo vya habari unakoma pale haki ya mtu inapoanza."

Nasema tena, uhuru wa vyombo vya habari unakoma pale ambapo haki ya mtu mwingine inapoanza, maana yake usiingilie mambo binafsi ya mtu mwingine. Uhuru ambao hauna ukomo,uhuru usiokuwa na mipaka unakuwa ni uhuru wa kuchochea vurugu. Kwa hiyo, naomba waandishi wa habari wenzangu nawapenda sana waandishi wa habari, fuateni maadili yenu ya uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nataka waandishi wa habari wasibague watu ama wa jinsia, ama wa kabila, ama wa vyama na kadhalika, wewe andika habari kwa mujibu wa hali ya kweli. Mkifanya hivyo mtajenga heshima yenu katika jamii hii. Hili la kwanza. *(Makofi)*

La pili, nimesahau kumbe ndugu yangu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, sikumtaja, naomba samahani Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na wewe pia ulichangia hoja hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hili la kwanza nataka nizungumze kuhusu umuhimu wa waandishi wa habari kufuata maadili, kujua mipaka yenu, kujua uzalendo, kujua kwamba nchi hii itahitaji mshikamano na maendeleo. Mimi naangalia sana televisheni za nje hasa *CNN, BBC* na kadhalika, sijaona mimi hata siku moja maiti ya Mmarekani kule Iraq, sijaona mimi, hawafi? Hawaumizwi? Wapo lakini wanalinda heshima ya Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona juzi hapa katika gazeti moja sikumbuki ni lipi kuna mtu ameruka anamkanyaga mwenzake kwenye kichwa, binadamu mwenzako unaruka juu unamkanyaga na unazidi kumuumiza, ni Mtanzania mwenzako na waandishi wanaandika. Yanatoka wapi haya jamani? Tuwaheshimu binadamu. Yule ni binadamu pia anaweza kuwa ndugu yako, mjomba wake, baba yako, mume wako na kadhalika. Kwa hiyo, ni lazima tuwaheshimu watu katika mazingira mbalimbali. Hili naomba nilizingumze la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nizungumze hili ambalo nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza na ningependa nimshukuru sana kwenye sakafu ya moyo wangu ndugu yangu Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, kwa kweli amesema vizuri sana pamoja na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Zaynab Vulu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwenye maandishi yao. Nawashukuru sana kwa sababu wameelezea vile ambavyo nafikiri inafaa muelezee. *(Makofi)*

Sasa hili la *MOAT* na TUT naogopa isije ikawa ya Mheshimiwa Adam Malima. Mwaka jana ikawa mwaka mzima tunakuwa kwenye kesi tu, kesi tu kwa sababu unataja mambo ya watu ambayo hawapendi wenyewe. Lakini nitasema yale ambayo nafikiri niseme, kwa sababu mwaka jana tulizungumza hapa mambo ya Bungeni tena Bunge likatumia milioni 400 sijui na mwaka mzima hayajamalizika. Lakini hili la *MOAT* na TUT kwa sababu mimi ni Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nina wajibu wa kuelezea yale ambayo nafikiri inafaa kuyaelezea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema kwamba TVT kwanza mjue TVT ina ruhusa kwa mujibu wa *charter* ya Serikali kufanya biashara, inaruhusa rasmi na Serikali tumekubali wafanye kazi hiyo kwa kipindi maalumu mpaka pale ambapo watajiweza wenyewe watajitegemea kama ilivyokuwa kwa *Daily News. Daily News* Serikali haitoi hela yoyote. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kuua vyombo vya habari kwa sababu sisi ndiyo tumeviruhusu viwepo kwa sheria na vipo vingi tu wala havina mpaka na mimi sijaambiwa kwamba ikifika vingapi uzuie, hapana. Redio zinakuja na magazetu yanakuja tu hakuna mpaka wowote kwa hiyo Serikali haiwezi ikaua vyombo vya habari kwa sababu yenyewe ndiyo iliyoruhusu viwepo vyombo vya habari na vishamiri katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi wenyewe pia Serikali ndiyo ambao tunatoa matangazo mengi sana kwa vyombo vya habari binafsi mengi sana kwa mamilioni. Mimi napenda mwakani tufanye hesabu tuleta hapa kwa kiasi gani Serikali inatumia kuviwezesha vyombo vya habari binafsi yaani bilioni ngapi kwa mwaka, mtanona ninyi matangazo makubwa na ya hakika ni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mashirika yake. Kwa hiyo, haiwezi kuwa sisi tunaviandama vyombo hivyo, kwa hiyo, nataka viimarike na visaidie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naamini kwamba kuimarika kwa chombo cha Taifa kama TVT ni kuimarika kwa watu wadogo na umma wa Watanzania. Ni kuimarika mahali Serikali inatamka tamko ambalo kwa watu wote bila kujali dini yake, kabila lake na chama chake. Serikali kwa kawaida inakuwa haina dini, wala kabila wala chama ni Serikali ya Watanzania wote. Ni lazima tuwe na chombo ambacho kinaweza kutoa kauli ambayo inakubalika na ina hakika, lakini Serikali ndiyo mtetezi mkubwa sana wa maslahi ya watu wa kawaida na wa chini kabisa. Kwa hiyo, Serikali ni lazima isaidie vyombo hivi yaani TVT na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi vyombo vya Serikali, TUT na Redio Tanzania na kadhalika ndiyo wenye jukumu la msingi la Katiba kuhabarisha watu wote kila walipo, Serikali ndiyo jukumu la kwanza na siyo vyombo vya watu binafsi. Kwa hiyo, ni lazima

tuwezeshe chombo hiki kitekeleze malengo yale ambayo imejiwekea na Serikali, ndiyo maana unaona kwamba kuna baadhi ya maeneo  hakuna vyombo binafsi, havipo na havitakuja huko vifanye nini na havipati faida, hivyo vinaishi kwa faida na si makosa hata kidogo ni haki yao. Lakini chombo cha Serikali hiki ni lazima kiwezeshwe ili kupokea na kutoa habari ziweze kufikika kila eneo. Kwa hiyo, nasema haiwezekani sisi chombo cha Serikali kiache kufanya wajibu wake wa kujiimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama Serikali inataka kuua vyombo vya habari kwa nini kila siku vinaongezeka? Kwa nini havifi? Kwa nini havifi ni kwa sababu vinapata faida na siyo sababu ya hii sababu ya hivi juzi kwa sababu TUT inataka matangazo juzi tu. Miaka yote walikuwa wapi kusema? TUT iko zamani hapa kwa nini ni juzi tu kwa zabuni hii moja ya paundi milioni 150 hela ndogo sana hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema hapa kwamba naomba *Daily News* ipo sasa hivi inajitegemea na ninaamini kabisa kwamba iko siku tukiwezesha hawa ndugu zetu wa TUT watafanikiwa kuweza kujitegemea wenyewe na wataendelea na kazi zao na kadhalika. Tuwape muda, sawa sawa na wapiganaji ngumi huwezi kumwambia TUT ijitegemee wakati bado dhaifu, nia yao ni kuimaliza TUT  tunajua sisi na hatukubali TUT ife, ni lazima tuiimarishe, tuipe nguvu ili iweze kushindana kweli kweli wakati huo itakuwa huru kushindana na wengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa kwamba tunataka uwe uwanja sawa wa biashara, ni kwa Tanzania tu basi? Uwanja huu upo hapa tu? Vipi kuhusu Kenya, Uganda na *South Africa* hakuna wenye usawa, hapa Tanzania tu? Wanajua hayo lakini wanataka kupotosha ulimwengu tu. Kwa hiyo, muache Tanzania afanye hivyo na Kenya na Uganda kwa hiyo jambo hili ni halali kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo haya ya habari kuna mambo matatu yaani kuelimisha, kupasha habari na kuburudisha, hayo ndiyo mambo ya msingi ya vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la biashara ni la nne sasa hivi lakini baadhi ya vyombo vya habari binafsi haya ya mwanzo matatu hawayataki ya kuelimisha, kupasha habari, hapana wao ni biashara tu ni kinyume na maadili ya uandishi, yote haya yawemo na kwa hiyo, TUT ikifanya kazi ya kuelimisha, sawa, kupasha habari, sawa, bashara hapana! Usawa uko wapi?  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kwamba tuna wajibu sote tufanye kazi hiyo yaani tuelimishe, tuburudishe, lakini biashara pia tupate tuiendeshe nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sidhani kwamba kuwepo kwa Redio ya Taifa *(RTD)* kumefanya redio nyingine zisiwepo, *Radio One, Radio Clouds, Radio Africa, Radio Free Africa, Zenji FM* hazipo kwa sababu ya hii tu, haziwe kuwa? Kwa hiyo, nasema redio hizi zipo lakini zinaishi pia basi tusaidiane na tusaidie kwa kusema kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwataje hawa wasije wakazuia shilingi hapa ni Wabunge Waheshimiwa wa muhimu sana hawa wote nawapenda sana hawa. Hapa nilisahau kuwataja Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu na Mheshimiwa Juma Killimbah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kusoma gazeti hili la Tanzania Daima la tarehe 05 Agosti, 2007. Kuna mwandishi mmoja anaitwa Balile, yeye alikuwa Mhariri wa hii Tanzania Daima. Ameandika kuhusu sakata hili la *MOAT* na TUT kwa sababu yeye ni mwandishi mwenzao, msikie lugha yao anasema nini yuko Uingereza anasoma lakini hata hivyo kaandika najua ataambiwa leo usiku aambiwe lakini potelea mbali na hili jambo ni jema. *(Makofi)*

Mwandishi huyo kasema hivi naomba nikariri pole pole ili msikie vizuri nisije nikakosea, Ndugu Balile kasema hivi; "Wamiliki hawa hawataki kusomesha wafanyakazi wao wawe na viwango vizuri hawa ndiyo wanaotudhalilishia vipindi vinavyotengenezwa na watu waliokuwa makondakta wakageuka waigizaji na sasa watangazaji, sisemi mtu hawezi kubadilika ila kutoka uigizaji hadi utangazaji bila kupelekwa shule kwanza ni kudhalilisha taaluma ya habari. " Mwisho wa kunukuu.

Huyu ni Mhariri wa Tanzania Daima na mwandishi mwenzao anaendelea kusema: "Kinachotakiwa hapa ni ubora wa vipindi na ubunifu utakaofanya mapato ya matangazo mengi zaidi. Nasikia kimeanzishwa kipindi cha vichekesho katika televisheni kinaitwa *Ze Comedy* kipindi hiki sasa kinafanikiwa hata matangazo ya vipindi vya televisheni nyingine ikifika wakati wake, kinachotokea hapa ni hali ya ubunifu, utafiti na kuipa jamii kinachohitajiwa kisha matangazo yataletwa yenyewe. Matangazo ya mpira ni moja kati ya huduma kubwa za msingi kwa wananchi. Kipindi cha nyuma tumeshuhudia malumbano kati ya wamiliki binafsi kwa sababu ya lengo lao na kupata faida na siyo kuhudumia wananchi, walifikia hatua ya kuwakosesha wananchi uhondo kwa michuano ya Kimataifa eti kwa sababu tu mmoja amenunua haki ya kurudisha matangazo hayo na kupata matangazo ya biashara hata kama matangazo yake yanaishia Manzese."

Anaendelea kwamba; "Wapo waliokuwa wanatoa huduma ya *cable* kwa kutumia *decoder* hawa nao nasikia walishafanya Watanzania kuwa kivuno, wapandisha dau hadi dola 70. Sasa nasikia baada ya mpango huu wa TUT umeshuka bei hadi dola 25. Mimi nasema usingizi waliokuwa nao TUT miaka iliyopita umelifikisha Taifa pabaya na kuwafanya baadhi ya watu kuwa mamba katika dagaa. Wakati umefika sasa Watanzania wanastahili kupata huduma bora iwe ni kwa kupitia kodi zao au matangazo ya vituo binafsi tuukubali ushindani tunaweza kushindana." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni gazeti la tarehe 05 Agosti, 2007 Tanzania Daima, Makala ya Ndugu Deodatus Balile kutoka Halle huko Uingereza, naye ni msomi huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba nashukuru sana kwamba Waheshimiwa Wabunge mmetoa mawazo yenu mazuri sana ya upande wa Upinzani, upande wa CCM na mmoja mmoja tutayathamini, tutayachukua, tutayaboresha mambo yetu na tunaamini kwamba tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mwisho nimalizie, watu wengi wamesema hapa kuhusu Mkurugenzi Dunstan Tido Mhando, ninamjua sana, ni mtu ambaye ana ari ya kufanya kazi ni mchapakazi, anapenda kazi yake na jambo kubwa zaidi ni mbunifu. Ni mbunifu sana na ndiyo maana nafikiri sasa ni tishio kwa *TV* za Tanzania, kaingia mwamba sasa, chaka limeingia simba sasa wanakimbizana watu. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaomba kumwambia Bwana Tido kwamba uzi ni huo huo tutakuunga mkono na utafanikiwa kwa sababu Serikali iko pamoja na wewe usiogope. Lakini nakuahidi kwamba iko siku na wewe pia utajitegemea mwenyewe kwa sababu nataka ujitegemee, usiwe na wasiwasi tukupe muda ujiandae ili mradi ujitegemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niseme kwamba nawashukuru sana waandishi wa habari wote kwa ujumla, nashukuru sana vyombo vya habari vya Tanzania vyote kwa ujumla kwa sababu Wizara yangu ndiyo Wizara ambayo inatawala vyombo vya habari vya Tanzania vyote, uongo, ukweli? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kweli!

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Kwa hiyo, vyombo vya habari vyote, redio, televisheni na magazeti viko chini ya Wizara Habari, Utamaduni na Michezo, hapana mwingine. Lakini pia si hayo tuna utamaduni, tafuta wewe kipindi cha redio, televisheni kama hutakuta utamaduni, hukuti? Gazeti hukosi michezo kila siku Mungu akupe nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawashukuru sana ndugu zangu waandishi wa habari, nyote nawapenda sana, tushirikiane na tusaidiane. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Mheshimiwa mwenyewe ana redio yake kwa hiyo siyo kwamba hajui mambo haya, anayajua vizuri. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kufikia uamuzi mzuri tunafuata hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo**

Kifungu 1001 *Administration and Genereal*... ... ... ... Sh. 1,003,665,300

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Christopher Ole-

Sendeka, Mheshimiwa Margaret Mkanga na Mheshimiwa Zaynab Vulu. Tunaanza na Mheshimiwa Margaret Mkanga.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa. Programu hiyo hiyo, mshahara wa Waziri, sina maana ya kuutoa, ni swali tu ambalo nataka ufafanuzi mzuri zaidi.

Katika mchango wangu wa maandishi niliuliza kwamba je, ile timu inayotegemewa kwenda China mwezi Septemba, 2007 ya *Special Olympic* ni kweli imeshaandaliwa kikamilifu kwamba wanakwenda wote 30? Nimeuliza hilo ili nipate jawabu sawa sawa kwa sababu ni mpaka jana wanaohusika wakifikiria kwamba angalau ni mwakilishi wao walikuwa wanaendelea kuhoji na kusema kwamba inaelekea hii safari haiwezekani. Kwa hiyo, nataka tu kuwekwa sawa hilo. Ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Joel Bendera ajibu kwa ruksa yako.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kumjibu Mheshimiwa Margaret Mkanga swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba suala analolizungumza ni kweli na ni kwamba mwezi Septemba, 2007 timu yetu ya Taifa ya *Special Olympic* inakwenda China.

Katika Bajeti iliyopita tulitenga fedha na katika Bajeti hii pia tumetenga fedha na fedha hizo na timu hiyo inaandaliwa ili iweze kwenda. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia kwamba safari hiyo ipo na tunaandaa kwa kushirikiana na wadau wengine wa michezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, karibu.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 96, programme 10, sub vote 1001.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliposimama kwenye kifungu kama hiki kuna masuala nilizungumzia na kama mnavyojua nilipata balaa kidogo lakini *alhamdulillah,* sasa naomba majibu ambayo yatanitosheleza ili yanisaidie mimi na wanaotusikiliza huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu Waziri wamezungumzia sana suala la sera ya habari na sheria ya habari na mwaka jana nililiulizia hili nikambiwa linakuja sasa na ninaomba maelezo kuhusu suala la usimamizi na udhibiti wa maudhui potofu ya utangazaji na ufuatiliaji wa maadili ya utangazaji.

Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake aliyonipa amesema suala hili kwa ukurasa namba 17 kifungu cha 20 hadi 22 cha hobuta yake linashughulikiwa na kitu kinachoitwa Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano ya *TICRA* na ina kazi maalumu. Lakini anasema wanapofanya kazi hiyo kuna kazi ya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha vituo vya utangazaji nchini vinazingatia Sheria na Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa nane anasema sheria yenyewe inalalamikiwa na wadau na imepitwa na wakati kwa sababu sheria yenyewe ni ya mwaka 1993 ya utangazaji. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie tena kama alivyonisaidia mwaka jana kwamba sheria hii kwanza ya habari na pili sera yenyewe ya habari baada ya kuzifanyia *reform* zinatoka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusiana na suala zima la TUT. Suala la TUT kwa wananchi wa Tanzania inapotoa matangazo kwenda Mkuranga au Namtumbo au Mchinga au Donge ni *obligation* ni wajibu wao. *ITV, Channel 10* na wengine watafanya kwa maslahi ya kibiashara, lakini hawa wanafanya kwa wajibu wao kwa sababu hiyo pesa wanayotumia tunachangia sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusitafute *excuses* hapa. Serikali inihakikishie kwamba itafanya kila linalowezekana kwa sababu kwanza kabisa lazima tutambue kwamba hao waliokuwepo kabla wameanza miaka sita, saba kabla ya TVT.

Kwa hiyo, ninaomba tuchukulie kwamba walikuwa na *head start* ya miaka saba, wasianze kulalamika sasa na kwamba TUT pesa walizopewa kwanza ni ndogo kwenye Bajeti ya Maendeleo, Redio Tanzania haikupewa chochote mwaka jana, haikupewa mwaka huu, TVT hakupewa chochote mwaka jana, hakupewa mwaka huu na katika matumizi ya kawaida TUT mwaka jana ilipewa shilingi bilioni 7.1 mwaka huu imepewa shilingi bilioni 5.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa hayo mawili. Hili la pili anisaidie kama tunatumia namna hii TVT itajitanua vipi ili iweze kufikiwa matangazo yake kwa ufasaha na huo mpira tuuone Mkuranga na nampongeza sana ndugu yangu Dustan Tido Mhando tulikuwa tunaishi wote *South London,* nimefurahi kwamba amerudi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nampa pole sana Bwana Malima kwa sakata la mwaka jana, mwaka huu hilo halitokei, usiwe na wasi wasi, tuombe Mungu na mimi pia nilikuwemo katika hao miongoni na wewe pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Serikali ingependa sana kila mahali iwepo televisheni na redio na ndiyo nasema wajibu wa Kikatiba kwamba kazi ya kupeleka vyombo vya habari kila eneo ni kazi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndio wajibu wetu huo. Jitihada zote hizi za kutafuta matangazo ni njia moja ya kusaidia Serikali ili ifikishwe hapo kwa hiyo, naamini kwamba *Inshallah* mwakani. Kwa

hiyo, naamini kwamba Serikali itatusaidia tukipata fedha kuweza kumaliza awamu ya pili ya vituo vya televisheni pamoja na redio ili kila mahali ikiwezekana zisikike. *(Makofi)*

Suala la sheria ni kwamba tunataraji kwamba sera na sheria zitatekelezwa. Tunataraji kwamba Bunge lijalo litakuja hapa na Wabunge watapata nafasi kujadili na kutoa maoni yao. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa majibu ya kuridhisha, lakini ningependa nipate bado maelezo katika maeneo mawili.

La kwanza wakati Naibu Waziri anayeshughulikia mambo ya lugha akijibu, alijibu vizuri kwamba kuna utaratibu mzuri wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha inayostahili kwa sababu sasa Afrika kwenye Kanda ya *SADC* na kadhalika imeanza kupewa hadhi. Lakini mambo aliyoyaeleza ya kukuza Kiswahili kwa hadhi hiyo ni pamoja na kuandaa walimu, kutengeneza kamusi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa nijiridhishe vizuri zaidi kwamba kwa uzito wa lugha ya Kiswahili kwa jinsi wenzetu katika Kanda na katika Afrika wanavyoipa Kiswahili uzito haya aliyoyasema Waziri ni kama hajanitosheleza. Nataka anipe uhakika kuna ratiba gani kamili na kuna *statement* gani ambayo Serikali inaandaa kama si leo na nina hakika si leo kwa sababu haijaandaliwa, lakini ni tamko gani ambalo Serikali itaandaa kwamba sasa Kiswahili kinaenda kuwa lugha ya kufundishia kwa sababu mpaka sasa hivi kuna mjadala tu unaendelea.

Kwa hiyo, nilitaka hilo anihakikishie na kama je, tuna ratiba fulani ambayo tunaiandaa, kama hatujaiandaa basi ni lini tutaiandaa ili Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia na hii ni muhimu kwa sababu duniani kote watu wanataka kufundishwa kwa lugha ya kuzaliwa kwa sababu dhana zile wanazielewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakati nachangia vile vile nilitaka kujua katika suala la TUT limejibiwa vizuri sitaki kuingilia yale mengine. Lakini nilikuwa na tatizo katika eneo moja ambalo Waziri hakuligusia kabisa. TUT ukienda kule pamoja na kwamba ni kioo cha Taifa ndiyo walezi wa maadili ya nchi hii na pale pia kuna suala la ulinzi wa Taifa lakini vijana wetu watangazaji hawana vyumba vya kutosha, wanafanya kazi kwa kujibana, mahali pa kurekodia vipindi nayo ni ya tatizo, lakini kuna majengo ambayo ni maghofu kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Sisi kwenye Kamati tumetembelea, mimi nilikuwa kwenye Kamati inayohusika na vyombo vya habari, tumetembelea na sijapata maelezo kwamba yale majengo yatamalizika lini. Ningependa Waziri anihakikishie na kwa kuwa kama *MOAT* wanavyosema kwamba wao wanapewa ruzuku, mimi sijaona hiyo ruzuku wanayopewa TUT. Sasa kutokupewa ruzuku ni pamoja na kuweza kumaliza majengo yake. Nataka kupata uhakika ni lini itapata fedha za kutosha kukamilisha yale majengo ili waweze kufanya kazi zao kikamilifu zaidi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, mimi nadhani badala ya ratiba nadhani mkakati. Ratiba itakuwa ngumu sana kuiandika hapa. Tunaomba majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba nimjibu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Kiswahili hilo halibishaniwi na kama nilivyosema sasa hivi ni lugha rasmi katika *AU* katika Bunge la Afrika, *East African Community*, *SADC* na kadhalika. Sasa liko suala la kutumia Kiswahili na kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia ni vitu viwili tofauti kidogo. Nadhani unachozungumza Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kama nimekuelewa vizuri ni hii Kiswahili kama lugha ya kufundishia. *(Makofi)*

Sasa kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti niseme tu kwamba Serikali haijachukua uamuzi rasmi wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia kuanzia chekechea hadi Chuo Kikuu. Tunachofanya kwa mujibu wa ile sera yetu ya utamaduni ni kwamba hilo limetamkwa katika sera, kinachofanyika ni maandalizi na maandalizi yana hatua mbili, hatua ya kwanza ambayo imechukuliwa tayari ni kuanzia Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi tunatumia kuanzia Shule ya Sekondari kwenda Chuo Kikuu.

Kwa hiyo, mkakati ni kwamba sisi Wizara tayari tunaandaa waraka wa Baraza la Mawaziri ili kupata *a corrective decision* ili kama Serikali tupige hatua tukiwa pamoja kwa sababu hili jambo linahusu Wizara zaidi ya moja. Kwa hiyo ningependa nieleze hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni TUT inafanana na hili la mwanzo la Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Yale majengo yao

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Majengo ya TUT. Kama tulivyosema wakati tunajibu, ni kwamba tayari tuna mazungumzo yanaendelea na kwa kweli tumefika hatua nzuri ili wenzetu wa *NSSF* kwa *guarantee* kwa udhamini wa Serikali waweze kuyakarabati majengo yaliyopo *Pugu Road* na Mikocheni. Lakini pia hata hizi juhudi za TUT kufanya biashara hii ambayo inapigiwa kelele ni maana yake ni kuendelea kupata maduhuli ili hatimaye iweze kujiendesha wakati huu wa uhaba wa fedha kwa sababu vipaumbele kama unavyofahamu vitabadilika mwaka hadi mwaka.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nami pia niungane na wenzangu kuwapongeza sana Mawaziri kwa jinsi ambavyo wamejibu hoja zetu, lakini nilikuwa naomba *clarification* kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni tumekuwa tukisikia kwamba kuna tatizo kubwa pale bandarini kwamba kuna nyasi zile bandia au majani bandia kwa ajili ya

Uwanja wa Taifa mpaka leo hatujui zimefikia wapi. Tulikuwa tunaomba kujua ni nani aliyeagiza na kwa nini kama Serikali ni hiyo hiyo kunakuwa na utata wa jinsi ya kuzipeleka hizo nyasi katika viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni *sub vote* hiyo hiyo lakini kifungu 260400 kuhusu *Medical Supplies*. Ukiangalia katika hiyo kasma utaona kwamba ni shilingi laki sita tu. Sasa nilikuwa naomba kwa sababu nikiangalia mwaka uliopita ilikuwa shilingi milioni 39. Je, tatizo liko wapi, kwa nini hela imekuwa ndogo kiasi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Kuhusu nyasi bandia ni kwamba kwa bahati nzuri nchi yetu Tanzania ni miongoni mwa nchi chache ni nchi 25 tu katika dunia ambazo zimepewa hizi nyasi bandia kuweka katika viwanja vyao. Tumepewa na *FIFA* na *TFF* wameomba Serikali ikomboe. Mwanzoni ilikuwa ni kwamba *TFF* wao wenyewe walipe, lakini Serikali kwa kuona umuhimu wa hilo wameona wao Serikali sasa ichukue jukumu na ndiyo Serikali imetoa fedha bandarini *TRA* ili kukomboa nyasi hizo na sasa hivi tayari zimeshatolewa bandarini zinawekwa.

Hili la pili ni kwamba hii *Vote* aliyozungumza ni fedha za matibabu kila Idara ina fedha zake. Zamani pia haikuwepo lakini kama mnavyofahamu kila Wizara imeombwa ipunguze matumizi kutokana na vipaumbele. Sasa moja ya vipaumbele ambavyo sisi vimepunguzwa ni katika matibabu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu nilichangia kuhusu *civic centre* chombo ambacho kinaweka vijana katika maadili mazuri na kwa kupata nasaha ya kubadilishana mawazo hapa na pale. Hilo la kwanza, sikupata maelezo yoyote kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili lilikuwa ni suala la BAKITA sasa kuanza kutafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili kuwafanya kila wananchi waweze kuzijua ili zisiwape taabu katika mwenendo wa maisha yao.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kutoa ufafanuzi kidogo kwa Mheshimiwa Mussa Zungu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *civic centre* kwa ajili ya mafunzo ya maadili, jambo hili Mheshimiwa Mussa Zungu ni jambo mtambuka sana. Sisi pale Wizarani mambo haya yanafanywa zaidi na watu binafsi katika maeneo mbalimbali. Lakini hata hivyo katika Halmashauri zetu za Wilaya hizi *civic centre* zinaweza zikaanzishwa na zikaendelezwa na Halmashauri zenyewe. Kumbe sisi Wizara tunaweza tukatoa hiyo *support* kwa ajili ya kuendesha hizi *civic centres* kwa ajili ya kufundisha maadili ya vijana na inakuwa kama sehemu pia ya taaluma ya michezo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili nilikuwa naomba lirudiwe hatukulisikia vizuri wote hapa.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwa suala la BAKITA kutafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili. Sheria hizi huwapa taabu sana wananchi ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza.

**MWENYEKITI:** Sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, BAKITA haina tatizo la kutafsiri sheria au nyaraka zozote nyingine. Ni jukumu la Wizara ya sheria kuwapelekea BAKITA watafsiri basi. Kwa hiyo, sisi tuko tayari kutafsiri na Wizara zote nyingine watuletee tuko tayari kutafsiri sheria za nchi.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja aliyotoa Mheshimiwa Mussa Zungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ili wananchi wa Tanzania waweze kuzielewa sheria zetu vizuri inapaswa iwe kwenye lugha ambayo inaeleweka kwa Watanzania walio wengi na kwa ajili hiyo basi kupitia Mwandishi wa Sheria wa Serikali tuna Kitengo ambacho tunajitahidi kuona kwamba zile sheria muhimu sana na ikiwezekana zote siku moja tujitahidi kuzitafsiri. Kwa hivyo, Serikali itajitahidi sana kuona kwamba katika kutoa haki zaidi sheria moja hadi nyingine kutafsiriwa kila uwezo wa Serikali utakavyowezekana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niko katika *sub vote* hiyo hiyo, mshahara wa Waziri na suala ambalo ningependa Waziri anipatie ufafanuzi zaidi ni suala hili ambalo liko katika vyombo vya habari sasa la *MOAT* na TUT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TUT ni *Public Broadcaster* na *public broadcaster* duniani zinaendeshwa kwa kanuni kuu nne uhuru, ufikiaji wa huyo mtangazaji kwa wananchi wote kwa ujumla, mchanganyo wa vipindi na vile vile kuhakikisha kwamba kunakuwa na utofauti kati ya *public broadcaster* na *private broadcaster. (Makofi)*

Sasa kitu ambacho mimi ningependa kujikita kwa leo ambacho ningependa kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri ni suala la uhuru unaporuhusu *public broadcaster* kama TVT kuingia katika *commercials,* kushindana na watangazaji binafsi katika matangazo ya biashara maana yake ni kwamba unaruhusu siku moja uhuru wa hii *public broadcaster* kuweza kuingiliwa na watangazaji kwa maana wafanyabiashara wanaotangaza. Bahati mbaya tu kwamba suala hili limechukuliwa kwa muono wa *MOAT v/s* TVT lakini ni suala pana kwa sababu nchi zote duniani mjadala wa *financing public broadcasting* ni mjadala mpana sana.

Sasa Waziri haoni kwamba kwa *challenge* hii ambayo *MOAT* wameileta ni vizuri kuanza mjadala kati ya Wizara, *public broadcaster* wetu ambayo ni TUT na wamiliki binafsi ili kuangalia njia bora zaidi za kuweka mazingira ambayo ushindani huu utakuwa ni *fair* kwa vyombo vya habari vya binafsi lakini pia ushindani huu hautaondoa uhuru wa TVT kuingiliwa na matangazo ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi huo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa ulishajibu sasa naomba ujibu *very briefly.*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejibu vya kutosha hapa nafikiri muda wangu wote nimetumia kwa hoja hii hapa. Lakini nasema kwamba hata wao *MOAT* hawakuja kushauriana na Serikali, waliamua kwenda kwenye vyombo vya habari wakatangaza tu basi. Kwa hivyo, wangekuja tungezungumza lakini hawakuja. Wao kama ni waungwana na wastaarabu wangetuambia basi. Lakini katika vyombo vyao na kutangaza na kutuponda ponda hivi nafikiri na sisi tumejibu mapigo tu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* hiyo hiyo mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la sheria ya maendeleo ya michezo, ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu katika hotuba yake ya Julai, 2006 alizungumzia juu ya Wizara kuhuisha sera ya michezo na kuandaa sheria ya maendeleo ya michezo. Nilikuwa nataka nifahamu tu kwamba imefikia wapi kwa sababu hivi sasa ni takribani mwaka mmoja, hilo limefikia wapi na lini hiyo sheria itakuwa tayari ili iweze kutumika? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mheshimiwa Idd Azzan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka jana tuliahidi kwamba sheria inaendelea kutayarishwa na kama alivyosema ni kweli hadi sasa tumeshaanza mchakato kuanzia ngazi ya Wilaya, Mikoa mpaka Taifa na kama akitazama katika kitabu chetu cha Bajeti cha mwaka huu bado tumeendelea kuzungumzia kupata maoni ya wananchi kwa sababu kutengeneza sheria ya kuendeleza michezo ni kitu ambacho lazima upate maoni mengi ya wadau na mustakabali wa mkutano wa mwisho utakuwa mwezi Oktoba. Kwa hiyo, baada ya hapo tutaweza kutengeneza sasa sheria baada ya kupata maoni kwa wananchi wote.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana *vote 96, programme 10, sub vote 1101,* kifungu 250100 Mshahara wa Waziri. Japokuwa ametuomba ametutajataja sana tusiishike shilingi lakini hatuna haja ya kuuchukua ila tunataka ufafanuzi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala la waandishi wa habari kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Nilieleza kwamba sisi pia

tunawategemea sana waandishi wa habari katika michango yao kwa maana katika utendaji wao wa kazi. Katika kueleza hayo nilitoa mfano ushiriki wa waandishi wa habari kwenye vita vya Uganda walivyoshiriki na walivyokuwa wanatuletea taarifa mbalimbali zilizokuwa zinatueleza sisi tumefikia wapi na tunawashambulia vipi wenzetu katika vita hivyo. Lakini kutokana na vita hivyo waandishi hao wa habari wako walioathirika, wengine kutokana na athari hizo marehemu sasa hivi, lakini wengine wapo na wengine hata hatujui wako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine nilimwona siku moja kwenye TV akijinadi alivyopewa tuzo ya redio yenye *band* moja dudu *proof*. Lakini sasa nikauliza je, Serikali ina mkakati gani kwa kuthamini michango ya waandishi wa habari wanaokwenda vitani, wanaokwenda kwenye maeneo mbalimbali ya kupambana na majambazi, wanaokwenda kuibua matatizo ya kijamii tunawapa nishani gani, tunawashirikisha vipi kwenye sikukuu zetu za mashujaa au siku ya vyombo vya habari duniani ili kuthamini mchango wa waandishi wa habari. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa hilo. Lakini kwa bahati mbaya sikulisikia, naomba sasa nipatiwe ufafanuzi kabla sijaing'atua shilingi.

**MWENYEKITI:** Mmmh, hebu jibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kutoa ufafanuzi kidogo kwa Mheshimiwa Zaynab Vulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wako waandishi wa habari walioshiriki vita kina Ben Kiko, kina Juma Dihule na wengine wengi aliwataja kwenye swali lake. Lakini hoja ya msingi ni kwamba kwanza inategemea mambo mawili au matatu. Kwanza inategemea mikataba yao ya kazi wakati ule. Kuna wengine ambao tuna taarifa kwamba walilipwa na Jeshi baada ya kutoka vitani ni kama kifuta jasho chao. Lakini pale Wizarani hatuna kumbukumbu ya maandishi yoyote ya ambaye hajalipwa haki zake kutokana na kushiriki kwa vita yake katika vita ya Kagera. Lakini ikumbukwe kwamba pia na waandishi hawa walikuwa wanafanya kazi yao kama watumishi wengine. Ilikuwa ni wajibu wao pia kwa sababu kuna madereva walifia vitani, lakini wengi wa hawa walioathirika katika vita ya Kagera walilipwa na Jeshi la Wananchi wakati ule. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nilipokuwa nachangia kwa maandishi pamoja na kuunga mkono hoja ya Serikali ya kuiwezesha TUT kutimiza wajibu wake wa msingi nilieleza kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ina wajibu wa kuwashirikisha pia wadau pale yanapotokea malalamiko na Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu hoja fulani hapa mbele alieleza kwamba waliamua tujibu mapigo. Lakini nilikuwa nataka tu kuomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa bosi wangu Waziri wa sasa wa Habari, Utamaduni na Michezo kwamba pengine Serikali haioni kwamba ni busara na hasa Wizara hiyo ambayo ndiyo ina mamlaka ya vyombo vya habari kuwaita wadau hao ili pengine kujua chanzo na msingi wa malalamiko kwa sababu kwa muda mrefu sasa ninaamini kwamba Serikali imekuwa ikiiwezesha TUT na hapakuwepo na malalamiko kwa wamiliki wa vyombo vya habari. Pengine kwa kuwaita wataweza kujua

chanzo cha malalamiko haya na kuyamaliza kwa nia ya kuweka mshikamano wa pamoja wa wadau wa sekta ya habari. Nilikuwa nataka kujua kama Waziri analionaje hili kwa nia ya kuweka mshikamano na kuiruhusu TUT iweze kutimiza wajibu wake wa msingi kwa kulinda maadili na umoja wa Kitaifa kama chombo kinachotegemewa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nielezee mapigo hajanielewa bwana. Nasema wenzetu wa *MOAT* hawakutaka kuonana na sisi wala TUT wakaamua waende kwenye vyombo vya habari na sisi tukaamua tutumie vyombo vya habari hivyo kwa kujibu mapigo. Lakini tuko tayari kuwasikiliza kuhojiana nao kukutana nao kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, zungumza tulikusahau, huku hukuandikwa. Endelea tafadhali ila kwa kifupi sana.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru naona leo nina bahati mbaya sana kwa sababu jina langu limesahauliwa na wewe umenisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nimechangia kwa maandishi kwenye mchango wangu nilikuwa nimezungumzia mambo matatu muhimu. Kwanza, nilisema suala la dharau nikazungumza habari ya ukiritimba halafu nikasema suala zima la uvunjaji wa Katiba katika Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo uliofanyika katika kipindi cha miaka 43 iliyopita. Hili linagusa moja kwa moja uvunjaji wa Katiba katika Chama cha Soka cha Tanzania *(TFF)* zamani kilikuwa *FAT*. Nilikuwa nikitegemea maelezo kutoka kwa Waziri au Naibu Waziri lakini sikupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi namwomba sana Waziri basi anisaidie kwamba hivi sasa ni kipindi cha miaka 43, *TFF* wanafanya kazi ya kuiwakilisha Tanzania bila ya ridhaa ya Zanzibar, wanafanya kazi hiyo bila ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kuwaruhusu, lakini pia wanatumia fedha za Shirikisho la Mpira la Ulimwengu bila ridhaa ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *TFF* bila ya ridhaa ya Zanzibar wanatumia misaada inayotolewa na *FIFA Gold Project* mfano hai ni pale katika nyasi ambazo zimeletwa hivi sasa. Nyasi zilizoletwa ni *Gold Project* kutoka *FIFA,* Zanzibar hawamo. Sasa katika mchango wangu nikawaambia hivi Mheshimiwa Waziri utakapokuja kunijibu mambo yafuatayo naomba yatekelezwe ili Zanzibar iweze kupata sehemu yake. La kwanza, namwomba tena sasa hivi anijibu hivi hivi nilivyomwomba. Kwanza kwa sababu miaka 43 imetumika Tanzania Bara na *FAT* sasa Ofisi za Shirikisho la Mpira zihamie Zanzibar.

La pili, msaada wa nyasi za uwanja zilizoletwa hivi sasa basi sehemu moja iende katika uwanja wa Mao Tse Tung, Zanzibar. Tatu, liundwe Shirikisho halali la Mpira wa Miguu katika Tanzania. *FAT* wafanye kazi zao za Bara na *ZFA* wafanye kazi zao Zanzibar. La mwisho, mgao wa fedha za *FIFA* ambazo ni dola 250,000 zigawiwe sawa sawa katika vyama hivi viwili.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea naomba ujibu kwa kifupi sana, kuhusu nyasi usijibu kwa sababu zilikuwa za kiwanja kile utapelekaje huko tena.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kumjibu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, madai yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwamba Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na *TFF* hawana dharau ya aina yoyote kwa Zanzibar na wala hatujavunja Katiba. Nilitaka niliweke hili wazi kabisa na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwamba Wizara yangu tumeshafanya vikao vingi tu kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Zanzibar na Bara kwa ushirikiano wa ujirani mwema. Vivyo hivyo *ZFA* na *TFF* wana vikao vyao tena vingi ambavyo wangeweza kumalizana wenyewe haya yanayozungumzwa kwa hatua ya vyama na ndio utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi *TFF*. Tulikuwa tunakutana Zanzibar na ndiyo maana hata timu hii ni ya Muungano, kuna wachezaji Zanzibar, Kocha Ali Bushir anatoka Zanzibar, Maximo tumemwajiri wote, kwa hiyo, si kweli kwamba haya yote kuna ubaguzi au kuna dharau ya aina yoyote.

Kuhusiana na *FIFA, FIFA* Kikatiba wanafahamu Tanzania. Tanzania maana yake Zanzibar imo na ndio utaratibu wenyewe. Hii miradi aliyoizungumza ya *GO.* Tumepata miradi ya *GO* ya kujenga Hosteli ya Karume ni mpango maalumu wa *FIFA* kwamba kwanza waanze na hosteli na nyasi bandia wametupa uwanja wa Taifa na wakasema Karume kwa sababu ni *training centre* waweke. Sasa hivi tumeshawaelekeza *ZFA* na *TFF* wawe na vikao kwamba msaada mwingine wa *FIFA* utakapokuja uende Zanzibar na unakuja. Kwa hiyo, ninamwomba avute subira, nchi hii ni moja, tutashirikiana katika kuendeleza michezo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 259,510,800/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 251,071,500/=
Kifungu 6001 – *Culture and National Languages* ... ...Sh. 1,794,095,500/=
Kifungu 6004 – *Sports Development*... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,647,145,000/=
Kifungu 7003 – *Information Services* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 6,074,987,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo**

Kifungu 6001 - *Culture and National Languages* ... Sh. 1,500,000,000/=

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho kifungu kidogo cha 6364 – Mfuko wa Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 74, kiambatasho cha sita ambao ni mgao wa msaada kimaeneo, kifani na kimkoa kwa mwaka 2006/2007, mgao huu haueleweki, ulitumia vigezo gani?

Kwa mfano ukiangalia mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Singida, Tabora na Tanga ilipata mgao kwa fani moja tu. Vile vile ukiangalia mikoa mingine Shinyanga, Rukwa na Iringa haikupata mgao kabisa na wakati huo huo Mkoa wa Dar es Salaam ulipata mgao kwa fani zote na kwa vikundi 27 na ambapo walitumia karibu asilimia 46 ya fedha zote. Kwa hiyo, kwa tafsiri ya haraka haraka unaweza ukaona kwamba labda kigezo kilichotumika pengine ni ule mtindo wa mjanja kupata. Ningependa tu kujua Mheshimiwa Waziri atueleze kwa mwaka huu ambapo tuna shilingi milioni 200 Wizara itatumia utaratibu gani katika kugawa hilo fungu?

**MWENYEKITI:** Hilo ndilo swali. Basi tunaendelea.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kutoa ufafanuzi kidogo wa swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura kama ifuatavyo:-

Kwanza, niseme tu kwamba fedha hizo za Mfuko utaratibu wake ni wasanii wenyewe kuziomba pale walipo. Kuna Kamati maalumu ya mfuko na kuna vigezo maalumu ambavyo vimewekwa na mfuko ambavyo ndio vinaangalia ni nani hasa wanastahili kupata fedha hizo. Kazi kubwa kwamba fedha hizi zinatolewa ili kuendeleza fani hii ya sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, katika hizi shilingi milioni 200 ni kuhimiza vikundi vingi vya sanaa katika mikoa mbalimbali vijitokeze kwa wingi. Lakini ni kweli mikoa mingi ya pembezoni ambayo kwa muda mrefu wamekuwa au hawaujui mfuko kama upo tumetoa mwito sana kupitia kwa Wabunge au kwenye Kamati yetu kwamba vikundi viombwe kuomba na taratibu zitafuatwa na taratibu ni za wazi kabisa wala hazina ubaguzi wowote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6004 – *Sports Development*... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,741,000,000/=
Kifungu 7003 – *Information Services* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 750,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*
*Bunge lilirudia*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2007/2008 ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na kupitisha bila ya mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe. Kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba tumekwenda kwa *speed,* sikupenda kurudia kwa sababu haina maana tunakaa na mtu mmoja kwa saa zote halafu tunaingia *guillotine* nayo pia haina heshima yake. Kuna maswali mengine ukiyauliza majibu hayawezi kubadilika ni kama yale yale. Kwa hiyo, tumeona afadhali kuliko kurudia na kurudia halafu tukafikia kulipitisha fungu dakika mbili sio vizuri sana. Kwa hiyo, wale ambao walijisikia kwamba walitaka kuendelea kubishana hawakupata nafasi sababu kubwa ni hizo. *(Makofi)*

Sasa nina matangazo Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, anapenda kuwatangazia wajumbe wa Kamati yake ya Fedha na Uchumi kuwa kesho tarehe 8 Agosti, 2007 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitafanyika saa 4.00 asubuhi chumba namba 428 ghorofa ya nne. Kwa hiyo, wajumbe wake msikose ni wakati mzuri wa kuweza kufikiria shughuli za kikazi. *(Makofi)*

Halafu tua tangazo lingine limetolewa na Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwamba kesho Wabunge wote wawe wa Chama cha Mapinduzi na wengine wanaopenda saa 5.00 asubuhi kule Kiliamani kutakuwa na *harambee* ya ujenzi wa Ofisi ya Tawi la CCM lililoko Dodoma, Mtaa wa Nyerere ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa mgeni rasmi, kwa hiyo, watu wenye mapenzi mema wote wanakaribishwa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo kama mtakavyofahamu kesho ni Sikukuu ya Wakulima kawaida kwa utaratibu wetu hatuna shughuli za Kibunge zinaweza kuwepo shughuli nyingine lakini shughuli za Kibunge hazipo, kwa hiyo, Waheshimiwa nasitisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Alhamisi tarehe 9 Agosti, 2007 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.37 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 9 Agosti, 2007 saa tatu asubuhi)*